

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MKUTANO WA KUMI NA NANE

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

Kikao cha Nane – Tarehe 3 Februari, 2010

D U A

Naibu Spika (*Mhe. Anne S. Makinda*) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 79

**Uhamishaji wa Rasilimali Watu Katika Mpango
wa Kupeleka Madaraka kwa Wananchi**

MHE. JOHN P. LWANJI aliuliza:-

Kwa kuwa, katika mpango wa kupeleka madaraka kwa wananchi (*Decentralization by Devolution*) Serikali iliahidi kuhamishia Mikoani na kwenye Halmashauri za Wilaya shughuli na miradi mbalimbali pamoja na rasilimali zinazohusika:-

- (a) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa, katika kutekeleza hilo imefanikiwa kuhamisha rasilimali fedha na kushindwa kuhamisha rasilimali watu na kusababisha upungufu wa watumishi kwenye shule, zahanati na kadhalika?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa, hali hiyo inakwamisha mpango mzima wa “D” by “D” kama vile mipango mingine mizuri ya maendeleo iliyowahi kukwama?
- (c) Je, ni hatua zipi za makusudi zinazochukuliwa katika kuoanisha rasilimali fedha na rasilimali watu katika Mpango wa “D” by “D” ili uende kadri ulivyokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, “*Decentralization by Devolution (D by D)* Sera ya Serikali ya kupeleka Madaraka kwa Umma. Katika kupeleka Madaraka kwa Umma masuala manne yanazingatiwa ikiwa ni pamoja na rasilimali watu na rasilimali fedha. Rasilimali hizo zinapelekwa katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa upande wa kupeleka rasilimali fedha nchi yetu imefanikiwa kwa kiasi fulani kwa sababu Serikali imejitahidi kupeleka fedha ngazi ya Halmashauri na hivi sasa fedha zinapelekwa hadi ngazi ya Vijiji. Vile vile, nakubali kuwa kwa upande wa rasilimali watu tunayo changamoto kwa sababu bado katika maeneo mbalimbali uko upungufu wa wataalam wanaohitajika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na upungufu uliopo wa watumishi, Serikali inajitahidi kuhakikisha kuwa Sera hii inaendelea kutekelezwa bila kukwama. Uhaba wa watumishi wenye sifa unaotokana na vigezo vya kuwapata watumishi.

Kwa mfano kumpata Daktari ni lazima asome miaka mitano (5). Watumishi wengine vile vile, hutakiwa kwenda mafunzoni na kufuzu kabla ya kuajiriwa. Aidha, watumishi kufariki dunia na wengine kutopendelea kufanya kazi katika maeneo ya pembezoni ni baadhi ya sababu zinazochangia upungufu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto hizo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Sera ya Kupeleka Madaraka kwa Umma haitakwama kwani Serikali imeshajipanga kukabiliana nazo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za makusudi zinazochukuliwa ili kuoanisha rasilimali fedha na rasilimali watu katika Sera ya Kupeleka Madaraka kwa wananchi ni pamoja na:-

(i) Kuwaendeleza watumishi kitaaluma. Kwa mfano Wizara ya Fedha imekuwa inasomesha Wahasibu katika ngazi mbalimbali za taaluma ya kiuhasibu pamoja na mifumo mbalimbali inayotumiwa na Serikali katika usimamizi na udhibiti wa fedha za umma.

(ii) Kuajiri watumishi wanaohitimu Vyuoni moja kwa moja katika Sekta ya Afya, Elimu, Fedha na Kilimo.

(iii) Serikali imeanzisha utaratibu wa kuhakikisha kuwa watumishi wanaoajiriwa wanaendelea kubaki katika maeneo ya kazi kwa kufanya yafuatayo hususan kwenye maeneo yenye mazingira magumu.

· Kujenga nyumba za watumishi;

· Kuweka nishati ya jua katika Zahanati na Mashule; na

· Kununua boti ili kurahisisha usafiri kwa maeneo zinapohitajika.

(iv) Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga katika Vyuo mbalimbali ili hatimaye ipatikane idadi kubwa ya wahitimu hususan katika Sekta za Elimu, Afya na Kilimo.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa baada ya kupiga kelele kuhusu shule zetu za Kata, Serikali imekuwa na mwelekeo mzuri wa kuweza kuwapeleka walimu katika shule hizo. Mimi nachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa hatua hiyo.

NAIBU SPIKA: Uliza swali la nyongeza usitumie sana hotuba!

MHE. JOHN P. LWANJI: Ndiyo.

NAIBU SPIKA: Unauliza maswali sio hotuba.

MHE. JOHN P. LWANJI: Lakini katika shule zetu hizi zilizobaki za msingi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendesha *crash programme* ya kunusuru upungufu mkubwa uliopo katika shule zetu za msingi pamoja na upande wa zahanati zetu na pia Maofisa Ugani upande wa kilimo ambacho sasa hivi tunakipigia kelele tuwe na kilimo pale.

Swali la pili, katika Wilaya yangu ambayo hali si nzuri kijiografia na kwa kweli kutokana na tatizo hilo kuna upungufu mkubwa wa watumishi. Serikali ina mpango gani maalum hasa katika Wilaya yangu na jimbo langu la Manyoni Magharibi kuhakikisha kwamba shule hizo pamoja na Maafisa ugani na wengine wanapelekwa haraka iwezekanavyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kushukuru sana kwa pongezi ambazo amezitoa kwa Serikali na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nataka kusema kwamba tunashukuru kwamba Mbunge ameona hilo. La pili, anachozungumza Mheshimiwa Mbunge anazungumzia habari ya kuwa na *crash programme*. Ukizungumza habari ya *crash programme* unazungumza utaratibu ambao unaweza ukasababisha watumishi hawa wakapatikana kwa haraka zaidi kuliko utaratibu ulioko kwa sasa hivi.

Lakini wakati tunapofanya hivyo ni vizuri pia kukumbuka pia tunaangalia ubora wa huduma itakayokwenda kutolewa kule. Mtakumbuka hapa nyuma kwamba walimu walikuwa wanapelekwa vyaoni wanakaa kwa miezi 2 halafu wanarudi wanakwenda kufundisha, halafu wanakaa tena kidogo wanakwenda, hivyo hivyo imekuwa ni malalamiko yake na watu wengine wame-*criticise* kusema kwamba huu utaratibu unatuletea mambo ambayo kwa kweli yanapunguza *quality* ya elimu. Lakini nataka niseme kwamba Serikali inaliona hili tatizo analolizungumza na ndiyo maana tumesema

kwamba kumekuwa na mazingira yale ambayo tumeyaona ni magumu tuhakikishe kwamba tunawapeleka walimu kule kwa kutoa motisha na wengine ili waweze kusaidia katika yale maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ameulizia kuhusu namna gani ambapo tunaisaidia Halmashauri yake ya Wilaya ya Manyoni, labda nimpe takwimu tu kama Mheshimiwa Naibu Spika utaniruhusu?

NAIBU SPIKA: Usichukue muda mrefu sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Kifupi sana.

Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 watumishi 3,654 walipangwa katika Halmashauri kwa mchanganuo ufuatao. Wizara ya Kilimo watumishi 856, Wizara ya Mifugo na Uvuvi watumishi 168, Fedha na Uchumi 250, Afya watumishi 2,380 na Serikali inashirikiana na asasi nyingine kuhakikisha kwamba sasa hivi kwa mfano sekta binafsi. Mashirika ya Dini yote haya yanatusaidia katika kuhakikisha kwamba hawa watumishi ambao anaowazungumzia wanapatikana ili kutoa huduma katika maeneo hayo.

Na. 80

Msaada Kutoka Nchi ya China Kwa Tanzania

MHE. PAUL P. KIMITI aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi karibuni Rais wa China alitembelea Tanzania na kuahidi kuisaidia nchi yetu katika sekta mbali mbali:-

- (a) Je, ni maeneo yapi ambayo nchi hiyo imeahidi kusaidia na kwa kiwango gani?
- (b) Je, ni kweli kuwa wananchi wa China ambao wameanza kuingia nchini kwa wingi wana vibali vya kuishi na kufanya kazi wanazozifanya?
- (c) Je, dawa na vipodozi vingi vya Kichina vilivyoenea nchini vimefanyiwa uchunguzi na kujua athari zake kwa afya ya binadamu?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMEIAH S. SUMARI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mbunge wa Jimbo la Sumbawanga Mjini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kufuatia ziara aliyoifanya Rais wa China hapa nchini tarehe 14 – 16 Februari, 2009, China imeahidi kusaidia na kushirikiana na Tanzania katika maeneo yafuatayo:-

(i) Uanzishwaji wa Benki ya Kilimo;

(ii) Kuimarisha miundombinu ya reli ya TAZARA kwa gharama ya kiasi cha shilingi bilioni 53.0;

(iii) Upanuzi wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Zanzibar kwa gharama ya kiasi cha shilingi bilioni 93.5;

(iv) Kushiriki uwekezaji kwenye Sekta ya Kilimo na Uvuvi;

(v) Kushiriki kwenye Sekta ya Nishati na Madini; na

(vi) Kushiriki katika ujenzi wa miundombinu ya teknolojia ule Mpango wa Taifa awamu ya pili ambao kwa sasa unakadiriwa kwamba utagharimu shilingi bilioni 132.9.

Makubaliano hayo bado uchambuzi wake unafanyiwa kazi kwa lengo la kutuwezesha kufahamu ni kiasi gani kamili cha fedha kitahitajika na kitapatikana kutoka China. Aidha, ahadi hizo zitakuwa kwa njia ya misaada, mikopo ya masharti nafuu, uwekezaji wa moja kwa moja au uwekezaji wa pamoja.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana imekuwa ikipokea maombi kutoka kwa raia wa China ya kutaka kufanyakazi hapa nchini katika sekta mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu na biashara. Baadhi ya maombi hukubaliwa na mengine hukataliwa. Kwa hiyo, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

(c) Wapo raia wa China ambao wana vibali vya kuishi na kufanyakazi nchini.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 51 cha Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003, dawa yoyote ili iweze kutumika nchini ni lazima isajiliwe na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA). Usajili hufanyika baada ya kufanyika kwa uchunguzi wa ubora, na usalama wa dawa husika, ikiwa ni pamoja na uhakiki juu ya utengenezaji wake kwenye kiwanda husika. Mamlaka imekwisha kusajili jumla ya dawa na vipodozi 335 kutokana na Viwanda vya Madawa vya China.

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa inayoonekana kuwa na athari kwa matumizi ya binadamu bila ya kujali inatoka wapi, haipewi usajili, hivyo kutokuruhusiwa kutumika nchini. Hata hivyo, wapo wafanyabiashara ambao sio waaminifu na wengine, kwa kutokuwa makini, huingiza dawa au vipodozi nchini ambavyo haviko kwenye daftari la usajili. Ili kuweza kunusuru maisha ya wananchi, Mamlaka ya Chakula na Dawa hufanya uchunguzi wa kina mara kwa mara kwenye maduka ya dawa na vipodozi na

wanapobaini uwepo wa dawa na vipodozi ambavyo havijasajiliwa nchini, Mamlaka huchukua hatua kwa mujibu wa sheria.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana aliyoyatoa. Lakini pia nitumie nafasi hii kumpongeza na kumshukuru sana Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa jinsi anavyojitahidi kutafuta misaada nchi mbalimbali bila ya ziara zake anazotoka nchi za nje asingeweza kupata misaada mikubwa kama hii, swali la kwanza.

Kwa kuwa Serikali ya Uchina imekubali kurekebisha na kukarabati reli kutoka Tunduma mpaka Kapirimposhi.

Je, Mheshimiwa Waziri utakubaliana nami ya kwamba kwa kuwa faida ya reli hiyo iko zaidi kutoka Dar es Salaam mpaka Tunduma na sio mpaka Kapirimposhi. Je, isingekuwa vizuri ili kupata biashara nzuri kutoka Congo iwepo reli ya kutoka Tunduma mpaka Kasanga ili tuweze kupata biashara nzuri kutoka upande wa Congo?

Inaonekana wako Wachina Wamachinga wamekuwa wengi sana hapa. Je, isingekuwa utaratibu sasa kupitia upya kuona maombi yao kama kweli yamekuja kwa nia hiyo ya kuwekeza au wengine wafanyabiashara.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge Paul Kimiti, Mbunge wa jimbo la Sumbawanga Mjini kwamba lingekuwa jambo jema sasa kujenga reli kutoka Tunduma mpaka Kasanga ili tuweze kuvuna kutoka Congo Serikali imesikia ushauri wake na kwa sababu ujenzi wa miundombinu ni moja ya vipaumbele vyetu nina imani kwamba Serikali itachukua hatua zinazofaa kutokana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge.

Ushauri wake wa pili, ninataka kumhakikishia vile vile kwamba tunakubaliana naye. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri kusema kwamba mna imani si mngesema ndiyo mnafanya.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kutoa maelezo machache ifuatavyo kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Paul Kimiti.

Kwa hakika haipendezi kutaja wafanyabiashara tulionao katika miji yetu ya Dar es Salaam kwa majina ya nchi ile wanazotoka, hasa kwa nchi rafiki kama China. Pale kuna Wapakistani, Wabangladesh, Wahindi, Wa-senegal, Wa-nigeria kwa kweli sio vyema sana kwenye jengo, kwenye nyumba kubwa kama hii ambayo tunaangaliwa duniani pote kutaja watu kwa makabila ya nchi wanazotoka.

NAIBU SPIKA: Haya tuseme Wamachinga kutoka nje ya nchi.
(*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi hii fupi ya kuongezea jibu katika swali zuri alilouliza Mheshimiwa Kimiti na kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na alichosema Mheshimiwa Waziri Marmo lakini ningependa kusema kwamba inapendeza vile vile siku moja kuona kwamba Kariakoo inakuwa Hongkong ya Afrika ambapo watu wote tunaweza kuja kununua bidhaa Kariakoo kutoka nchi mbalimbali za Afrika na ndicho kinachofanyika sasa hivi. Kuhusu wananchi wa nje kufanya kazi ya Umachinga au kufanya biashara ndogo ndogo kazi kubwa imefanywa kati ya Wizara mbalimbali kuona kwamba vibali vya ukaazi, vibali vya biashara na shughuli zinazofanyika na wananchi wa nje zinaangaliwa vizuri zaidi na kuona kwamba hawachukui biashara ya Watanzania walio na biashara ndogo ndogo pamoja na hivyo tumekubaliana na Waziri wa Biashara wa China alivyokuwa nchini kwamba ni vizuri sasa kuwa na *Industrial Parks* inazunguka Dar es Salaam ili badala ya kuchukua bidhaa kutoka China sasa bidhaa hizo zinatengenezwa na Watanzania wakishirikiana na wenzao kusudi Kariakoo iwe kweli Hongkong ya Afrika.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi na yale ya Mheshimiwa Marmo na Mheshimiwa Nagu napenda kuongezea kidogo kwenye swali la kwanza la nyongeza la Mheshimiwa Kimiti. Kwanza sio kweli kwamba makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na China ni ya kurekebisha reli kutoka Tunduma mpaka Kapirimposhi. Makubaliano ni reli nzima kutoka Dar es Salaam mpaka Kapirimposhi. (*Makofi*)

L Serikali ya Tanzania na Serikali ya Zambia sasa hivi inafanya utafiti wa kuhakikisha Lubumbashi inaunganishwa na Tunduma. Kwa hivyo ombi hilo tayari limeshafikishwa kwa Serikali ya China na China italeta timu mbili mwezi wa tatu, timu moja ya kitaalamu, timu moja ya masuala ya fedha ili kutazama hayo yote na kuhakikisha kwamba reli hii kwanza inarekebisha kutoka Dar es Salaam mpaka Kapirimposhi na vile vile tunaangalia uwezekano wa kufungua *Southern DRC* kwa *TAZARA* na *Port* ya Dar es Salaam.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana maswali ya nyongeza mengine hayatakuwepo kwa sababu wamejibu na wakauliza wenyewe haya.

Na. 81

**Kampuni za Bima Kucheleweshwa Fidia
kwa Waathirika**

MHE. ATHUMANI S. JANGUO aliuliza:-

Kwa kuwa, Bima hutumiwa kwa kuweka tahadhari ya maisha au vyombo vinavyotumiwa na anayelipia Bima kama Magari, Majengo, Bima ya Maisha na Kinga ya ajira ili inapotokea ajali, kuungua, kuibiwa, kufa au kukosa ajira mwathirika aweze kufidiwa; na kwa kuwa, Kampuni za Bima hufanya tathmini ya thamani kwa vitu vinavyowekewa Bima kisha kuweka viwango vya kulipia kila mwaka:-

(a) Je, kwa nini Kampuni za Bima zinashindwa kufidia kikamilifu hasara mara inapotokea ajali kabla ya kufanya tathmini mpya wakati thamani ya mali iliyowekewa Bima ilikwishakubaliwa na pande zote mbili tangu mwanzoni?

(b) Kwa kuwa, mara nyingi tathmini inayofanywa baada ya *grid* huwa chini ya thamani iliyomo ndani ya Mkataba. Je, sababu zake ni nini?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE):
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Athumani Saidi Janguo, Mbunge wa Jimbo la Kisarawe, lenye sehemu (a) na (b), naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bima ni Mkataba wa makubaliano kati ya mteja na Kampuni ya Bima. Lengo kuu Mkataba wa Bima ni kumkinga mteja dhidi ya majanga yanayoweza kutokea.

Mkataba wa Bima umeweka utaratibu wa kufidia majanga ambayo yameorodheshwa ndani ya mkataba. Majanga hayo ni pamoja na moto, kifo, wizi au uharibifu wa mali na ajali nyingine yoyote. Hata hivyo, ili mkataba utambuliwe kisheria, lazima mteja awe amelipa ada yake ya bima kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Athumani Saidi Janguo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kuna aina mbili za Bima. Bima ya maisha ambayo hakuna tathmini inayoweza kufanyiwa kutokana na ukweli kwamba thamani ya maisha ya binadamu haifahamiki. Aina nyingine ya Bima ni ile ya uharibifu wa mali na ajali.

Katika bima ya uharibifu, Kampuni ya Bima haiwajibiki kufanya tathmini ya mali itakayowekewa bima, ila ni mteja ndiye hulazimika kutaja thamani ya mali yake. Kwa maana hiyo, tathmini inayofanywa na Kampuni ya Bima mara baada ya ajali kutokea, hufanywa kwa lengo la kuthibitisha hasara iliyotokana na janga kabla ya kuandaa malipo stahili ya fidia, ambayo yatamsaidia mteja kuirejeshea mali yake katika hali iliyokuwapo awali. Utekelezaji huu ni kwa mujibu wa mkataba wa bima.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kuna baadhi ya Makampuni ya Bima huchelewa kulipa malipo ya fidia bila ya sababu yoyote ya msingi na hivyo kupelekea usumbufu mkubwa kwa wateja.

Serikali tayari imeliona tatizo hilo na ndio maana Sheria ya Bima Namba 10 ya mwaka 2009, kifungu Namba 131, kinampa Mamlaka Kamishna wa Bima kuchukua hatua za kisheria dhidi ya Kampuni ya Bima itakayoshindwa kulipa fidia ya bima ndani ya siku 45.

Aidha, kifungu Namba 122 cha sheria hiyo, kinampa idhini Waziri anayesimamia masuala ya Bima, ya kuunda Mahakama ndogo ya bima inayoshughulikia malalamiko ya wateja wa bima dhidi ya makampuni ya bima.

MHE. ATHUMANI S. JANGUO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ambaye anaeleza hali halisi ilivyo ningeomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa tathmini ya hasara ya ajali hufanywa na watu wanaoitwa *accessors* ambao huteuliwa na Makampuni ya Bima bila ya idhini ya mteja. Kwa hiyo matokeo yake huwa wanapendelea sana kutoa thamani ambayo inapendelea Kampuni ya Bima badala ya kutoa tathmini ambayo inalenga kuthibitisha hasara iliyopatikana. Je, Serikali iko tayari kufanya marekebisho ili hawa *accessors* wawe wanateuliwa kwa makubaliano ya pande zote mbili.

Pili, pamoja na Sheria Na. 10 ya 2009 ambaye ameisema Mheshimiwa Waziri bado tatizo linaendelea la kuchelewa na kufidia kidogo. Waziri ataweza kuliambia Bunge hili kwamba tangu Oktoba mwaka jana hadi leo ni masuala mangapi ambaye yameamuliwa na huyo Kamishna wa Bima na kwamba yeye mwenyewe ameshateua Mahakama Ndogo ngapi kushughulikia suala hili.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda tufahamiane Mheshimiwa Janguo kwamba mteja anapoweka thamani ya kitu chake anachokiweka bima maana yake nini? Maana yake kama imetokea hasara, hasara hiyo haiwezi ikarekebishika mteja huyo anapaswa kulipwa ile *amount* ambayo ameiweka.

Kwa mfano kama gari limeibiwa kabisa ushahidi umethibitika kwamba gari ile haipatikani ile thamani uliyoiweka ndiyo unapaswa kurejeshewa. Kwa maana hiyo hata kama ukisema unataka kurekebisha sheria kwa maana kwamba huyo *accessor* iwe ni makubaliano baina ya mteja na Kampuni tutabidi turudi kwenye mkataba, mkataba wenu unasema vipi.

Pili, tatizo la kuchelewa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa sina idadi ya Makampuni mangapi ambayo Kamishna ambayo tayari ameshayachukulia hatua lakini nitamtafutia na tutaweza kumpatia ili kuweza kujua ni Makampuni mangapi ambayo ameshayachukulia hatua.

Kwa upande wa Mahakama kama nilivyoeleza Waziri mwenye mamlaka ya masuala ya Bima ndiyo mwenye mamlaka ya kuweka hiyo Mahakama ndogo na hivi sasa wanamalizia hizo kanuni ili Waziri aweze kuitangaza hiyo Mahakama ndogo ambayo itashughulikia malalamiko ya mteja na Makampuni ya Bima.

Na. 82

Upungufu wa Umeme na Miundombinu Chakavu

MHE. JENISTA J. MHAGAMA (K.n.y. MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi karibuni kumekuwa na taarifa mbalimbali zinazowatisha wananchi juu ya upungufu wa umeme na miundombinu chakavu katika mfumo wa umeme wa Tanzania' na kwa kuwa, *TANESCO* kupitia *strategic plan* yake iliweza kujipatia mkopo wa takribani bilioni 300 kwa ajili ya kuboresha hali hiyo:-

Je, ni maeneo yapi yamefanyiwa kazi mpaka sasa?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ilikabiliwa na tatizo la mgao mkubwa wa umeme kuanzia mwezi Februari, 2006 hadi mwezi Desemba, 2005. Mgao huo uliongeza gharama kwa *TANESCO* kwa kuwa mauzo ya umeme yalipungua, manunuzi ya umeme kutoka kwa wazalishaji umeme wa binafsi yaliongezeka, gharama kubwa za kuzima na kurudisha umeme, uharibifu wa vifaa vya kuwasha na kuzima umeme na malipo ya masaa ya ziada kwa watendaji. Malalamiko ya wateja yaliongezeka kutokana na kutoridhika na huduma itolewayo na shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kunusuru utendaji wa Shirika, *TANESCO* iliandaa mpango ulioitwa *Five Year Financial Recovery Plan*, ambao ulikuwa ni mpango wa miaka 5 ya kunusuru Shirika. Mpango huo ulilenga kulipa madeni kwa wazalishaji binafsi wa umeme na kununua vifaa vya ujenzi wa njia za umeme ili kuongeza ufanisi katika utendaji.

Kupitia mkopo wa takriban shilingi bilioni 300 Shirika limeweza kununua vifaa vya kutosha na kutekeleza mpango wa kuunganisha wateja 100,000 kila mwaka. Wateja wapya waliunganishiwa umeme kwa mwaka 2007 walikuwa 32,180, mwaka 2008 (56,383) na wateja 59,547 mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine ni uunganishwaji wa waombaji wapya wa umeme ndani ya siku thelathini.

Vile vile, Shirika limeweza kukarabati miundombinu ya usafirishaji umeme na usambazaji katika maeneo mbalimbali na linaendelea na mpango wa kupunguza upotevu wa umeme. Upotevu wa umeme umepungua kutoka asilimia 23 iliyokuwepo kwa mwaka 2006/2007 hadi asilimia 21 mwaka 2008/2009. Shirika pia limeimarisha usafiri kwa kununua magari mapya kwa ajili ya utekelezaji na usimamizi wa kazi za kusafirishia na kusambaza umeme.

Upotevu wa umeme umepungua kutoka asilimia 23 iliyokuwepo kwa mwaka 2006 hadi kufikia asilimia 21 kwa mwaka 2009. Shirika pia limeimarisha usafiri kwa kununua magari mapya kwa ajili ya utekelezaji na usimamizi wa kazi za kusafirishia na kusambaza umeme.

MHE. ENG. STELLA MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa mji wa Songea ni miongoni mwa maeneo ambayo yalistahili kunufaika na mpango huo wa ukarabati wa miundombinu; na kwa kuwa mji huo unakabiliwa na tatizo kubwa la umeme kutokana na mitambo yake kuwa chakavu. Je, Mheshimiwa Waziri ana mpango gani kunusuru hali hiyo katika mji wa Songea?

Kwa kuwa Mji wa Mbinga hivi karibuni ulipewa mashine zenye Megawatt 2 lakini mpaka sasa ni megawatt 0.5 tu ndiyo inatumika kutokana na wateja wake kutokuunganishwa. Je Wizara inampango gani wa kuhakikisha mashine hizo zinatumika kikamilifu na kupunguza hasara zinazojitokeza kwa kutembeza mashine bila wateja wa kutosha?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuimarisha huduma ya umeme katika mji wa Songea juhudi zinafanyika. |Sasa hivi tuna mpango ya muda mfupi ambao ni pamoja na kuendeleza ukarabati wa mashine zilizoko pale. Kwa mfano zile mashine za ABC ambazo ilifanyiwa *overhaul* kwa ujumla na tunaamini kwamba ndani ya siku chache zijazo zitakuwa zimeshakamilika na kurudisha hali ya huduma ya umeme katika hali ya kawaida.

Lakini nilishawahi kusema na narudia kusema kwamba Serikali ina mpango wa kununua *generator* nyingine ikiwa ni mpango wa muda mfupi katika hali ya kukabiliana na tatizo la umeme katika mji wa Songea Serikali inaendelea na mchakato ambao tunatarajia kukamilisha nao kabla ya mwezi wa sita tuwe tumeshakamilisha taratibu za kupata *generator* moja itakayowezesha sasa kuondoa hilo tatizo ambalo limekuwa likisababishwa na ubovu.

Kuhusu Wilaya Mbinga ni kweli ni kati ya Wilaya ambazo zinaziada ya vyanzo vya uzalishaji wa nishati ya umeme. Lakini changamoto iliyopo ni kwamba ziada hiyo haijatumika kwa sababu ya wateja wachache waliunganishiwa.

Tumekubaliana na Shirika la *TANESCO* tunaangalia utaratibu wa kuushirikisha Wakala wa Umeme Vijijini kuweza kuwasaidia Bajeti kuweza kuunganisha wateja wengi zaidi kwa sababu mashine zilizopo zinakuwa *under utilized* na hazitumii kikamilifu uwezo uliopo.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru swali moja dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa *TANESCO* kwa kushirikiana na Wizara wamefanya kazi nzuri sana kuhakikisha umeme umefika Peramiho na umeshaanza kuwashwa na Mheshimiwa Waziri anasubiriwa sana kwa sherehe kubwa ya kumpongeza; na kwa kuwa Waziri kwa kushirikiana na Wakala wa Umeme Vijijini *REA* wameanza kufanya kazi nzuri sana ya kufikisha umeme Madaba.

Je, kwa *speed* hiyo hiyo Mheshimiwa Waziri ataniambia kwamba atawahimiza *REA* kuhakikisha sasa ule umeme wa maji Madaba nao unaanza kufanyiwa kazi kama ulivyofanyiwa wa Peramiho?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nitafanya kama ambavyo ameomba. Tutawahimiza *REA* waharakishe kuweza kukamilisha kipande ambacho bado hakijaunganishwa. Lakini nipende kutumia nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Peramiho kupitia kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa ushirikiano ambao amekuwa akitupa na ni mmojawapo wa Wabunge wavumilivu sana katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Na. 83

Kijiji Kilichoko Jirani na Geita Gold Mine

MHE. ERNEST G. MABINA aliuliza:-

Kwa kuwa, kijiji cha Nyakabale ni miongoni mwa vijiji vilivyoathirika na mgodi wa *GGM*.

- (a) Je, kijiji hicho kimo ndani ya eneo lenye leseni ya *GGM*?
- (b) Je, mmiliki wa mgodi wa *GGM* ana uhalali gani wa kutupa vifusi na mawe karibu na kijiji cha Nyakabale?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina wa Geita lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lote la kijiji cha Nyakabale lipo ndani ya leseni za uchimbaji na utafutaji madini zinazomilikiwa na kampuni ya *Geita Gold Mining Limited*. Sehemu za kusini na mashariki mwa kijiji cha Nyakabale zipo ndani ya leseni ya uchimbaji madini - *Special Mining Licence SML 45/1999*, na sehemu iliyobaki ipo ndani ya leseni za utafutaji wa madini ambapo Kaskazini kuna leseni *PL* Na. 4872/2007 na magharibi kuna leseni *PL* Na. 1883/1999.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu Na. 38 cha Sheria ya Madini ya mwaka 1998 mwombaji wa leseni ya uchimbaji madini anatakiwa kuwasilisha

maombi yake yakiwa yameambatana pamoja na taarifa zingine. Mapendekezo ya namna atakavyotupa mabaki ya miamba inayotokana na uchimbaji kama ilivyobainishwa kwenye kifungu Na. 38 (c) cha Sheria ya Madini ya mwaka 1998.

Aidha kwa mujibu wa kifungu Na. 39 (d) cha Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 inabidi mwombaji aambatishe *Environmental Impact Assessment* na *Environmental Management Plan* inayoelezea pamoja na mambo mengine namna atakavyotupa mabaki ya miamba. Taarifa hizo ziliwasilishwa na Kampuni ya *Geita Gold Mining Limited* kupitia mamlaka husika na hatimaye leseni *SML 45/1995* kutolewa.

Ili kuhakikisha kuwa vifusi na mawe hayaleti madhara kwa wananchi wanaoishi karibu na mahali kwa wananchi wanaoishi karibu na mahali yanayotupwa kampuni inahakikisha utupaji wake unafanywa kwa kuzingatia *Environmental Impact Assessment* na *Environmental Management Plan* iliyowasilishwa na kupitishwa.

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza napenda nitoe pongezi ya *GGM* ambao wamekubali kuupa mji wa Geita maji kutoka Ziwa Victoria.

Kijiji cha Nyakabale mpaka sasa hivi kiko ndani ya leseni kama Waziri alivyoainisha na unakuta kwamba wananchi wa Nyakabale hawawezi kufanya kazi ya maendeleo kwa sababu wako ndani ya ile leseni. Je, kwanini Serikali isizungumze na *GGM* wale wananchi wa Nyakabale wakawa wabia au wakawa na share kwenye kampuni ya *GGM*?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunashukuru kwa pongezi ambazo ameipa Serikali lakini tunaomba turudishe shukrani za pekee kwa yeye Mheshimiwa Mabina kwa kuwezesha kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Geita kupatikana kwa ushirikiano ambao sasa umeimarika sana kati ya wananchi wa Geita lakini pia mgodi wa *GGM*. Mheshimiwa Mabina amekuwa mstari wa mbele miaka michache iliyopita hali haikuwa ya kuridhisha lakini sasa mahusiano haya yamekuwa mazuri na kwa kweli sisi kwa niaba ya Serikali tunampongeza sana na tunaomba Waheshimiwa wengine waendeleo na hilo.

Kwa ombi ambalo amelileta ninaamini kwamba Mheshimiwa anafahamu mazingira ya Kijiji cha Nyakabale yanaongozwa na Sheria zilizopo sasa. Ni kwamba Sheria sasa ya madini inaruhusu watu kuishi ikiwepo shughuli zingine zikiendelea kwa mfano ya utafutaji madini lakini pia kwa kuzingatia maelekezo na kanuni zingine kama za mazingira.

Mpango uliopo ni kwamba sasa hivi tunaboresha Sheria zetu kwa Sheria tunayotarajia kuiwasilisha Bungeni mwaka huu. Lakini pia mpango uliopo ni kuhakikisha kwamba makampuni yanayofanya kazi hapa hasa ambayo mitaji yake ni mikubwa kuweza kuyasajili katika Mamalaka zetu za masoko ya Hisa hapa Tanzania na hivyo ni namna mojawapo ya kuwashirikisha Watanzania. Lakini niseme kupitia Kamati ya mahusiano iliyopo kati ya Mji wa Geita pamoja na mgodi wenyewe kuna mambo mengi

ambayo wanaweza kuyafanya kwa manufaa ya wananchi, hasa wanaoishi katika mji wa Geita.

MHE. MOHAMMED H. MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wananchi hawa wa kijiji cha Nyakabale wameathirika kwa muda mrefu sana kwa milipoko, mitetemko na athari mbalimbali ambazo Serikali ina rekodi kamili. Je, ni fidia gani ya kiafya mgodi huu wa *GGM* unawapatia *special* kwa wananchi wa Nyakabale ambao wameathirika kwa muda mrefu wameshindikana kuhamishwa na kupewa eneo jingine?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niweke kumbukumbu sahihi. Kusema kwamba wananchi wengi wa Nyakabale na Geita wameathirika sana ni kauli ya jumla mno na tusingependa Watanzania na ulimwengu mzima uamini hivyo.

Kila linapotokea jambo uharibifu wowote kama tunavyosema siku zote kwa shughuli za madini na shughuli zingine zinaongozwa na Sheria zilizopo na kila jambo ambalo linafanywa lenye kuathiri mali zake linashughulikia kwa mujibu wa Sheria zilizopo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mbunge na Watanzania kwa ujumla kwamba kila inapojitokeza hivyo Sheria imechukua mkondo wake na fidia ama malipo kwa hayo madhara yamekuwa yakishughulikiwa kwa mujibu sheria zilizopo.

Lakini mojawapo ya namna ya kupunguza matatizo ya Mji wa Geita ni pamoja na Mheshimiwa Mabina alilosema. Sasa hivi Mgodi wa *GGM* ina mpango wa kuleta maji katika mji wa Geita ambao utarahisisha pamoja na mambo mengine kupunguza matatizo ya kiafya ambayo yanayotokana na maji ambayo siyo salama na bora.

Na. 84

Utafiti wa Madini Nyakafuru

MHE. EMMANUEL JUMANNE LUHAHULA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilipojibu swali linalohusu watafiti wa madini Nyakafuru Wilayani Bukombe, mwaka 2006 na Kampuni ya *Resolute Co. Ltd* ilisema kuwa leseni yao itasaidia Julai, 2007:-

- (a) Je, kama hawajapata Madini ya kutosha, kwanini wasiwaachie wananchi waendeleo kuchimba kwa lengo la kuboresha maisha yao?
- (b) Ikiwa kampuni ya *Resolute* imesema kuwa hakuna Madini ya kutosha huko Nyakafuru na wakati huo huo wamechukua hatua ya kuihamisha Sekondari iliyoanza kujengwa Bukandwe wakidai kuwa mahali shule ilipojengwa pana madini. Je, Serikali inasemaje kuhusu hilo?

- (c) Je, ni maeneo yapo yenye migodi/ watafiti wa madini yana mahusiano mazuri kati ya wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo wadogo wananchi wa maeneo yapi hayana mahusiano mazuri na kwa nini hakuna mahusiano hayo mazuri.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Jumne Luhahula, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, utafutaji wa madini katika eneo lijulikanalo kama Nyakafuru *Project* unafanyika kwenye eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 390.5 lenye leseni za utafutaji madini ishirini ikiwemo leseni namba *PL 1549/2000* kampuni ya *Sukuma Mines Limited* iliyotolewa tarehe 5/7/2000.

Mradi huo unaendeshwa kwa ubia kati ya Kampuni ya *Mabangu Mining Limited* (66%) ambayo ni kumpuni tanzu ya *Resolute (Tanzania) Limited*, pamoja na kampuni ya *IAM Gold Tanzania limited* (34%) ambayo ni kampuni tanzu ya kampuni ya *Spinifex Gold Limited*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya leseni *PL 1549/2000* kumaliza muda wake wa awali wa miaka mitatu na kuhuishwa mara mbili kila kipindi kwa miaka miwili ilimaliza muwa wake tarehe 4/7/2007. Mnamo tarehe 5/7/2007 kampuni ya *Mabangu Mines Limited* iliomba leseni vya utafutaji madini katika eneo hilo na kupewa leseni namba *PL 5374/2008* tarehe 24/10/2008. Muda wa miaka mitatu ya awali wa leseni hiyo utamalizika tarehe 23 Januari, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipingi cha miaka saba ya awali ya leseni hiyo kampuni imekuwa ikifanya utafutaji wa kina wa madini katika eneo la leseni yake ili kugundua na kukadiria kiasi cha mashapo ya madini kilichopo na ubora wake kwa lengo la kuchimba kwa faida.

Kutokana na kazi za utafutaji madini zilizofanyika kuligundulika mashapo yenye dhahabu wakia 737,790, sawa na tani 20.916 kiasi ambacho ni kidogo kuchimbwa kwa faida hivyo ikilazimu kampuni kuendelea na utafutaji wa madni ili kugundua mashapo zaidi.

Kwa sasa mradi wa utafutaji madini wa Nyakafuru bado unaendelea kwa kuwa maeneo hayo ya leseni za Kampuni ya *Resolute Tanzania Limited* na *Mabangu Mining Limited*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni iliona kuwa ni vema kufanya utafutaji wa madini katika maeneo yanayozunguka mradi wa Nyakafuru ili kupata mashapo zaidi. Katika eneo la Mkwani kuligundulika dhahabu wakia 81,917 sawa na tani 2.3223. Eneo la Kanengele liligundulika kuwa na dhahabu wakia 249,856, sawa na tani 7.0833. Takwimu hizo ni kwa mujibu wa taarifa ya kampuni ya mwaka 2007.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi bado unaendelea, kwa sababu za kiafya na kiusalama, ilionekana si vizuri kuanzisha shule ya sekondari ndani ama karibu na maeneo yenye shughuli za utafutaji madini. Hivyo, kampuni ya *Resolute Tanzania Limited* iliwaomba wananchi wachague eneo jingine na ikawajengea Shule hiyo pamoja na kisima cha maji chenye pampu ya kusukuma maji. Hivyo uamuzi wa kuhamisha shule hiyo ulifanyika kwa nia njema na kwa makubaliano kupitia Serikali ya Kijiji na Serikali za Mitaa.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuweka mahusiano mazuri na wachimbaji wadogo na wakubwa pamoja na jamii inayozunguka maeneo yote yenye shughuli za uchimbaji madini ikiwa ni pamoja na wachimbaji wakubwa kuwasaidia wachimbaji wadogo teknolojia ya kisasa ya uchimbaji na uchenjuaji madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuweka mahusiano mazuri na wachimbaji wadogo, kampuni ya *IAM GOLD Tanzania Limited* iliamua kuachia maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa Rwamgasa na Nyarugusu Wilayani Geita ili waendeshe shughuli zao kwa mujibu wa Sheria.

Kampuni nyingine ni *Barrick (Tanzania)Limited* ambayo kwa sasa iko kwenye hatua za mwisho za kuangalia namna ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wanaozunguka mgodi wa *North Mara* kwa kuhusisha jamii inayozunguka mgodi huo ambapo tarehe 25 Januari, 2010 walifanya *risk assessment* ya mradi huo.

Aidha Serikali inasisitiza wachimbaji wadogo na wakubwa kuendesha shughuli zao kwa kuzingatia Sheria na taratibu za nchi ili kuweka mahusiano mazuri baina yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Serikali kuendelea kuboresha mahusiano kati ya watafutaji/wachimbaji wakubwa na wadogo na jamii zinazozunguka maeneo ya migodi. Serikali ina amini kwamba ushirikiano wenye nia njema kati ya Serikali. Watafutaji/wachimbaji wadogo na wakubwa pamoja na jamii zinazozunguka maeneo ya migodi ndiyo suluhu ya kudumu.

MHE. EMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze tu Waziri kwa majibu yake. Lakini kwa kuwa hawa watafiti wamekuwa muda mrefu na masuala haya nimeyauliza muda mrefu lakini pia mahusiano, nimeuliza suala la Turawaka jinsi wasivyoshiriki kuchangia shughuli za maendeleo ene la Runzewe, labda kwa sababu majibu ni marefu ninaomba kwa kifupi Mheshimiwa Waziri akubaliane na mimi baada ya Bunge hili atembelee Bukombe aje azungumze na wananchi wanaozunguka maeneo yale ya Nyakafuru pamoja na Runzewe ili aone mahusiano yaliyopo na hapo hapo atapata nafasi ya kueleza suala la umeme katika maeneo hayo.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwongozo wako na kwa jinsi ambavyo Mheshimiwa Wabunge ameomba nakubaliana naye nitakwenda, suala la mahusiano ni jambo endelevu na tutaendela kulishughulikia kwa kadiri itakavyojitokeza.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hali ya watafiti katika hali ya Kahama ni sawa na Wilaya ya Bukombe ambako kuna maeneo makubwa yanayomilikiwa na watafiti kwa muda mrefu na hakuna dalili zozote za uchimbaji kama kule katika kata ya Idahina. Waziri anaweza kuliambia Bunge hili ni hatua zipoi zinachukuliwa kwa watafiti ambao wamekuwepo kwa muda mrefu na hakuna dalili za kuanza uchimbaji.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la lenyewe ni la kuweka kumbukumbu sawa kwamba watafutaji na wachimbaji madini wanaongozwa na Sheria na miongozo na kanuni zilizopo, hakuna hata mtafutaji au mchimbaji mwenye leseni ambaye anaweza kuendesha shughuli zake kinyume na maekezo ya leseni yake.

Kwa hiyo, watafutaji wanaoendelea kufanya hivi wako ndani ya muda wao wa leseni lakini mara nyingi uchimbaji unafikiwa baada ya watafutaji kujiridhisha kwamba kuna mashapo ya kutosha. Namhakikishia Mbunge kwamba tutaendelea kumpa taarifa kuhusu maendeleo katika eneo la Idahina kama alivyouliza ambako kimsingi ni maeneo ambapo Mheshimiwa Mbunge anatoka.

Na. 85

**Umeme wa Jua katika shule za Sekondari za
Kata na Zahanati**

MHE. DAMAS P. NAKEI aliuliza:-

Kwa kuwa, umeme ni mahitaji ya msingi sana kwa wananchi vijijini hususani, katika shule za Sekondari za Kata na Zahanati.

Je, Serikali inasemaje juu ya umeme wa jua (*solar energy*) kama umeme mbadala katika shule za sekondari za Kata na Zahanati?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Majibu, naona hujajibu siku nyingi ndiyo maana umebanwa sana.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme utokanao na mionzi ya jua ni chanzo mbadala cha nishati katika maeneo ambayo hayajaunganishwa na umeme wa Gridi ya Taifa, kwa matumizi ya nyumbani na taasisi za kijamii kama vyuo vya elimu, magereza, vituo vya

afya, shule za sekondari, zahanati, vituo vya polisi vijijini na pia mitambo ya mawasiliano.

Katika kuendeleza teknolojia ya umemenuru serikali inatekeleza mradi mmoja wakati miradi miwili inafadhiliwa na wahisani ambao ni mpango wa maendeleo wa Umoja wa Mataifa(*UNDP*) na Serikali ya Uswidi. Katika kupunguza gharama za mifumo ya umemenuru, mwaka 2005 Serikali iliondoa kodi zote kwenye vifaa vya umemenuru na vya upepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi uitwao *The Transformation of the Rural Photovoltaic Market* unafadhiliwa na *Global Environment Facility (GEF)* kupitia mpango wa maendeleo wa Umoja wa Mataifa (*UNDP*). Mradi huu unatekelezwa katika mikoa ya Mwanza, Mara, Kagera na Shinyanga. Kupitia mradi huu, uhamasishaji wa umemenuru ulifanywa kwa kujenga mifumo ya mfano mashuleni, vituo vya afya na zahanati. Mafundi mchundo na wajasiriamali wa Halamashauri za Wilaya katika mikoa iliyotajwa walishirikishwa katika kutekeleza mradi pamoja na kupewa mafunzo ya masuala ya umemenuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya matokeo mzuri ya mifumo ya maonesho, Halmashauri zimehamasishwa kutenga fedha katika bajeti za kila mwaka kwa ajili ya umemenuru katika shule na vituo vya afya vijijini. Aidha, kupitia mradi huo viwango vya ubora wa vifaa vya umeme wa jua vimeandaliwa na tayari vimethibitishwa na Shirika la viwango Tanzania(*TBS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ta Uswidi kupitia shirika lake la maendeleo inafadhili mradi ujulikanao kama (*Facilitation of the rural PV Project*) chini ya usimamizi wa Wizara ya Nishati na Madini. Mradi huu unalenga kukuza soko la umemenuru unaoendelea kutekelezwa katika mikoa ya Iringa, Tanga, Morogoro, Pwani, Kigoma, Rukwa, Mtwara, Mbeya, Dodoma, Ruvuma, Lindi, Tabora na Manyara. Utekezaji wa mradi katika mikoa hiyo umetoa mafunzo ya ufundi kwa mafundi mchundo 120 na mafunzo ya biashara kwa wafanyabiashara 149 wa vifaa vya umemenuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi pia umewezesha kujenga uwezo kwa watalaamu wa mamlaka ya mapato Tanzania(*TRA*) na (*TBS*) katika kuhakiki ubora wa vifaa vya umeme wa jua. Aidha, shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) litawezeshwa kuwa na vifaa vya kuhakiki viwango vya ubora (*testing facility*). Baada ya hapo kutakuwa na zoezi la kupitia tena mikoa iliyokwishaifikiwa ili kubaini matatizo na kuona jinsi ya kuyarekebisha.

Mikoa iliyolengwa ni ile ambayo haijafikiwa sana na huduma ya umeme wa gridi na ile ambayo haikuguswa na mradi wa Mwanza. Mkoa uliobaki katika mpango huo ni Singida ambapo uzinduzi wa mradi wa ukuzaji na uendelezaji wa soko na matumizi ya umeme unaozalishwa kwa nishati ya mionzi ya jua utafanyika tarehe 11 Februari, 2010.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) inatekeleza mradi wa umemenuru ujulikano kama *Sustainable Solar Market Packages (SSMP)* katika Wilaya ya Sumbawanga. Mradi huu wa mfano unaofadhiliwa na benki ya Dunia utawezesha mifumo maalum wa umemenuru kujengwa katika vituo 5 vya afya, zahanati 26 na shule za sekondari tisa. Matokeo yake yanatumika katika kuendeleza uzoefu katika maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Watanzania wote kuwa, nishati ya jua inaweza kutoa mchango mkubwa katika kuinua huduma za jamii, hususani katika sekta ya elimu, afya na mawasiliano iwapo mahitaji muafaka ya nishati yatawekwa katika mipango na Bajeti za taasisi za sekta hizo.

MHE. PASCAL D. NAKEI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Aidha nampongeza Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi fulani zoezi la kuweka umemenuru katika Halmashauri yangu au katika Jimbo la Babati Vijijini limekwishaanza, lakini kwa upande wa shule za sekondari zoezi hilo bado halijaanza.

Je, ni lini Serikali itawezesha zoezi hilo likaanza katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Babati?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru kwa pongezi ambazo ameipa Serikali kwa juhudi zinazofanyika lakini pia na sisi tunaipongeza Halmashauri ya Wilaya yake kwa jinsi ambavyo imetoa ushirikiano na yeye mwenyewe binafsi kwa ufuatiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema namna bora kabisa ya kuweza kuvuna rasilimali hii ya Nishati mbadala hasa umemenuru ni kwa kushirikisha Serikali kwa ngazi zote za Halmashauri lakini pia na mipango iliyopo katika Serikali Kuu kupitia Wizara, nimwombe Mheshimiwa Mbunge tuendele kushirikiana, yeye kama sehemu ya madiwani wa Halmashauri husika waboreshe Bajeti kwa ajili ya kupata mitambo ya umemenuru itakayofungwa katika maeneo na taasisi mbalimbali lakini pia tumwombe aendele kuwasiliana na sisi wizarani tuone ni namna gani ambavyo tunaweza kuendelea kushirikiana naye ili kuwezesha maeneo yake mengi zaidi kupata umemenuru.

Na. 86

Elimu ya Uzazi wa Mpango kwa Wanaume

MHE. ANNE KILANGO MALECELA aliuliza:-

Kwa kuwa, mwanamke wa kawaida anao uwezo wa kuzaa mtoto mmoha kwa mwaka na kwa kuwa mwanaume anao uwezo wa kuzaa watoto hata kumi kwa mwaka kulingana na atakavyoamua mwenyewe.

Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kutoa elimu ya kutosha ya uzazi wa mpango kwa wanaume pia, kuliko kutoa kwa wanawake tu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba uniruhusu nichukue nafasi hii nitoe pole nyingi sana kwa wananchi wa Mkoa wa Tanga kwa ajali mbaya iliyotokea kwa kuhusisha basi la Chatco katika Wilaya ya Handeni na kusababisha vifo vya watu 24 na majeruhi 37, nawashukuru sana uongozi wa Wilaya ya Handeni na Korogwe chini ya Uongozi wa Mkuu wangu wa Mkoa Major. Gen. Said Kalembo, kwa kushughulikia suala hilo. Nawaombea majeruhi wapone haraka na Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba uzazi wa mpango ni muhimu katika kuboresha afya, kuinua hali ya uchumi, kuongeza kasi ya maendeleo na kupunguza maradhi na vifo katika jamii. Wanaume na wanawakekwa pamoja wanatakiwa kushirikishwa. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na wadau wake ina mikakati mbalimbali ya kuinua ushiriki wa wanaume katika huduma za uzazi wa mpango.

Mikakati inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na kutoa elimu ya afya ya uzazi kwa jamii wakiwemo wanaume kwa kutoa elimu kwa mtu mmoja mmoja, familia na vikundi.

Programu za uelimishaji wa jamii zinaendeshwa kwa kutumia televisheni, redio, magazeti, vipeperushi na vijarida kwa lengo la kuwafikia watu wote wakiwemo wanaume katika sehemu mbalimbali. Aidha akina mama wanashauriwa kuambatana na waume zao wanapokwenda kupata huduma za kliniki ili kuwawezesha kupata elimu ya uzazi wa mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize kuwa suala la uzazi wa mpango sio la wanawake pekee yao, wanaume nao wanao wajibu wa kushiriki kikamilifu. Aidha naomba nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kutoa wito kwa wanaume wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kuendelea kutimiza wajibu wao wa kushiriki kikamilifu katika suala la uzazi wa mpango ili kuboresha afya za familia, kuinua hali ya uchumi, kuongeza kasi ya maendeleo na kupunguza maradhi na vifo na athari nyingine zinazoweza kusababishwa na ongezeko la watu katika jamii. *(Makofi)*

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata majibu kutoka kwa Naibu Waziri lakini nina swali mmoja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia swali langu vizuri uzito wa swali langu uko hapa kwamba mwanamke wa kawaida ana uwezo wa kuzaa mtoto mmoja kwa mwaka mmoja, lakini mwanaume ana uwezo wa kuzaa watoto wengi kwa jinsi atakavyojipangia mwenyewe, swali linakwenda hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, imejitokeza kwamba watoto wanaozaliwa nje ya ndoa ni wengi sana na wazazi wa upande wa kiume wanawatelekeza watoto hawa kwa wale akina mama ambao wamezaa nao, na kwa kuwa, sasa hivi tumepata vipimo vya *DNA* ambavyo vitamfanya mzazi wa kiume ashindwe kumkana yule mtoto, japo bado wanaume wakitakiwa kwenda kupima *DNA* wengine wanakaidi.

Je, Serikali haiwezi kutunga sheria kali zaidi kuwadhhibiti wanaume wanaozaa watoto nje ya ndoa na kuwatelekeza kule kwa akina mama na kuwaachia akina mama mzigo wa kulea watoto wao wenyewe wakati watoto wale hawakufanya makosa na hawakujileta wenyewe duniani? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Naomba utulivu ndani ya Bunge na wanaoongea waongee kwa sauti za chini kabisa!

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba mwanaume anaweza akazaa watoto wengi ndani ya mwaka mmoja ukilinganisha na mwanamke mmoja kuzaa mtoto mmoja kwa mwaka.

Lakini, katika mojawapo ya njia nyingi ambazo tunaweza tukazitumia ambazo ndiyo maana tunasema akina baba na wenyewe waende katika kupata elimu ya uzazi wa mpango, ndio maana nimesema siyo kwamba lazima mama awe anatumia njia ya mpango, lakini hata baba vile vile anaweza naye akatumia njia ya mpango ili aweze na yeye hata kama atakuwa anaenda nje ya ndoa lakini asiweze kuzaa kwa sababu kuna njia nyingine badala ya mama kufunga uzazi, baba naye akafunga uzazi. Kwa hiyo, ni vitu ambavyo elimu inaweza ikatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile ni kwamba ni kweli kabisa kuna akina baba wanazaa nje ya ndoa na wanawatelekeza watoto. Kweli tuna vipimo vya *DNA*, lakini nakumbuka kabisa kama mnavyofahamu tumepitisha sheria ya watoto. Kwa hiyo, sheria ile pamoja na vipimo hivi vya *DNA* ambavyo tulivipitisha hapa tukiwepo katika Bunge lako Tukufu, nafikiri ni njia moja wapo kabisa ambayo itaweza kuwabana akina baba ambao watazaa lakini na kuwatelekeza watoto na hivyo kusababisha watoto wengi kuishi katika mazingira hatarishi.

Na. 87

Ukosefu wa Madaktari Hospitali ya Rufaa Mbeya

MHE. FLORENCE E. KYENDESYA aliuliza:-

Kwa kuwa Hospitalia ya Rufaa ya Mbeya ni ya Kitaifa, lakini ina matatizo makubwa ya uhaba wa Madaktari Bingwa hasa Idara ya Mifupa iliyo na Daktari mmoja tu; na kwa kuwa baadhi ya wagonjwa hukaa muda mrefu bila kuonana na Daktari Bingwa hivyo kuwepo malalamiko mengi kutoka kwa wananchi:-

Je, Serikali inafahamu tatizo hilo? Na kama inalijua, ni hatua zipi zimechukuliwa za kuongeza Madaktari ?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Florence Esssa Kyendesya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba upo uhaba mkubwa wa watalaam wa afya katika fani zote na katika ngazi zote za kutolea huduma za afya nchini ikiwemo Hospitali ya Rufaa ya Mbeya. Aidha, baadhi ya fani ikiwemo fani ya mifupa, zina uhaba mkubwa zaidi wa watalaam hususani Madaktari bingwa ikilinganishwa na fani nyingine. Sababu kubwa ni uhaba wa watalaam husika katika soko la ajira ambao umechangiwa kwa kiasi kikubwa na uwezo wa vyuo vyetu kuzalisha watalaam husika kwa wingi na tatizo la watalaam wetu kutopenda kujiendeleza katika fani hizo adimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua tatizo hilo, Wizara kwa kushirikiana na Vyuo Vikuu vya hapa nchini inatekeleza mkakati wa kuanzisha mafunzo ya fani zenye upungufu wa watalaam ikiwa ni pamoja na upasuaji wa mishipa ya fahamu, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya figo, magonjwa ya moyo, mazoezi ya viungo na huduma kwa wagonjwa mahututi.

Kipaumbele kimewekwa katika kusomesha watalaam katika fani hizi adimu ili hatimaye kujenga uwezo wa kutoa huduma na kufundisha watalaam hapa hapa nchini. Watalaam wa afya waliogharamiwa na Wizara kujiunga na mafunzo ya uzamili katika fani mbalimbali ikiwa ni pamoja na fani ya upasuaji mifupa ndani na nje ya nchi wameongezeka kutoka wastani wa wanafunzi 60 kwa mwaka 2005/2006 hadi kufikia wanafunzi 240 mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa Hospitali ya Rufaa ya Mbeya na kwa kutambua tatizo la upungufu wa watalaam linaloikabili Hospitali hiyo, Wizara imekuwa ikifanya jitihada za kuongeza watalaam kila inapowezekana kufanya hivyo. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba kwa mwaka 2009/2010 Wizara imewapangia kazi jumla ya watalaam 56 kufanya kazi katika Hospitali ya Rufaa ya Mbeya.

Kati ya hao, wawili ni Madaktari Bingwa wa mifupa na hivyo kufanya Hospitali hiyo sasa kuwa na jumla ya Madaktari Bingwa wa Mifupa watatu.

Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara itaendelea kufanya kila linalowezekana ili kuhakikisha kuwa Hospitali ya Rufaa Mbeya pamoja na Hospitali nyingine nchini zinapatiwa watalaam wa kutosha ili kutimiza azma yetu ya kutoa huduma bora za afya kwa wananchi.

MHE. FLORENCE E. KYENDESYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Pamoja na majibu mazuri ya Serikali yanayotia moyo, ninalo swali moja dogo la nyongeza. Nakubaliana kabisa na majibu ya Serikali, pia naipongeza kwa kutuongezea Madaktari wawili Bingwa wa Mifupa. Lakini kwa kuwa bado uhaba unaendelea hasa Idara ya Upasuaji ambayo yupo Daktari Bingwa mmoja ambaye huyo huyo ndiye Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, ingawa anasaidiwa na Daktari Bingwa mmoja ambaye yuko kwa mkataba, ni mstaafu. (*Makofi*)

Je, Serikali haioni kwamba huyu Daktari anafanya kazi usiku na mchana bila kupumzika, kama binadamu kwa kweli anapaswa apumzike wakati mwingine. Je, Serikali haioni kwamba anachoka, halafu na ndoa yake inaweza ikayumba kwa sababu nyumbani hakai? (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Kwa kweli swali ni kwamba hamwoni uwezekano wa kuongeza madaktari wengine?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la msingi nimesema nimekubali kwamba kuna Daktari mmoja Mtalaam wa Mifupa, lakini katika idadi ya watalaam wale 56, nimesema kutakuwa na Madaktari Bingwa wengine wawili wa mifupa ambao tunawapeleka kule Mbeya.

Kwa hiyo, naamini kabisa, pamoja na Madaktari wengine ambao ni *General Practitioners* ambao watakuwepo kule watasaidiana na huyu Daktari Bingwa anayemsema Mheshimiwa kwamba yuko pale na kwa maana hiyo sasa wataweza kupanga, yeye atakuwa anapumzika wakati wengine nao wanaendelea kufanya kazi. (*Makofi*)

Na. 88

Kupanua Kituo cha Polisi, Ngaramtoni ya Juu

MHE. ELISA D. MOLLEL aliuliza:-

Kwa kuwa, mji wa Ngaramtoni ya Juu katika Wilaya ya Arumeru una watu wengi na unaendelea kukua kwa kasi kubwa:-

Je, Serikali haioni busara ya kupanua kituo cha Polisi kilichoko sasa ili kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elisa David Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Uhaba wa Vituo vya Polisi nchini ni tatizo kubwa. Ili kutatua tatizo hili Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI na wananchi na mkakati wa kuwa na Vituo vya Polisi katika mpango wa kiutawala wa Serikali, kwa maana ya kuwa na vituo vya Polisi katika kila Wilaya, Tarafa na Kata na Sheria. Lengo ni kwenda sambamba na mpango wa Serikali na *Decentralization by Devolution* ili kuwahakikishia wananchi usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti, ukubwa wa eneo la nchi, mpango huu utatekelezwa kwa awamu kwa kuzingatia maeneo yenye uhalifu mwingi zaidi na yale yaliyo mipakani. Wizara yangu inaona umuhimu wa kituo cha polisi Ngaramtoni ya Juu katika Wilaya ya Arumeru, hivyo basi upanuzi wake utaendelea kutazamwa kutokana na hali halisi ya kifedha.

MHE. ELISA D. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Lakini mimi hapa sizungumzii juu ya uhaba, nazungumzia juu ya kituo hiki ambacho kiko sasa hivi na nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza kabisa, kwa kuwa kituo hiki cha Polisi cha Ngaramtoni ya Juu kiko karibu na shamba la Serikali lililoko Ngaramtoni ya Juu, ningependa kumwuliza Waziri. Je, Serikali haioni busara kutenga sehemu ya kupanukia hiki kituo cha Polisi kutoka kwenye shamba la Serikali?

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa vitendea kazi kituo hiki cha Polisi ambacho ni muhimu sana katika jamii, vitende kazi kama gari au pikipiki? Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la msingi ukitizama lilikuwa halizungumzii kupata eneo kutoka katika eneo la Serikali, lilikuwa ni upanuzi wa kituo. Lakini sasa kwa kuwa unazungumzia kupata eneo kutokana na eneo ambalotayari liko mikononi mwa Serikali kama unavyosema, basi hili ni suala ambalo siwezi nikakupa jibu la moja kwa moja katika hili, lakini tutalitizama, lakini pia nia ipo ya kupanua kituo hicho kama nilivyokwambia. Sehemu ya pili kuhusu vitendea kazi, hili ni tatizo Mheshimiwa Mollel tumewahi kulizungumza mimi na wewe na Wabunge wengine. Lakini ni kitu ambacho kinazungumzika, tutakitizama kwa mujibu wa hali halisi tuliyonayo. (*Makofi*)

Na. 89

Wizi wa Mifugo Katika Wilaya ya Tarime na Rorya

MHE. CHARLES N. MWERA aliuliza:-

Kwa kuwa wizi wa mifugo katika Wilaya ya Tarime na Rorya umedumu kwa muda mrefu; na kwa kuwa Serikali imeanzisha Kanda Maalum ya Kipolisi katika Wilaya hizo:-

- (a) Je, ni ng'ombe wangapi wameibiwa na wananchi wangapi wameuwawa?
- (b) Je, ni majambazi wangapi wameuwawa na ni silaha ngapi zimepatikana kutoka kwa majambazi hao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles N. Mwera, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanzishwa kwa Mkoa wa Kipolisi wa Tarime – Rorya mwezi Julai, 2009 hadi Desemba, 2009 jumla ya ng'ombe walioibiwa ni 1,638. Kati ya hao, jumla ya ngiombe 841 waliokolewa 9walipatikana). Aidha, jumla ya wananchi waliuwawa katika kipindi hicho ni 15.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya majambazi wapatao 11 waliuwawa. Pia silaha 9 zilizokuwa zinatumiwa kwenye uhalifu zilikamatwa toka kwa wahalifu mbalimbali.

MHE. CHARLES N. MWERA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Niishukuru Serikali kwa juhudi inazofanya kupambana na wezi wa mifugo. Nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa uwizi wa mifugo umekuwa ukifanywa na wezi kutoka Kenya. Je, Serikali ina juhudi gani inazofanya kushirikiana na Serikali ya Kenya kuzuia wizi wa mifugo maeneo ya mpakani?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu majambazi ambao wanatoka Kenya, Mheshimiwa Mbunge anafahamu. Hili ni suala la muda mrefu, Serikali yetu imekuwa na mazungumzo kati ya Polisi wa kwetu na Polisi wa Kenya; na kwa kweli katika jitihada ambayo tumekuwa nayo ya mazungumzo imeweza kusaidia katika kupunguza tatizo hili. Lakini, bado nataka kumwambia kwamba kumekuwepo na ushirikiano kati ya watu kutoka kwetu huku (majambazi kwa maana hiyo) na majambazi kutoka Kenya.

Kwa hiyo, ni kitu ambacho tunakwenda nacho; na kwa kuwa tumeweka Polisi wa kutosha sasa, tumeweka jitihada ambazo Mheshimiwa Mbunge anazielewa. Nataka kusema tu kwamba jitihada unazozifanya wewe Mheshimiwa Mbunge na ambazo amazifanya Mheshimiwa Sarungi, Mbunge wa Rorya ambazo zilipelekea hata Waziri Mkuu kwenda kule na jitihada hizi ambazo tunazifanya za kuzungumza na Polisi wa Kenya, nafikiri huko mbele ya safari itatufikisha mahala ambapo patakuwa ni pazuri. *(Makofi)*

Sheria ya Kutaka Mikataba Iridhiwe na Bunge

MHE. USSI AMME PANDU aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni imebainika kuwa mikataba mingi ni mibovu imepitishwa na kufungwa na baadhi ya mashirika na taasisi za Serikali, na kwamba mikataba hiyo hewa ina dalili za ufisadi pia:-

- (a) Je, ni lini Serikali italeta sheria hapa Bungeni ya kutaka mikataba yote ya Serikali iridhiwe na Bunge kwa maslahi ya Watanzania?
- (b) Je, kuendelea kufungwa kwa mikataba na kuwa siri sio kwamba kunaendeleza wimbi la ufisadi?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Ussi Pandu Amme, Mbunge wa Mtoni, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna tuhuma wala ushahidi kwamba ipo mikataba hewa inayopitishwa na kufungwa na baadhi ya Mashirika ya Umma au Taasisi za Serikali. Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyofahamu mimi kuna hoja na hisia miongoni mwa watalaam kwamba ipo mikataba halali ambayo inahofiwa kwamba ina masharti ambayo yanatumiza sana kama nchi au haikuzingatia maslahi ya nchi au sekta husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria Na. 4/2005, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inao wajibu wa kuishauri Serikali juu ya mambo ya mikataba ya kibiashara pamoja na mikataba na itifaki za kimataifa kuhusu mambo ya sheria. Serikali imehukua na inaendelea kuchukua hatua za kuwaongezea watalaam ujuzi na umahiri katika eneo hili la mikataba ili kuhakikisha kwamba wanapata ujuzi si katika sheria tu ila fedha na uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi, ninaomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Amme Pandu, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali haina mkakati au mchakato wowote wa kuleta Muswada wenye mapendekezo ya kutunga sheria ya kutaka mikataba yote ya Serikali iridhiwe na Bunge. Mikataba inayolengwa katika swali hili ni ya biashara ambayo kwa kawaida ni shughuli ya utendaji inayotekelezwa na watumishi wa Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 35(1) ya Katiba ya nchi kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Rais kwa matakwa ya Ibara ya 33(2), mbali ya kuwa kiongozi wa nchi na Amiri Jeshi Mkuu, ni kiongozi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge linayo nafasi ya kuisimamia na kuishauri Serikali kuhusu mikataba inayofungwa kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 63(2) na (3) ya Katiba.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba utaratibu uliopo sasa unaendeleza ufiisadi. Mikataba hii inayozungumziwa ni ya kibiashara inayohusu manunuzi ya vifaa au huduma. Bunge lako tukufu limetunga Sheria ya Manunuzi ya Umma, sura ya 410 ya Sheria za Tanzania ambayo imeweka masharti ya kuzingatiwa wakati wa kuingia mikataba. Masharti haya husimamiwa na Serikali kupitia Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (*PPRA*). Upo utaratibu wa kisheria unaoiwezesha mamlaka hiyo kubatilisha mikataba isiyoridhisha.

Mheshimiwa Nabu Spika, mwisho, ninapenda kutoa rai kwamba ni jambo jema kuwa na imani na Serikali ambayo ndiyo yenye mamlaka ya utendaji na kwamba Serikali haiwezi kubariki mikataba isiyokuwa na maslahi au manufaa kwa wananchi wetu.

MHE. USSI AME PANDU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu yasiyoridhisha ya Mheshimiwa Mwanasheria, naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Bunge hili ni kutunga sheria na kuisimamia Serikali jinsi ya kutekeleza majukumu yake. Sasa kama kuna mfano hai ambao umejitokeza wa mikataba mibovu iliyofungwa kama ule wa *TICTS*, *Richmond* na ule wa *TRL*. Je, kwa nini Serikali haioni kwamba kuna haja mikataba hii kuletwa Bungeni na kutungwa sheria ambayo Bunge hili lisimamie na liridhie mikataba hiyo?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninasita kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kwa sababu mambo hayo bado yako hapa Bungeni. Ninamwomba tu asubiri mpaka yatakapomalizika hapa Bungeni.

Na. 91

Serikali Kushawishi Wawekezaji Kujenga Bandari Mbweni na Uwanja wa Ndege Bagamoyo

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi yetu imezungukwa na nchi nyingi zinazohitaji huduma za bandari; na kwa kuwa bandari zetu za Dar es salaam, Tanga na Mtwara zimeshindwa kustawisha Uchumi wa Jiografia:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kushawishi wawekezaji kujenga Bandari ya kisasa Mbweni ya kuhudumia majirani na kukuza uchumi?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kushawishi wawekezaji kujenga uwanja wa Ndege wa kisasa Bagamoyo wa kuhudumia majirani?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifutavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha utafiti wa *Port Master Plan* ya jinsi ya kuendeleza Bandari zetu zote kwa kipindi cha miaka 20 ijayo kuanzia 2008/2009 mpaka 2028/2029. Utafiti huu ulikamilika Machi, 2009, utekeleji wake ulianza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010.

Mpango wa *Port Master Plan* umeainisha maeneo muhimu ya kujenga bandari mpya hususani katika mwambao wa bahari ya Hindi ambayo ni Mbegani (Bagamoyo) na Mwambani (Tanga). Aidha umeainisha umuhimu wa kufanya upanuzi katiaka bandari ya Dar es salaam na bandari ya Mtwara.

Eneo kwa ajili ya ujenzi wa bandari Mbegani (Bagamoyo) limeainishwa na taratibu za kisheria kwa ajili ya kupima, kufanya tathimini, kulipa fidia na kumilikishwa zinaendelea chini ya utaratibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.

Kazi ya upembuzi yakinifu (*feasibility study*) ilianza mwezi Oktoba, 2009 na itakamilika mwezi Aprili, 2010. Vilevile, eneo kwa ajili ya ujenzi wa bandari Mwambani (Tanga) limepatikana, limepimwa na kulipwa fidia. Kazi ya upembuzi yakinifu itafanyika mwaka wa fedha wa 2010/2011. Hivyo, Serikali kwa sasa haina mpango wa kujenga bandari ya kisasa pale Mbweni.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya viwanja vya ndege Tanzania (TAA) kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya makazi imetenga eneo la kujenga kiwanja cha ndege cha kisasa katika Wilaya ya Bagamoyo.

Serikali inaendelea na juhudi za kushawishi wawekezaji kutoka sehemu mbalimbali na tayari wameshajitokeza wawekezaji kutoka nchi za Korea kusini, China, Marekani na Malaysia ambao wametembelea na kuona eneo hilo la ujenzi. Aidha wawekezaji hawa kila mmoja kwa wakati wake wanategemewa kuleta mapendekezo yao ya namna ya kutekeleza mradi huu. Kwa sasa Serikali ipo kwenye mchakato wa kuandaa upembuzi yakinifu (*feasibility study*) wa mradi huo.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana. Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri sana na nimeridhika. Pia napenda kuipongeza Serikali kwa kutengeneza hiyo *Port Master Plan* ya miaka 20 ya kuziwezesha bandari zetu zote nchini hapa kuweza kufanya kazi vizuri kwa miaka 20 ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari ya Itungi Mkoani Mbeya inarahisisha sana biashara kati ya Tanzania na nchi jirani ya Malawi, lakini bandari ya Itungi huwa inajaa mchanga kwa kipindi kirefu kwa mwaka.

Je, kwenye *Port Master Plan* hiyo Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hilo la kujaa mchanga kwenye bandari ya Itungi?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, bandari ya Itungi hivi sasa imefungwa kwa sababu imejaa kabisa mchanga na haiwezi kutumika na jiografia ya pale Itungi ni kuwa tatizo hilo la bandari kujaa mchanga ni tatizo ambalo litaendelea kuwepo miaka hadi miaka. Hivi sasa bandari hiyo imehamishiwa eneo la Kiwira ambako kuna kina kirefu, si mbali na eneo hili la Itungi.

Pale Kiwira kuna *natural harbour* ambayo ina kina kirefu na meli ambazo zinafanya huduma sasa hivi katika Ziwa Nyasa zinatumia bandari hiyo ya Kiwira.

Kuna tatizo la barabara ya kuingilia katika bandari pale, sasa hivi ni ya changarawe na haiko katika hali nzuri sana. Katika mpango huu wa kuendeleza *Ports* zetu tunatarajia kwamba tutaifanyia marekebisho barabara ile, lakini pia kuiboresha bandari ya Kiwira ambayo itaweza kutoa huduma kwa miaka mingi ili kuweza kutumia vizuri pesa za taifa hili. (*Makofi*)

Na. 92

Air Tanzania Kuanzisha Safari Zake Dodoma

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati wa kujibu Swali Na. 219 katika Mkutano wa 16, Serikali ilieleza kuwa, ipo mipango ya kujenga kiwanja kipya cha ndege hapa Dodoma; na kwa kuwa, kiwanja cha ndege kilichopo sasa ni kikongwe lakini bado hakijatumiwa ipasavyo kwani hakuna ndege za abiria wa kawaida pamoja na Serikali kuahidi Bungeni kwamba *Air Tanzania* ingeanza safari zake na ni miaka miwili imepita safari hizo hazijaanza.

Je, Serikali inasema nini juu ya ahadi hiyo ambayo hadi sasa haijatekelezwa?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wakati nikijibu Swali la Bunge Na. 219 katika Mkutano wa 16 wa Bunge, nilieleza kwamba Serikali ina mpango wa kujenga

kiwanja kipya cha ndege katika eneo la Msalato nje kidogo ya Manispaa ya Dodoma. Mpango huo bado upo na kwa sasa tayari Serikali imeshalipa fidia kwa wakazi wote walioikuwa wanaishi katika eneo hilo ili kupisha ujenzi wa kiwanja kipya. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika kwa fedha za msaada jumla ya Dola za Marekani 440,000 kutoka Benki ya Uarabuni ya Maendeleo kwa Afrika (*BADEA*). Kwa sasa, Serikali iko katika mazungumzo na washirika wa maendeleo wa Tanzania ikiwemo *BADEA* ili kupata fedha za ujenzi wa kiwanja hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya ndege ya Tanzania (*ATCL*) katika Mpango wake wa biashara wa 2008/2009 ilikuwa imepanga kuanza kutoa huduma za safari za ndege kati ya Dar es Salaam na Dodoma kuanzia mwezi Julai, 2008. Aidha, tangazo la kuanzishwa kwa huduma hizi lilitolewa ndani ya Bunge lako Tukufu wakati wa kikao cha Bunge la Bajeti la 2008/2009. Hata hivyo, mpango huo haukutekelezwa kutokana na kutokuwa na maandalizi ya kutosha pamoja na ukosefu wa fedha za kuanzisha safari hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *ATCL* inajipanga upya ili iweze kutoa huduma kati ya Dar es Salaam na Dodoma kama ilivyo katika mpango wake wa Biashara wa 2010/2011. Kwa sasa Kampuni inaendelea na maandalizi ya kuandaa Miundombinu itakayowezesha huduma za usafiri wa anga mjini Dodoma kutolewa.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Ni kigezo gani cha kitalaam katika mipango bora ya nchi kilichotumika kuwa na mipango ya kujenga kiwanja kingine kipya wakati kilichopo hakina hata ndege za abiria yaani hakitumiki?

Je, Serikali ina mamlaka na Mashirika binafsi ya ndege yaliyopo hapa nchini katika kupanga *route* kwa kuzingatia kwamba mji wa Dodoma hivi sasa una ongeziko la watalaam, watu kutoka Serikalini, Wabunge, wafanyabiashara mbalimbali wasiopungua 4,000 katika kipindi kidogo cha miaka miwili iliyopita?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanja cha Dodoma ni kiwanja kidogo ambacho uwezo wake ni kwa ajili ya kupokea ndege zenye uwezo wa kubeba abiria wachache. Lakini kwa sababu Dodoma ni Makao Makuu ya nchi, katika miaka kadhaa inayokuja na hasa katika kukidhi mahitaji ya Jiji la Dodoma kwa miaka 50 ijayo ni muhimu kuhakikisha kwamba tunakuwa na kiwanja kikubwa cha kimataifa ambacho kitakidhi mahitaji ya Makao Makuu ya nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, hiki ambacho tunacho ambacho sasa hivi kiko kati kati kabisa ya mji, tutaendelea kukitumia kwa kipindi cha miaka ambacho kitaweza kutoa *service*. Lakini kwa miaka mingi ijayo tutahitaji kiwanja kikubwa ambacho kinakidhi hadhi na mahitaji ya Makao Makuu ya nchi na ndio sababu tumetenga eneo mapema na kuanza kulifanyia mipango ya kuweza kujenga kiwanja hicho.

Serikali haiyapangii Mashirika ya ndege *route*. Lakini, kwa umuhimu wa mji wa Dodoma, tunajitahidi kushawishi Mashirika ya ndege binafsi zianzishe safari zake Dodoma pamoja na Shirika la Ndege la Taifa. Tarehe 27 Januari, 2010 *Air Zahara*

imepewa *Provisional AOC (Air Operators Certificate)* ambayo inaruhusu kuanzishwa safari za ndege za kupangwa ama *Schedule Services*; na katika mpango wa *Air Zahara* kuanzia tarehe 8 Februari, 2010 inatarajia kuanza *route* za Dar es salaam – Dodoma – Dar es salaam na Dar es salaam – Mbeya tutegemee kuwa hivi karibuni tutakuwa na *Air Services* za Dodoma.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda pia umekwisha.

Sasa ninapenda kutambulisha wageni walioko hapa Bungeni. Kwanza ni wageni kutoka Ubalozzi wa Marekani ambao ni Balozzi mwenyewe Mheshimiwa Alfonso Lenhardt, pia yupo Mkuu wa kitengo cha Siasa na Uchumi, Mr. Carl Fox na Mratibu wa Masuala ya Siasa na Uchumi, Miss Tina Mdobilu. Mheshimiwa *Balozzi, you are very much welcome. We understand that its your first time to be in our House and also for the past six month you have been in our Country, we have been seen your efforts to try to help us in this Country. Thank you very much. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine ni wa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja pia ni wageni wa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige ambao ni Diwani wa Kata ya Bugarama, Jimbo la Msalala ambaye ndiye Kiongozi wa msafara, Mheshimiwa Boniface Shija, karibu sana Mheshimiwa Diwani. Ninadhani umefuatana na wenzio, Katibu wa CCM, Kata ya Bugarama, Ndugu Silvester Lusobangija, yuko Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kakola kwa tiketi ya CHADEMA, Ndugu Emmanuel Bombeda, siyo Mheshimiwa Mgeni wa CHADEMA, huyu ni mgeni wa hawa jamaa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, yuko Maalim Kadau na Ndugu Buchward Mbelwa, wote mnakaribishwa na karibuni sana hapa Dodoma. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, ambaye ni Mkurugenzi wa *Club* mpya ya *Sun Cirro* Shekilango Dar es salaam (*Club* kubwa na ya kisasa kuliko zote Dar es salaam), Ndugu Claud Masuke. Halafu kuna Kada wa CCM Kata ya Kiwalani, Jimbo la Ukonga, huyu ni Ndugu Godlisten Malisa, karibuni sana wageni. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Celina Kombani ambao ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake Wakatoliki, Morogoro, Ndugu Antonia Mitti, amefuatana na Ndugu Magdalena Vullu, Ndugu Scolastica Haule, Ndugu Hapiness Inana na Ndugu Devotha Ngatabura. Karibuni sana, nadhani ni wanachama wa WAWATA kwa sababu wamevalia sare ya WAWATA. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna Wageni wa Mheshimiwa Alhaji Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini ambao ni Katibu Mwenezi wa CCM, Kata ya Ntuntu, Ndugu Joseph Yunde. Halafu yupo Katibu wa CCM, Kata ya Suyu, Ndugu Michael Labia na Katibu Kata wa CCM, Kata ya Mgungira, Ndugu Jeremiah Lissu, karibuni tena wanachama wa huko Singida Kusini. *(Makofi)*

Pia tuna mgeni wa Mheshimiwa Lucy Owenya ambaye ni Miss Eva Kiwia, mtoto wa Wifi yake yaani mtoto wake huyo, karibu sana Bi. Eva Kiwia. *(Makofi)*

Halafu kuna wageni wa Mheshimiwa Charles Kajege ambao ni wanafunzi saba wa Shule ya Sekondari na Msingi wa Kata ya Nansio na Mwibara. Wanafunzi wenyewe wako wapi? Wasimame walipo, wao hawa wamefuatana na Mtendaji wa Kijiji cha Nmabaza, Ndugu Yolanda Mganga na Katbu wa Mbunge Mashaka Magessa. Ahsanteni sana, tunafurahi kuwaona watoto hao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna mgeni wa Mheshimiwa Dr. Festus Limbu wa Magu ambaye ni Mhadhiri na Mtaalamu wa Upasuaji, *Surgeon College of Medicine University of Dodoma*, Dr. Fabian Anaclet Massanga. Huyo ni mgeni wetu sisi sote maana tukiumwa hapa, tuko huko, ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe ambao ni viongozi watano wa Chama cha Wafanyakazi wa Mgodu wa Makaa ya Mawe ya Kiwira, Mkoa wa Mbeya, wakiongozwa na Mwenyekiti, Ndugu Daniel Kibona na Katibu wake Ndugu Thomas Cheyo. Karibuni sana sisi Azimio letu litakuja katika siku hizi za karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Martha Mlata kutoka Taasisi ya Usalama Barabarani kwa Watu wenye Ulemavu ambao ni Mwenyekiti Ndugu Jutorum Kabatale, Ndugu Hamis Nasoro Cheni, Mkurugenzi, hawasimami, nimesema ni viongozi wa Taasisi ya Usalama Barabarani kwa Watu wenye Ulemavu, kwa hiyo ahsante sana kwa kuweza kuja, tumefurahi kuwaona. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Bwana Richard Kigaraba kutoka Kibondo, ni Mtanzania mwenzetu ambaye amewahi kuwa Mkurugenzi wa Miradi ya Maedeleo kwa Bara la Afrika na Mradi wa Umoja wa Mataifa wa Shirika la Posta Ulimwenguni lenye Makao Makuu Uswiss kwa muda wa miaka 25, amekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge, Ndugu Richard Kigaraba uko wapi? Ooh! Una historia kubwa sana, nadhani utapata nafasi ya kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge huko nje kuhusu huu utalamu mkubwa. *(Makofi)*

Tuna wageni 14 kutoka Jumuiya ya Walimu wa Madrasa Dodoma, wamekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge. Wageni wetu hao 14 tunaomba wasimame walipo, wale Walimu wa Madrasa, walikosa nafasi labda kesho watakuja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tuliopewa, sasa matangazo ya shughuli za kazi.

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa William Shellukindo, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya

Bunge ya Nishati na Madini kuwa kutakuwa na kikao leo tarehe 3 Februari, 2010, saa saba mchana, katika ukumbi namba 227, ghorofa ya pili.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kuwa kutakuwa na mkutano leo tarehe 3 Februari, 2010, saa tano asubuhi, katika ukumbi namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi, anaomba niwatangazie Wajumbe kuwa kutakuwa na kikao leo tarehe 3 Februari, 2010, saa saba mchana, katika ukumbi namba 133, ghorofa ya kwanza.

Haya ndiyo matangazo ya shughuli zinazotakiwa kufanyika sasa hivi.

Waheshimiwa Wabunge, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto, Mheshimiwa Margaret Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii pamoja na wajumbe wa Kikundi cha Kufuatilia Masuala ya Jinsia Bungeni (*Parliamentary Gender Group*) kwamba saa saba leo mchana, wakutane kwenye Ukumbi wa Mafunzo *African Dreams*.

Mheshimiwa Ngeleja anasema sijatangaza wageni wake, ngoja niangalie, nimewataja wengi sana, tena wa kwanza kabisa, nimewataja wageni wa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Willliam Ngeleja na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige ambao ni Mheshimiwa Boniface Shija, Mheshimiwa Silvester Msobangija, Mheshimiwa Emmanuel Pombeda, Mheshimiwa Maalimu Kadau, Mheshimiwa Buchwadi Mbelwa, sasa sijui ndiyo hao Waheshimiwa, tunaendelea na kazi.

MHE. WILLIAM H . SHELLUKINDO: Mwongozo wa Spika!

NAIBU SPIKA: Ndiyo Mheshimiwa!

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimeleta tangazo langu sijalisikia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shellukindo, nimetangaza la kwanza kabisa na ni chumba namba 227, naeleweka, sasa tunaendelea. (*Kicheko*)

HOJA ZA SERIKALI

MAAZIMIO

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) wa Mwaka 2008 (*SADC Protocol on Gender and Development*)

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu kwamba, Azimio hili tulikuwa tumeanza kulijadili jana jioni na tunao wachangiaji wengi na tutachukua muda wote wa asubuhi hii. Kwa hiyo, wanaoitwa sasa ni Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu na Mheshimiwa Anna Lupembe, wajiandae.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Azimio hili la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya Nchi za *SADC*. Mimi napenda kusema kwamba ninaunga mkono Azimio hili, pia niipongeze Wizara, Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kuweza kufikisha Mkataba huu ndani ya Bunge lako Tukufu ili uweze Kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kusema kwamba ninaunga mkono Azimio hili lakini ninaunga mkono isipokuwa Ibara ile ya 20(2)(a) ambayo inaruhusu utoaji wa mimba.

(Hapa kulikuwa na minong'ono toka kwa Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wakitoka nje ya ukumbi)

NAIBU SPIKA: Jamani, mnapoondoka, muondoke *quite, quite*, kimya kimya.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele hiki kinasema kwamba kuna mimba za dharura, mtu yeyote unapokwenda kushiriki katika tendo hili lazima unajua matokeo ya tendo hili ni nini lakini pale unaponiambia kwamba kuna mimba za dharura, sikubaliani na suala hili na hivyo ninaungana na Kamati ya Bunge kusema kwamba kipengele hiki tusikiunge mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii kuwaambia vijana wa kike na wa kiume, wale ambao hawako tayari kulea, basi wasishiriki tendo hili na kusababisha kuja kutoa uhai kwa watoto ambao wana haki ya kuishi Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Itifaki inavyozungumzia kwamba ifikapo mwaka 2015 nchi zote za *SADC* zilizoridhia Mkataba huu ziwe zimeondoa zile Sheria kandamizi zinazomkandamiza mwanamke mfano Sheria ya Ndoa na ile Sheria ya Mirathi. Hivyo, tunayo changamoto kubwa kama nchi kuhakikisha kwamba zile Sheria zote zinazomkandamiza mwanamke zinafanyiwa marekebisho ili ziweze kuletwa ndani ya Bunge letu Tukufu ili liweze kuzipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niongelee suala la uchumi. Kipato cha mwanamke na mwanaume katika nchi yetu kinatofautiana sana na mwanamke amekuwa na kipato kidogo sana katika nchi yetu lakini wanaume wamekuwa wana kipato kikubwa na hivyo kumnyima haki mwanamke huyu mwenye kipato kidogo hata kushiriki katika uchaguzi. Tunajua chaguzi zetu zinahitaji fedha na kama mwanamke huyu hatawezesha, hataweza kushiriki katika shughuli zozote za kimaendeleo hata za kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utafiti uliofanyika mwaka 2009 wa *World Economic Forum*, umeonyesha kwamba nchi yetu mwaka 2009 ilikuwa nafasi ya 26 mwaka 2006 lakini mwaka 2009 imeporomoka kutoka nafasi ya 26 mpaka nafasi ya 73. Hii inaonyesha kabisa nchi yetu haina mikakati madhubuti ya kumwezesha mwanamke huyu maskini ambao wengi wako vijijini, wanajishughulisha na shughuli ndogondogo za kilimo ambazo zimeendelea kuwafanya kuwa maskini. Tunataka Serikali yetu ituambie katika mpango huu wa Kilimo Kwanza ambapo nchi yetu inaonyesha kabisa kwamba kina mama wengi wanajishughulisha na shughuli za kilimo huko Vijijini, imejipangaje kumsaidia mwanamke huyu kupitia fedha za Kilimo Kwanza ili kuweza kumsaidia mama huyu naye aweze kupata kipato kikubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kazi nyingi sana zinafanywa na akina mama lakini kazi zao zimekuwa hazithaminiki hasa kutokana na mfumo dume ambao ulikuwepo katika nchi yetu lakini kina mama wamekuwa mstari wa mbele kufanya kazi ndogondogo ambazo zimekuwa zikiongeza kipato katika familia zao, lakini inapofika wakati wa kupata mapato hayo mwanaume ndiye anayekuwa mstari wa mbele kusimamia mapato hayo na kumfanya mwanamke maskini huyu kuendelea kuwa maskini na kushindwa kujishughulisha katika shughuli za kisiasa. Pamoja na kuridhia Mkataba huu lakini bado tunazo changamoto kubwa za kuweza kumtoa mama huyu ili na yeye aweze kusikika na kuweza kuwa na maamuzi katika familia na hata katika vyombo vya Kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la afya. Mkataba huu unatutaka itakapofika mwaka 2015, tuwe tumepunguza vifo vya akina mama na watoto angalau kwa 75%. lakini pamoja na hayo bado tunazo changamoto kubwa. Juzi kulikuwa kuna swali hapa lililokuwa linazungumzia kuhusu kupunguza vifo vya akina mama na watoto lakini tuna upungufu mwingi sana wa Vituo vya Afya katika vijiji vyetu, hatuna Wahudumu wa kutosha katika Hospitali zetu, pia katika hospitali zetu hatuna vifaa vya kutosha. Kwa hiyo, bado tunazo changamoto nyingi sana za kuhakikisha kweli ifikapo mwaka 2015 tunaweza kupunguza vifo vya akina mama na watoto. Kusema eti tunamaliza tutakuwa tunajidnaganya kwa sababu bado hatuna hivyo vitu nilivyovisema katika hospitali zetu. Kwa hiyo tunatakiwa kufanya jitihada za makusudi ikiwemo Wizara ya Afya aidha, iongezewe bajeti ili kuweza kuhakikisha vitu hivyo vinapatikana yakiwemo magari ya wagonjwa ili pale akina mama wanaposhindwa kujifunga kwenye Vituo vya Afya vidogo waweze kukimbizwa kwenye Hospitali kubwa, hizi bado ni changamoto na tunatakiwa tuzifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, vipovifaa vya akina mama ambavyo wanatakiwa kutumia wanapojifungua. Hivi majuzi tumeambiwa kulikuwa na taulo za akina mama zimeingizwa ambazo ni feki lakini mpaka sasa Serikali haijatuambia nini madhara ya taulo hizo na ni zipi ambazo si feki ili tunapokwenda madukani tujue tunanunua taulo zipi. Tunaitaka sasa Wizara inayohusika ikae na ituambie kwa sababu akina mama tumekuwa ni waathirika wakubwa, vifo vya akina mama na watoto, ni sisi bado mnatuletea taulo ambazo hazina sifa za kutosha, waathirika tutakuwa ni sisi akina

mama. Kwa hiyo, Wizara husika tunaitaka itoe tamko juu ya taulo hizo, akina mama tumechoka na sasa tunaziomba Wizara zinazohusika zichukue hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie suala la uwakilishi na ushiriki wa wanawake katika siasa. Bahati nzuri Azimio hili limefika wakati muafaka ambapo tunakwenda kwenye uchaguzi mwezi wa kumi lakini tunavitaka Vyama vya Siasa kama kweli vina nia ya dhati basi, vionyeshe mfano mwezi wa kumi utakapofika pale ambapo kina mama wanaonyesha nia ya kwenda kwenye Majimbo tuwape *support* za kutosha. Tunaviomba pia vyombo vya habari, viendelee kutoa elimu kwa wapiga kura wetu kwamba kina mama tunaweza kwa sababu wale waliokwishakupata nafasi tumeweza kuonyesha kuwa tunaweza. Lakini ziko mila potofu ambazo zinadai kwamba hawawezi kuongozwa na akina mama. Mila hizo zimepitwa na wakati, tunawaomba mtuunge mkono, mkitu-*support* tunaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Viti Maalumu lisiwe tu kwamba Viti Maalumu tuwape akina mama ili mtuzuie kwenda kwenye Majimbo, Viti Maalumu vipo ili viwe ngazi ya kutuwezesha akina mama kufika kwenye Majimbo. Kwa hiyo, akina baba, tunawaomba pale tutakapokuja kwenye Majimbo yenu, mtupokee, mtupe ushirikiano kwa sababu na sisi tunaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wanaosema kwamba ni Majimbo yao. Lakini ninaamini ni Majimbo yetu wote, waamuzi ni wananchi. Tutapimwa kutokana na kazi tulizofanya. Ninaamini wanawake wana uwezo na hatuhitaji tu Viti Maalumu kwa sababu ni vya kupewa, tunataka pia hivyo vya kugombea kwa sababu akina mama tunaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi hizi za uwakilishi tusingalie tu nafasi za Ubunge au Udiwani, zipo nafasi nyingi sana ambazo tungependa wanawake nao waweze kuongezeka kwa sababu tunao wanawake wasomi na wenye uwezo. Naomba nionyeshe nafasi hizo kwa uchache na kwa jinsi akina mama walivyo wachache katika nafasi hizo. Mfano tuna ma-DC 112 lakini ni ma-DC 25 tu ndio wanawake sawa na 18.7%; tuna ma-DAS 105 lakini akina mama ni watano tu (5) sawa na 14%; tuna ma-DED 116 lakini tuna ma-DED 21 tu ambao ni wanawake sawa na 26.5% na tuna Wakuu wa Idara za Serikali 1600 lakini wanawake ni 158 tu ambao ni sawa 18%. Hii inaonyesha kwamba bado akina mama hatujafikia ile asilimia ambayo tunaipigania. Hivyo ziko changamoto ambazo Serikali inatakiwa kuzifuatilia kwa kuhakikisha akina mama wanaweza kushika nafasi hizi ambazo zipo na akina wa kufanya kazi hizo na wenye uwezo, wapo. Kwa hiyo, pamoja na kuridhia mkataba huu, bado tuna changamoto nyingi sana ili tuweze kufikia asilimia inayozungumziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie suala la haki za Wajane na Wagane lakini wanaoathirika sana ni Wajane kwa sababu ni mara chache sana unasikia Wagane nao wananyanyasika. Akina mama wengi wanahofiwa na waume zao, tumekuwa tukisikia kwenye vyombo vya habari wanavyonyanyasika wao na watoto wao. Familia wanaposikia ndugu yao amefariki huwa wanakuja kwenye familia ile na kumfukuza mama na watoto lakini pale wanapokuwa hai wakitafuta mali, hakuna hata mmoja anayekuja kushirikiana nao lakini pindi anapofariki mume, ndugu wa mume ndiyo

wanajitokeza kuja kudai mali na kumwambia yule mama hukuja na kitu hapa kwa hiyo utaondoka bila kitu, watoto anapewa zawadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuhakikisha kama nilivyosema mwanzo zile Sheria za Mirathi na za Ndoa zije ndani ya Bunge ili tuweze kutoa haki kwa akina mama hawa na watoto ambao wanazalisha watoto wa mitaani. Wagane kama wapo nao pia wajitokeze kwa sababu hatuwezi kuwasemea watu ambao hawajitokezi, kama wapo wanaonyanyaswa, kama wapo wanaume wanaopigwa na wake zao basi wajitokeze ili na sisi tuweze kupigania haki zao lakini kusemea ndani bila kulalamika, bila kuchukua hatua, tutashindwa jinsi ya kuwatetea na kuwasaidia. Hivyo ni changamoto kwa wanaume kama wapo nao wajitokeze ili tuweze kuwasemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nivipongeze vyombo kama *TAMWA*, *TGNP*, *NOLA*, Madhehebu ya Dini kwa sababu yamekuwa yakijitokeza sana na kutoa elimu kwa wanawake juu ya kujua haki zao. Hivyo, tunaomba vyombo vingine viendelee kutoa ushirikiano ili jamii nzima iweze kutambua haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 9 katika mkataba huu, kinazungumzia haki za walemavu kwamba katika Sheria zote za nchi ziwe zinaangalia haki za walemavu na mimi ninaungana nao. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya *LAAC*, tunakagua majengo mengi, shule lakini cha kushangaza zile njia za walemavu katika shule au katika majengo hayo, wengi hawazingatii. Kwa hiyo, tunaomba sana wale wote wanaopewa kazi hizi wazingatie haki za walemavu kwa sababu nao wanahitaji kusoma lakini kwa shule tulizonazo majengo ya vyoo yalivyo, ni vigumu sana kwa watu wenye ulemavu kufika. Pia majengo ya Serikali jinsi yalivyo ni vigumu kwa watu wenye ulemavu kufika na kupata huduma aidha elimu au kwenda kupata taarifa zozote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo tunaomba sana, turidhie Itifaki ya Haki za Watu wenye Ulemavu na mkatuahidi ingeletwa Sheria ya Watu wenye Walemavu lakini mpaka leo Sheria hiyo haijaletwa ndani ya Bunge. Tunaomba zichukuliwe hatua za haraka, Sheria hiyo ije iweze kupitishwa na Bunge ili wale wote watakaokiuka Sheria hizo waweze kuchukuliwa hatua maana bila Sheria watu watafanya mambo wanavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, ninaomba kuunga mkono Azimio hili lililoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nilikuwa nimewaita kina Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, nawaomba niwakatili kwa sababu *AG* anataka kuchangia na ana safari, kwa hiyo, nitaomba *AG* azungumze kwanza. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, naomba ufike mbele, ilikuwa aseme kwenye Kauli za Mwaziri lakini tulikuwa tuna-*sort out* kitu kimoja kwa hiyo, tunaendelea.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba na mimi kuchangia kwa ajili ya kutoa ufafanuzi unaohusu, kama Bunge linaweza Kuridhia Itifika ya Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za

Kusini mwa Afrika (*SADC*) bila masharti yaliyomo kwenye Ibara ya 20(2) ya Itifaki hiyo yanayohusu kutoa mimba zinazotokana na ubakaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa kuweka masharti wakati wa kuridhia Itifaki au Mkataba wowote wa Kimataifa, unatokana na Ibara ya 19 ya Mkataba wa Vienna wa mwaka 1969 ambao ulianza kutumika mwaka 1980 yaani *The Vienna Convention on the Law of Treaties of 1980*). Kwa desturi, katika mikataba inayohusu inayohusu *economic intergration* ndani ya *SADC* na *East African Community*, si kawaida kuweka *reservation*. Aidha, Ibara inayohusika yaani ile ya 20(2) ya Itifaki hiyo, si msingi kabisa wa Itifaki yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 19 ya Mkataba wa Vienna, inaruhusu *reservations* kwa mambo ambayo hayaathiri Mkataba au Itifaki na kwa kuwa suala la kutoa mimba si msingi wa Itifaki hiyo, Bunge hili laweza kama nilivyomsikia Mheshimiwa Grace Kiwelu akizungumza kwamba Bunge laweza kuridhia hilo bila kuwa na masharti ya Ibara ya 20(2). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu kwamba Bunge hili liliridhia Itifaki ya Maputo kuhusu Haki za Wanawake Barani Afrika chini ya Mkataba wa Afrika kuhusiana na Haki za Binadamu na Watu Barani Afrika (*The Protocol to the African Charter on Human And Peoples' Rights on Rights of Women in Africa*), ninashauri kwamba Bunge ili kuepukana na yale yanayotokea kwenye Itifaki ile, liliridhie Itifaki hii bila kuhusisha masharti ya Ibara ya 20(2)(a) katika utekelezaji wa Itifaki husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuacha shaka yoyote ya maana, kwa mujibu wa Katiba na desturi za Tanzania, Itifaki yoyote ya Kimataifa au Mkataba wowote wa Kimataifa (*Treaty*), hauwezi kuzibana sheria zetu kama Bunge hili halijatunga sheria mahsusi za kutekeleza. Hivyo, hata ile Itifaki ya Maputo ambayo inahusu Haki za Wanawake Barani Afrika, itakuwa ni kinyume cha sheria yetu kama itatekelezwa na kifungu kile cha kutoa mimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, ninashauri kwamba Bunge hili likubali kuridhia Itifaki yenyewe bila masharti yaliyopo katika Ibara ya 20(2). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaomba radhi Waheshimiwa Wabunge wengine ambao walitangulia kuomba kabla yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Azimio hili. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana na mimi kwamba Mwanasheria Mkuu ametusaidia siyo sisi Wabunge tu lakini na nchi nzima, vinginevyo wangeiweka katika sura ambayo kila mtu alivyoisema, lakini ukweli ni kwamba wote tumekubaliana Itifaki inakubalika lakini kifungu hiki, kiko kinyume na mila na sheria zetu zingine. Tunakushukuru sana Mwanasheria Mkuu kwa maelezo hayo ya kikamilifu.

Waheshimiwa Wabunge, nitamwita sasa Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya na Mheshimiwa Bernadeta Mushashu ajiandae.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niwe mchangiaji kuhusiana na Azimio lililoletwa mbele yetu linalohusu Mkataba wa Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) wa mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe shukrani kwa waandaaji wa Azimio hili hasa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Naibu wake pamoja na watendaji wao wote wa Wizara. Lakini pia nichukue fursa hii kutoa shukrani sana kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuona na kuzingatia na kuheshimu sana masuala ya jinsia hususani kuwapa wanawake nafasi mbalimbali za uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba kwa kuwa nchi yetu inaendeshwa kwa utawala wa sheria, tumeweza kuheshimu sana MaAzimio mbalimbali ambayo yamekuwa yakipitishwa na kwa kweli leo hii ndiyo maana tunajivunia hali halisi ya nyongeza ya watu mbalimbali ambao wapo kwenye uongozi wakiwepo Mawaziri kama alivyo Mheshimiwa Sitta na Naibu wake, lakini tunao Makatibu Wakuu wa Wizara, wako Ma-RC, ma-DC, Wakurugenzi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kasi inayohitajiwa ya kwenda kasi katika nyongeza hii, lakini ni wajibu pia ili kuweka usawa huu kijinsia, sasa inahitajika sana kufanya maandalizi ya kutosha ili kuwa na watu ambao watakuwa ni *capable* pale wanapoinjia katika kufanya shughuli za kiuongozi na shughuli mbalimbali za kiutendaji. Kwa hiyo, ni wajibu wa Serikali na taasisi mbalimbali ziweze kuona umuhimu wa kumwezesha mwanamke kwa masuala mbalimbali na kumwaandaa ili anapokuja kushika nyadhifa, tunakoelekea huko tunakosema *fifty fifty* basi awe amekuja kwa ukamilifu zaidi na ili kupanua wigo wa kufanya shughuli za kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba wanawake katika nchi yetu wako wengi sana hususani katika Jimbo langu la Uchaguzi la Iramba Magharibi na wanawake ndiyo watendaji wa shughuli nyingi za kuleta maendeleo. Wanawake kule Jimboni kwangu ndiyo wanaofanya kazi hasa za kutunza familia na kilimo. Nataka nitumie fursa hii niombe Wizara, kwamba bado uelewa ni mdogo sana huko vijijini, tupenyeze hii fursa huko vijijini ili tuhakikishe hawa wanawake ambao wamekuwa wakitumika na wanatumika sana nao waweze kuendelezwa ili tunapofikia katika usawa wajue haki zao na kama nilivyosema ifikapo mwaka 2015 kuondoa sheria kandamizi kwa kuzielewa wao wenyewe wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu tunaporidhia Itifaki hii zipo Itifaki mbalimbali ambazo zimetangulia na hii imekuwa kama ni mwendelezo tu. Tunazo Itifaki ambazo zimetangulia ambazo zilianza na ndiyo chimbuko lake *Beijing Platform* lakini ikafuatia CEDAW nakadhalika. Sasa sisi kwa hali hii leo tutakaporidhia Azimio hili

lakini tunaliridhia tukiwa katika Jumuiya ya SADC na wakati huo huo sisi Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, wanachama wenzetu wengine Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi, wao wanaweza wakawa hawamo katika hili Azimio, ni wajibu wetu na ni wajibu wa Serikali kwa ujumla kuona umuhimu wa kuweza kuambukiza hili suala katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ili twende kwa pamoja. Leo tutakapokwenda kwa Tanzania tunazingatia yale masharti ya kuondoa zile sheria kandamizi za wanawake basi na Jumuiya ya Afrika Mashariki yote kwa ujumla iwe inafuata utaratibu huu na hivyo naamini kabisa tutakwenda vizuri katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo msemu mzuri sana na rahisi watu wanasema ‘mjenga nchi ni mwananchi na mvunja nchi ni mwananchi mwenyewe’. Nataka nizungumzie kuhusiana na suala la akina mama wale waliopo madarakani au katika nyadhifa mbalimbali. Kumekuwa na tabia ya akina mama kubezana wao kwa wao na hili ni lazima tuliseme na hata humu ndani lipo hata kama leo mama mmoja akigombea nafasi fulani wao ndiyo wanakuwa namba mmoja kuweza kubeza nafasi ya mama mwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wa akina mama mnapobebwa basi na wewe ubebeke kwa sababu unapoanza kumvunja nguvu yule mama mwenzako sasa hata wale wengine ambao ndiyo wanaokubeba nao watapata nafasi ya kuweza kubeza nafasi yenu akina mama. Kwa hiyo, usishangae mnapofikia mahali mnasema wanaume wanatuingilia katika hili, chimbuko ni ninyi wenyewe, mnapoanzisha chokochoko, mnaruhusu wanaume wapenye, mngeweza kuweka misimamo ninyi wenyewe kwa kusimama kwa miguu miwili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tena wewe una uzoefu wa kutosha sana kwa sababu umeingia katika nafasi ya maamuzi kwa muda mrefu na unazijua hizi chokochoko. Kwa hiyo, tunaporidhia hili Azimio lazima sasa akina mama tusimame kidete kwa jambo hili kwa kusema akina mama, siyo vibaya nikisema akina mama wenzangu tusimame kidete ili tuweze kusaidiana kuhakikisha kwamba suala la akina mama linapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii pia ni Waziri anayeshughulikia masuala ya asasi zisizokuwa za Kiserikali. Tunazo asasi nyingi sana zisizokuwa za Kiserikali zinazoshughulika na masuala haya ya mtambuka ya jinsia hasa masuala ya akina mama. Tunayo *TGNP*, *WLAC*, *TAMWA*, *TAWLA* na zinginezo nyingi zilizopo Mikoani. Nataka niseme kwamba bado sijaona kasi ya asasi hizi kuweza kuchochea kwa dhati kabisa maendeleo ya akina mama hasa huko vijijini. Kikubwa zaidi tumekuwa tukishuhudia wale wanaoendesha hizi asasi wamekuwa na kauli nzuri sana za kuhamasisha akina mama lakini unajua unapohamasisha kitu fulani inakuwa wewe ni mfano, bora ukitangulia kukifanya kile kitu kwa vitendo na wale ambao unawahamasisha watakufuata kwa urahisi zaidi, badala ya kuendelea kupiga kelele bila kufanya kile kitendo ili na wale watu wakaiga. Naomba wahamasishaji katika asasi hizi badala ya kubaki katika maeneo ya Dar es Salaam, au katika maeneo ya mijini watoke, waje mpaka Iramba, waweze kuwawezesha akina mama ili akina mama washiriki katika masuala mbalimbali ili waamini kwamba itakuwa ndiyo ukombozi wa mwanamke na ndiyo

tutahakikisha kwamba tunapokwenda katika masuala haya ambayo yamezungumziwa na Azimio hili kwa kweli tutakuwa tumejihakikishia kwamba akina mama wameimarika na sasa wanaweza wakajiwezesha wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuipongeza Serikali na hasa Mwanasheria Mkuu kwa tamko lake alilolitoa sasa hivi, ni tamko zuri ambalo kwa kiwango fulani lilikuwa linaleta mkanganyo kwamba kwa kufuata taratibu na sheria za nchi yetu, lakini mbali ya hizo na imani za dini zetu, jana Mheshimiwa Mongela alisema yeye ni Mkatoliki safi na mimi ni Muislamu safi, tunaposema katika dini zetu sisi tunaoamini kupitia kwa Mungu ukaja ukawa unaruhusu suala la utoaji wa mimba hata hizi zinazoitwa za dharura, ni kosa sana na kwa kweli lingeweza kutia doa katika Azimio hili na pengine Azimio hili lisingeungwa mkono au ingeonekana pengine tumburuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono Azimio hili, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Itifaka hii muhimu sana ambayo imewasilishwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Serikali kwa ujumla wake na Watanzania wote ambao wana nia njema ya kuhakikisha kwamba Itifaki hii inazaa matunda yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia katika kifungu hiki ambacho Tanzania tumeona kwamba kwa sasa tusikiridhie. Pamoja na kuunga mkono lakini labda niungane pia na hisia za nchi nyingine ambazo zimeona iko haja ya kuwa na kifungu kama hiki. Ni kweli lazima tutambue kwa uwazi kabisa kwamba Mwenyezi Mungu ameumba makundi ya wanawake na wanaume, ametutofautisha katika hisia zetu. Katika suala la upendo na mapenzi, mwanamke ndiyo anayebeba dhamana kubwa na ndiyo maana hata Wanasaikolojia wanasema hata ubongo wetu ulivyoubwa uko tofauti sisi ni kwamba kuna mtawanyiko kichwani, unaweza kuangalia mambo mengi kwa wakati mmoja, lakini mwanawake unakuta hisia zake zimekaa upande mmoja, hii ndiyo dhana halisi iliyopelekea watu kufikia kuona kwamba iko haja ya kuwa na kipengele kama hiki. Tatizo kubwa ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, *imagine* wewe mwanamke uko unafanya shughuli zako, huna ugomvi na mtu halafu, linatokea jibaba huko lilikotoka, hulijui likoje, linakuja linakubaka na pengine uko shambani, linabaka vikongwe, watoto na watu wa umri ambao haustahili, sasa hali kama hiyo inatengeneza chuki ya kupita kiasi. Tunafahamu kwamba upendo wa mtoto au maisha yake yanaanzia toka tumboni na wakati huo ndipo mtoto anapojengeka, sasa unapokuwa una kiumbe ambacho umekipata katika mazingira ya utatanishi ni tabu kubwa sana kwa mama. Lakini tunasema kwamba pamoja na hali hizo zinazojitokeza, nawaomba akina mama wezangu tuvumilie kama ambavyo tunavumilia kila siku, tusiingie katika mtego huo wa kutoa mimba, tuvumilie kumtunza kwa sababu

Mungu mwenyewe kwa sisi tunaoamini anaweza akakupa kiumbe chenye tabia tofauti na uliyoyatarajia na hakika akatengenezwa na akawa mtoto mwenye faida. Kwa hiyo, tuweke zaidi uvumilivu katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea katika Itifaki hii ambayo niseme wazi kwamba utunzi wake ukiufuatilia ni *feedback* ya mambo mbalimbali ambayo pia Tanzania tumekuwa tukiyafanya na nashukuru sana kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kunichagua kuwa katika mojawapo ya wawakilishi katika *SADC Forum*, nimehusika pia katika kuiangalia Itifaki hii katika hatua zake za utungaji na hivi kuchangia mambo mengi kufuatia uzoefu ulioko Tanzania. Kwa hiyo, uzoefu wetu pia umeweza kuchangia katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Tanzania tunatambua umuhimu wa kuheshimu na kuthamini jinsia zote bila kujali walemavu, wazee, wanaume au wanawake, tunahitaji usawa ulio sawa kweli. Katika Itifaki hii, ninachopenda kuchangia hapa ni suala la elimu. Hivi karibuni tumekuwa tukizungumzia umuhimu wa elimu kwa Mtanzania yeyote tungetamani sasa wale ambao wamepata mimba wakiwa shule warejeshwe mara moja baada ya kujifungua. Lakini si hivyo tu, tunaomba Muswada wa Sheria za Walemavu uletwe mara moja na vilevile katika utoaji wa mikopo nafikiria mtu akishakuwa mlemavu, niliwahi kuchangia hivyo na na bado nasisitiza, kitendo kile cha kuwa mlemavu tayari huyu mtu amepungukiwa kwa sababu Katiba yetu inaruhusu upendeleo ule wenye nia njema, mimi nazidi kushawishi walemavu wawezeshwe kusoma bure katika ngazi zote ili mradi sifa za kuingia katika ngazi hizo zitakuwa zinakubaliwa. Si kusoma tu wawezeshwe na vifaa vya kufikia shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulemavu ni taabu, mimi ninao watoto walemavu, nafahamu, najitahidi sana kuwa-*support* wajisikie sawa na watoto wengine. Inawezekana kama tunawaweka hivyo, kwa mfano, baiskeli, mzazi mwingine anaweza akawa hana uwezo wa kununua baiskeli ya kuenda shule lakini ikatokea Serikali imemwezesha ikamsaidia huyu mtoto kwenda shule. Kwa wale wanaokuwa vijiwani usiku wanaomba, hivi kweli tuna furaha gani kuona walemavu wamekaa pale kwenye taa wanaomba mpaka saa nne za usiku, usalama wao uko wapi? Mimi nimejaribu kuongea nao, wengine wanasema kuna watu wenye heshima zao wanawabeba usiku, wanawapeleka wanakojua na wanawarudisha. Kwa hiyo, wanakuwa katika mazingira hatarishi. Nchi hii katika kuridhia Itifaki hii, tuone zaidi haya maeneo ambayo kwa kweli yana maumivu makubwa kwa watu wa eneo hilo, tuwasaidie walemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijikite katika Ibara ya 66 (1) ya Katiba. Ibara hii inazungumzia kwamba kutakuwa na Wabunge wanawake ambao watapatikana kwa asilimia isiyopungua 30 ya Wabunge wote. Tanzania kupitia Serikali yake na Chama cha Mapinduzi katika Ilani yake, kimedhamiria kwa dhati kuona kwamba ifikapo mwaka 2010 mwishoni, Wabunge wanawake wanakuwa asilimia angalau 50 au kama kuzidi basi asilimia moja si mbaya kwa lengo la kuona kwamba Watanzania wanapata maendeleo ya haraka na baada ya kutambua kwamba wanawake ni nguzo kuu ya maendeleo katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia Katiba pamoja na dhamira nzuri ya Chama cha Mapinduzi na Vyama vingine ambavyo ni vya Upinzani ya kutaka wanawake wafikie asilimia 50 kwa 50, naona kifungu hiki kina kikwazo kwa sababu, kwanza tuna idadi maalum ya Wabunge wanaotakiwa wakae katika ukumbi huu nadhani hawazidi 360; kwa kuwa tuna idadi ambayo ni *fixed* ina maana hata kama tukaamua kuongeza asimilia ya Wabunge wanawake kwa Viti Maalum kwa asilimia 50 basi ina maana hatutaweza kuzidi kufikia Wabunge wa Viti Maalum 130. Kwa hali ya sasa kwenye Majimbo, Wabunge wanawake hawazidi 18, kwa maana hiyo ni kwamba ukiwajumlisha watakuwa ni 148 au 150 lakini wanaume watakuwa 200 na kitu kwa hiyo tutakuwa hatujafikia hiyo asilimia 50. Kwa hiyo basi, kuna haja ya kuwa na uwezeshaji maalum kwa upande wa Wabunge watakaolingia katika Majimbo ili kuhakikisha kwamba asilimia kubwa nyingine inatoka kwenye Majimbo na ile asilimia ya Viti Maalum kuweza kufikia asilimia 50 kwa 50 kama itapungua au kuzidi basi asilimia moja si mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine tumekuwa tukipata uzoefu katika nchi mbalimbali. Kuna wenzetu kwenye lile la Bunge la SADC, kwamba ninyi Tanzania mmetumia *affirmative action* ya kuwa na Viti Maalum lakini hii bado inawaweka ninyi kuwa wanyonge. Tukasema hapana lengo ni kumwezesha huyu mwanamke asogee. Matokeo yake, nchi zile ambazo hazikufanya hivyo idadi badala ya kuongezeka imekuwa ikipungua. Kwa hiyo, kuna haja ya kuulinda hatua hii mahsusi ya kuwawezesha wanawake lakini sasa uwezeshaji huo usiwe katika ngazi ya Ubunge peke yake uanzie ndani ya Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa lile kongamano la wanawake tulilolifanya pale Ubungo, tulisikia maneno kutoka kwa wanawake wenzetu, kuna vyama vinafanya uzalilishaji mkubwa kwa wanawake. Namna ya kuingia kuwa Mbunge, namna ya kupata nafasi na nikizungumza hapa sichagui Chama nazungumza kama mwanamke, kuna tabia ambazo hazivumiliki. Ndiyo maana nasema kwamba kumnyanyasa mwanamke ni kitu kibaya iwe ndani ya Chama changu cha CCM au Vyama vyovyote vile. Utaratibu wa Wabunge wa Viti Maalum na eneo lao la kufanyia kazi, haujawa wazi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu jinsi tunavyoingia na kwa Sheria iliyopo na Katiba inasema kwamba Vyama vya Siasa ndivyo vitapendekeza na kupeleka orodha kwa Msajili wa Vyama, sasa hiyo orodha inapatikana vipi?

NAIBU SPIKA: Kwa Tume.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Kwa Tume ya Uchaguzi, sasa kwa bahati mbaya kwa sababu hakujawa na uwazi katika kuwapata hao wanawake katika kila Chama na kwa sababu hakuna njia *uniform* kwa Vyama vyote, ina maana Chama chochote kinaweza kujifanyia kinavyotaka. Sasa hapo tunakuwa sisi wanawake tumewezeshwa lakini hatujawezeshwa vizuri kwa sababu kuna maeneo yanatunyanyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata katika kufuatilia kazi zetu, mimi Manyanya nasema ni Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Ruvuma na kwa sababu

walinichagua wale wanawake wa UWT Mkoa wa Ruvuma, nachukulia eneo langu la kazi ni Mkoa wa Ruvuma lakini Mbunge aliyeibuliwa tu kutoka katika sura nyingine hajui yeye yupo kwenye eneo gani au anafanya kazi zake kadri anavyopangiwa na Chama chake. Kwa hiyo, kwa sababu Wabunge wote tunalipwa pesa ya Watanzania na hivi tunafikiria namna ya kudhibiti rushwa, namna ya kuhakikisha mtu anafanya kazi kufuatana na anavyolipwa kama ambavyo Mbunge wa Jimbo anadhibitiwa kwenye eneo lake, kwa nini kusiwe na uwazi katika maeneo ya kazi ya Wabunge wa Viti Maalum. Naona hiyo ni sehemu mojawapo ya kutunyanyasa, tunataka tufanye kazi kwa kujivunia, tukifahamu eneo letu ni lipi na niweze mimi kupima vizuri kazi zangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna huu Mfuko wa Jimbo ambao utakwenda kwa ajili ya kuhamasisha wananchi katika maendeleo Majimboni. Mfuko ule ukitumika vibaya ndiyo kiboko cha wanawake ambao hawajaingia kwenye Majimbo kutokuingia. Tuliunga mkono baada ya kutambua umuhimu wake lakini tunataka na tunaomba Serikali iweke utaratibu ambao utatambua kazi za wanawake Wabunge na maeneo ambayo watakuwa wamepangiwa ili nao shughuli wanazozihamasisha, ziwe zinapata nguvu ya Mfuko huo na hii itaonyesha wazi kwamba wanawake wamewezeshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa pole kwa Watanzania wote na familia ya Mzee Kawawa, kwa kumpoteza Mzee wetu, namwomba Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi roho ya Marehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Waziri na Naibu Waziri, kwa kuweza kutuletea Azimio hili la Kuridhia Itifaki ya Jinsia na Maendeleo ya *SADC*. Nikizingatia Ibara ya pili na ya tatu, Itifaki hii ina lengo la kumwezesha mwanamke katika nyanja zote, ina lengo la kuleta usawa wa kijinsia na ina lengo la kuondoa ubaguzi katika nyanja zote za kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile Itifaki hii inataka kila nchi ambayo ni mwanachama wa *SADC* kuhakikisha kwamba baada ya kuridhia Itifaki hii, inarekebisha sheria zake ambazo zina ubaguzi wa kijinsia na inaweka mipango na mikakati ya kuhakikisha wanaleta usawa wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 17 ya Itifaki hii inasisitiza umuhimu wa kumwezesha mwanamke kiuchumi. Napenda kuipongeza Serikali kwani hata kabla ya Itifaki hii kuletwa, wao walishaanza kuhamasisha akina mama na watu wote ambao kipato chao ni kidogo, wajiunge pamoja, waingie kwenye Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) kusudi kupitia *SACCOS* hizi waweze kupata mitaji na mitaji hii iwawezesha kuboresha kilimo chao au shughuli zote za biashara wanazofanya. Ibara hii inasisitiza umuhimu wa elimu ya ujasiliamali. Ukiangalia wanawake wengi walichangamkia mpango huu wa Serikali wa *SACCOS* na kweli wamepata mikopo midogo midogo na

wanafanya shughuli nyingi sana. Akina mama ni wafanyakazi, ni wachapakazi sana na wanachangia kwa kiasi kikubwa sana katika pato la Taifa lakini wengi unakuta huyu akianzisha *salon* kesho yake na mwingine anaanzisha *salon* akifikiria bila shaka mwenzangu kapata faida. Huyu akianzisha duka la vyombo na mwingine anaanzisha duka la vyombo. Akianzisha Mama Ntilie na jirani yake anaanzisha Mama Ntilie. Hii ni kwa sababu wanakosa elimu sahihi ya ujasiriamali. Kwa hiyo, ninachopendekeza hapa ni kwamba elimu ya ujasiriamali kama Itafiki hii inavyoeleza inabidi itolewe. Kwa hiyo, Serikali ingeweka mkakati wa makusudi kuhakikisha kwamba elimu ya ujasiriamali inatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunatambua kwamba wanawake wengi wanakosa kufaidika na mikopo na mikopo mikubwa tunajua kwamba inatoka kwenye mabanki lakini wanawake wengi hawawezi kuipata hii mikopo kwa sababu unakuta kwamba wanatakiwa kuwa na dhamana. Hata ukimkuta mwanamke aliyeolewa labda ana kiwanja na mume wake wamejenga nyumba katika mazingira ya kawaida unakuta kwamba hicho kiwanja na nyumba vinakuwa katika majina ya mwanaume. Kwa hiyo, inakuwa vigumu kwa huyu mwanamke kuweza kutoa dhamana aweze kupata mikopo mkubwa. Kwa hiyo, ninapendekeza kwamba uwepo mpango wa makusudi kama *affirmative action* ya aina fulani ili kuwawezesha wanawake kupata mikopo mikubwa kutoka kwenye benki zetu na wao waache kufanya biashara ndogo ndogo waweze kufanya hata biashara kubwa kama wenzao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 13 na Ibara 12 zinazungumzia uwakilishi na ushiriki wa wanawake katika mambo ya uongozi na nafasi mbalimbali za uwakilishi na maamuzi. Napenda kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwani kwa miaka mingi, nafasi za uongozi wa wanawake zimekuwa zikiongezwa vijijini kwenye vitongoji, kwenye Serikali za Mitaa, Madiwani wamekuwa wakiongezeka mwaka hadi mwaka hata Wabunge. Kwa nia hiyo hiyo, ndio maana Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005, Ibara ya 120 inaeleza wazi kwamba wanalenga kuongeza ushiriki wa wanawake katika uongozi na nafasi nyingine zozote kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2010 ambao ni mwaka huu. Hiki kitu kilikwishaazimiwa na Umoja wa Afrika. Naipongeza CCM kwani hata kabla ya kuletwa Itifaki hii, wao walikuwa wanakwenda mbele kwenye kuleta usawa wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza Ilani na Itifaki hii kwa vitendo, napendekeza kwamba Ibara ya 66(1)(b) irekebishwe na kuruhusu wanawake Wabunge na Madiwani wawe siyo chini ya asilimia 50 ya Wabunge na Madiwani wote. Vile vile Sheria ya Uchaguzi na Sheria ya Vyama vya Siasa, ivitake Vyama vyote vya Siasa, wawateue wanawake. Hili ndilo tatizo, haiwezekani katika Tanzania hii sasa hivi tunao wanawake 18 tu Wabunge wa Majimbo ambao ndio wamechaguliwa kwa ridhaa ya wananchi. Sasa hivi Tanzania tunao wasome wengi lakini tukienda kwenye Vyama vya Siasa wanawake hawateuliwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile inabidi wananchi waweze kuandaliwa kwa sababu ukimsimamisha mwanamke hapa na mwanaume bado kuna jamii ambayo wanaona kiongozi wa kisiasa anastahili awe mwanaume. Sasa najiuliza Serikali tumefanya nini kumwezesha yule mwananchi aweze kuona kwamba huyu mwanamke ni

msomi vya kutosha, ana uelewa wa kutosha, anastahili kutuwakilisha. Kwa hiyo, napendekeza kwamba Sheria za Uchaguzi na Sheria za Vyama vya Siasa viwatake sasa Vyama vya Siasa viweze kutekeleza haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii inatambua na inahimiza wanachama kuweka mikakati makusudi kwa maana ya *affirmative action* ili kuondoa vipingamizi vilivyopo na ili kuboresha mazingira ya kumwezesha mwanamke kushiriki sawa katika nyanja zote. Ili kutekeleza Itifaki hii ya Jinsia na Maendeleo ya *SADC* na kuleta usawa wa kujinsia napendekeza yafuatayo:-

Kwanza, Ibara ya 12 na 13 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya haki na usawa zizingatiwe.

Pili, Ibara ya 66(1)(b) na ya 78 zinazotambua kuwepo kwa *affirmative action*, mkakati wa makusudi wa kutambua Wabunge Viti Maalum, uendeleo kuwepo kwa sababu kama nilivyoeleza haya matatizo mengine yaliyoko kwenye jamii yatakuwa hayajatoka *still* tunahitaji *affirmative action*. Kwa hiyo, napendekeza iendeleo kuwepo kwenye Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Katiba hii inamtambua Mbunge wa Jimbo, inamtambua Mbunge Viti Maalum lakini Mbunge wa Jimbo inaelezwa yeye anatakiwa kufanya kazi katika eneo lipi pamoja na kuwa Mbunge wa Viti Maalum anatambuliwa na Katiba lakini haielezi Mbunge huyu anafanya kazi katika eneo lipi. Matokeo yake ni kwamba Wabunge wa Viti Maalum wa Chama Tawala cha Mapinduzi wanawajibika katika Mkoa mzima, unakuta mtu anafanya kazi katika Majimbo 10 yaliyo katika Mkoa, unakuta mtu anafanya kazi katika Majimbo sita yaliyo katika Mkoa, hapa anafanya kidogo, hapa kidogo matokeo yake hata kazi anazofanya hazionekani, wala hazithaminiwi kwa sababu zimesambaa maeneo yote. Lakini sioni inashindikana nini Serikali kuweka sheria kwamba umeshachaguliwa Mbunge Viti Maalum eneo lako ni fulani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wa Viti Maalum wa Chama cha Mapinduzi tunafanyakazi kwenye Mikoa, msiniulize Wabunge wa Viti Maalum wa Vyama vingine vya Siasa maeneo yao ni yapi. Wengine labda ni Taifa au Mikoa sijui. Sasa ingekuwa ni vizuri basi ili kuleta usawa wa kijinsia tunaozungumzia hata maeneo ya kufanyia kazi yakaweza kutambuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza ili tuweze kutekeleza hii Itifaki kivitendo, haya yafanyike, kwanza Sheria za Uchaguzi na za Vyama vya Siasa ziwatake Vyama vya Siasa viwe na utaratibu ulio wazi wa namna gani hawa Wabunge Viti Maalum au Madiwani Viti Maalum watapatikana kwa sababu kama mlivyokwishaelezwa wengine wananyanyasika kijinsia kusudi waweze kupata nafasi hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Wabunge Viti Maalum baada ya Uchaguzi Mkuu watangazwe na Tume ya Uchaguzi kama Wabunge wengine na maeneo yao ya

kufanyia kazi yatangazwe. Wanaweza wakapangiwa labda Wilaya kadhaa katika Mkoa lakini basi wapewe eneo ambalo liko *manageable*, wanaloweza kulifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge Viti Maalum nao wapewe vyeti. Baada ya uchaguzi, ni Wabunge wa Majimbo tu huwa wanapewa vyeti lakini Wabunge Viti Maalum hawapewi chochote, sasa wanatambulika vipi? Ni vitu vidogo vidogo lakini na wao wapewe ili kusudi watambulike kama Wabunge wa Majimbo ili kuleta usawa wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Azimio la Kuridhia Itifaki hii, limeletwa mbele yetu, uwezekano mkubwa ni kwamba tutaliridhia lakini haitoshi itabakia kwenye karatasi kama mikataba mingine ya Kimataifa na Kikanda tunayoisikia au tuliyowahi kuiridhia. Kwa hiyo, ili Itifaki hii iweze kutafsiriwa kivitendo, nashauri kwamba Sheria za Uchaguzi, sheria zinazomgusa mwanamke kwa mfano zinazomnyanyasa kwa mfano Sheria ya Ndoa, Sheria ya Ardhi na kadhalika zote zirekebishwe. Lakini vile vile zitungwe kanuni za kuhakikisha kwamba tunaupata huu usawa ambao umelengwa na Itifaki hii. Kama nilivyotangulia kusema, Itifaki ni nzuri sana lakini isipotekelezwa kwa vitendo yatabaki maneno matamu tu yaliyobaki kwenye *shelve*. Kuwe na mpango mkakati wa makusudi wa kumwezesha mama kupata usawa wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, namshukuru Waziri, Itifaki ni nzuri, imeletwa muda muafaka wakati tunakaribia uchaguzi na bahati nzuri hata hizo Sheria za Uchaguzi bado hazijapitishwa. Kwa hiyo, ni mategemeo yangu kwamba haya mambo yote yaliyoelezwa kwenye Itifaki hii yatazingatiwa kwenye sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Itifaki hii. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa hii Itifaki lazima iishie kipindi hiki cha asubuhi, naona nitakayemwita sasa Mheshimiwa Anna Lupembe atakuwa msemaji wa mwisho kwa upande wa sisi Wabunge.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya mwisho kwa kunitambua sasa. Nami niungane na wenzangu kuhusu kuunga mkono Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Jinsia ya Maendeleo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchini za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Waziri, kwa kutuletea Itifaki hii ambayo itatuletea manufaa mengi makubwa katika nchi yetu ya Tanzania. Kwanza kabisa, nianze kutoa mchango wangu kuhusu suala la UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii itatusaidia sana kutokana na kwamba waathirika wa UKIMWI wapo katika maeneo mengi hususani vijijini, mijini na kuna mashirika na *NGOs* mbalimbali ambazo zinawasaidia kwa ukaribu zaidi na kutoa semina kwamba yeye kama mwaathirika wa UKIMWI afanye nini. Lakini maeneo ya vijijini hakuna wanaofika maeneo yale, walioathirika na UKIMWI wa vijijini wanakufa kutokana na kutokujijua na vilevile kutojua wafanyeje. Vijijini kule tuseme zahanati zetu,

hizi dawa za kuongeza siku, hospitali nyingi za vijijini, hakuna. Sasa unakuta mgonjwa wa UKIMWI akienda kwenye zahanati au akiwa nyumbani, wengi wao kule vijijini wanakuwa nyumbani, wananyanyapaliwa sana. Unamkuta labda mama au baba ni mgonjwa akizidiwa ndugu wa yule mgonjwa wengine wanadiriki hata kumfungia hatimaye kufariki. Hiyo ni kutokana na kukosa maelekezo mazuri, semina mbalimbali ambazo zinazofanyika huku maeneo ya mijini, kule vijijini hakuna. Vilevile mijini kuna lishe mbalimbali ambazo zinapatikana katika maeneo mengi ya hospitalini, lakini vijijini hakuna lishe zozote ambazo zinaenda katika maeneo ya zahanati, vituo vya afya pamoja na *dispensary* zetu. Katika Itifaki hii tungeomba Wizara kama Wizara sasa hivi iweze kupita maeneo mbalimbali kujua waathirika wa UKIMWI huko vijijini wanasaidiwaaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuja kwenye masuala ya ndoa, akinamama wengi katika ndoa zao wananyanyasika na mama ndio mlezi mkuu wa nyumba. Unakuta mama ni mama wa nyumbani, kipato hana, anategemea labda baba akitoka ndio amwachie chochote kwa ajili ya watoto. Lakini unakuta wakati mwingine baba anadiriki kuondoka nyumbani haachi hata senti tano, akimuuliza mwenzangu mbona leo hujaniachia anasema sina, ina maana yule mama sasa aanze kuhangaika, huo ni unyanyasaji! Yule mama sasa aanze kutumia akili yake mwenyewe ili wale watoto wale siku hiyo au unakuta saa nyingine wako shuleni, mtoto anakuja kwa mama, mama ninaomba hela ya daftari, *pencil*, mama nimefukuzwa shule, sijapeleka ada, mama yule aanze kuhangaika, baba akirudi jioni akiambiwa anamwambia mama sina kwani wewe hujui jinsi gani ya kutafuta, huo ni unyanyasaji wa jinsia, akina mama wengi katika ndoa zao wanapata tabu sana. Sasa kutokana na hii Itifaki ambayo iko mbele yetu nafikiri itasaidia sana hawa akina mama ambao wananyanyasika katika ndoa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la watoto wanaonyanyasika, nasema watoto wanaonyanyasika kwa sababu gani? Unakuta wazee, watu wazima na akili zao wanaenda kumtongoza mtoto wa darasa la pili, mtoto wa miaka sita, saba, mtoto mdogo, huo si unyanyasaji? Anaenda kumnyanyasa mtoto mdogo, anaenda kumbaka mtoto mdogo, huo ni unyanyasaji wa jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna watoto ambao wako mitaani kwa mfano Dar es Salaam unavikuta vitoto vimekaa kwenye laini ya magari, mimi kila siku najiuliza hao watoto wametoka wapi, watoto wadogo! Je, Wizara kama Wizara wale watoto wanaozurura pale Dar es Salaam, hatuwaoni? Ile si unyanyasaji wa jinsia? Ninajua kuwa kuna watoto ambao wengine mama zao wako pale pale pembeni yao wanaombaomba kwa nini Serikali isijipange vizuri, ikaenda kuwachukua wale watoto kwa lazima? Tunasema kuwa Itifaki hii ina maana kuwa unyanyasaji huu uishe, ina maana kuwa Wizara iende ikatafute wale watoto wanaozurura ovyo kule na kuombaomba hela, watoto wale wanatakiwa waende shule. Ninaomba na wale akinamama wanaokaa mle pembeni ingawa wanakaa pale barabarani bado wanazaliana wakiwa pembeni mwa barabara ile. Sasa mimi huwa nakaa najiuliza, je, hawa akinamama wanaomba lakini unamkuta hapo hapo ananyonyesha mtoto mdogo vilevile mtoto yuko pembeni wa miaka mitano, miaka minne, miaka mitatu, miaka miwili wanaomba, Serikali inachukua hatua gani? Tunasema ni maskini lakini unakuta wengine wana hali nzuri, ni mtu mzima, anasema vizuri, anatembea vizuri, je, Serikali inachukua hatua gani ili Itifaki hii isitubane kwa kusema

kuwa wale watu tunaowaacha vile tunawanyanya? Naomba Serikali ichukue hatua kwa watu wale ambao ni wengi sana Dar es Salaam, Mikoa mingine ni sehemu chache sana ambazo utawakuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuja upande wa mirathi, inasikitisha mirathi inavyowasumbua akinamama wengi. Mama mjane huyu amefiwa na mume wake lakini mirathi inachukua miaka kumi, ishirini na wengine wanakufa huku wanadai mirathi ya waume zao, anahangaika hii mirathi watoto alioniachia mume wangu nikipata pesa niwasomeshe, ile mirathi yule mama anafuatilia mpaka na yeye mwenyewe anakufa, unakuta watoto wanaanza kufuatilia mirathi hawapati ile mirathi inakuwa shida. Huu ni unyanyasaji. Ninaomba kwenye kipengele cha mirathi, Serikali iangalie kwa umakini sana, akina mama wanapata tabu au uwekwe mfumo ambao hao akinamama watapata mirathi yao kwa ukaribu, maana unakuta mtu anafariki Sumbawanga, labda alikuwa Mwalimu, yule mama atachukua *documents* zote atapeleka Halmashauri ya Wilaya, akifika pale yale makaratasi sijui yanatupwa, pale tu yanaweza yakakaa mwezi mzima au mwaka mzima au miaka miwili ikatoka pale ikaja Hazina, ikifika Hazina ndio kabisa ndio watu wanasahau. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huu ni unyanyasaji mkubwa sana akinamama wengi wameathirika, watoto wengi wameshindwa kwenda shule kutokana na kwamba wazazi wao au baba yao amefariki, mirathi hakuipata. Matokeo yake yule mtoto kama ni mtoto wa kike anatakiwa aolewe kabla ya muda na unakuta mtoto wa kiume mama yule ameshindwa kumsomesha anavuta bangi maana hajui aende wapi au anakuwa jambazi. Tunaomba Serikali huu mpangilio wa mirathi uangaliwe upya, huu ni unyanyasaji. Ninaomba elimu basi ipite, waeleweshwe wale akinamama wajane ambao wako sehemu mbalimbali katika Mikoa, Wilayani, wajue jinsi gani ya kuweza kujisaidia kama mume wake amefariki, elimu ipitishwe. Tunasema usawa wa mwanamke, usawa wa mwanamke utatoka wapi wake mwanamke huyu anadai haki ya mume wake lakini hapati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo naomba niishie hapa, naunga mkono Itifaki hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili ni zuri sana, linahitaji utekelezaji kwani kulipitisha peke yake haitoshi. Kwa kuwa Maazimio mengi hupitishwa Bungeni lakini hayana nguvu kisheria; ni vema baada ya Azimio hilo kupitishwa, sheria zote zinazomkandamiza mwanamke zianganaliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi kama Rwanda, wamepiga hatua sana kwenye masuala ya jinsia. Usawa unaonekana kirahisi, wanawake wana haki sawa na wanaume kuanzia kwenye kila kaya mpaka kwenye nafasi za uwakilishi. Wao ni mfano mzuri Afrika.

Tatizo la mila na desturi limekuwa kisingizio cha kuendelea kukandamiza haki ya mwanake. Wenzetu wa Rwanda, mila na desturi haziwezi kuwa juu ya sheria au sawa na sheria. Ni kosa kutekeleza mila inayomkandamiza mwanamke, kwa mfano, Sheria yao ya Ndoa inamtaka kila mwanamke na mwanaume wanapofunga ndoa, lazima kwanza wafunge ndoa ya serikali halafu ndio wafunge ya kidini. Hii ni kwa sababu wanataka utambuzi wa mke/mume halali serikalini ili inapotokea kutengana au mmoja kufa, mrithi halali afahamike; hakuna yeyote katika familia ya mume au mke anayeweza kuingilia mali iliyochumwa na wawili hao. Hivyo, mjane au mume anayeachwa, anatambulika kisheria kuwa ndio mrithi; lakini huku kwetu Tanzania, bado mila na desturi zina nguvu sana na manyanyaso yako dhahiri, inabidi sheria kali zitungwe na mila zisiwe sawa na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri tuwe na *Bureau of Gender*. Kazi ya *Bureau* au Baraza iwe ni kuhakikisha inasimamia utekelezaji wa mambo yetu yanayohusu masuala ya usawa wa kijinsia, mfano mzuri ni Finland wao wanayo hiyo *Bureau of Gender*, wanaangalia kila sekta kuanzia nyumbani, maofisini, Ofisi za Serikali na zile za binafsi, mashuleni, jeshini na kila mahali walipo wanaume na wanawake katika kuhakikisha hakuna unyanyasaji. *Maternity Leave* ni kwa wote; wanaume na wanawake, kwani zamani wanawake walikosa ajira kwa kuwa wana kipindi ambacho watakuwa na likizo ya uzazi.

Naona ni muhimu kuwa na chombo hicho cha kusimamia masuala ya jinsia na kutambulika kisheria ili kufanya kazi yake ipasavyo, kwani kutaangalia kila sekta kwa kuwa suala la jinsia ni mtambuka kila kona lipo.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kuwa wanafanya kazi nzuri ya kutukuka, kuwatetea watoto, akinamama na wengine wote wenye mapenzi mema ya kuleta usawa na maendeleo hapa nchini na nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, sisi kwa pamoja bila kujali jinsia, tuendeleo kutetea usawa kwa akinamama kwenye maeneo ya uwakilishi kama vile Ubunge na Udiwani na pia tuendeleo kuitetea serikali iendeleo kutoa nafasi za kutosha kwa wanawake kwenye nafasi mbalimbali za utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuwa na usawa, nawashauri akinamama waende kwenye Kata, Majimbo na kadhalika, kugombea Udiwani na Ubunge na nafasi zote zenye ushindani hata kwenye vyama vya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwakilishi kwenye Udiwani Ubunge, nafasi za kisiasa, tusiteteo ukomo kwa sababu wanaojua ukomo wa wanasiasa ni wapiga kura; mtu anaweza kuwawakilisha wananchi kwa muda mrefu ilimradi bado ana uwezo na watu wale wanampenda.

Mheshimiwa Waziri, Itifaki hii izingatie sana haki za Watoto, Wazee na Walemavu. Nami kwa nguvu zangu zote, naunga mkono Itifaki hii, isipokuwa ibara ya 20(2)(a) na naomba Wabunge wote waiunge mkono.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze Serikali kwa kuleta Itifaki hii ili ipitishwe na Bunge.

Nampongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kusimamia vema Itifaki hii hadi kuiwasilisha leo Bungeni. Nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa jinsi alivyowasilisha mapendekezo na maoni ya Kamati katika Bunge Tukufu leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuridhiwa Azimio hili na Nchi Wanachama (SADC), linaletwa kwetu kuliridhia na kulitekeleza katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayapongeza Mashirika ya Serikali na yale yasiyo ya kiserikali, kwa kuweza kusimamia vyama na kutoa mafunzo mbalimbali kuhusu masuala yanayomhusu mwanamke na udhalilishaji wa mwanamke nchini.

Wanawake wengi walikuwa hawafahamu masuala mengi yanayohusu haki zao za msingi, hasa wale walio vijijini.

Utekelezaji wa Itifaki hii ni vema uzingatie yafuatayo:-

(a) Serikali iangalie utekelezaji wa Sheria ya Mtoto iliyopitishwa na Bunge inayohusiana na masuala yanayomhusu mtoto na unyanyaswaji.

(b) Uwezeshwaji wanawake kiuchumi na kijamii. Mara nyingi wanawake katika jamii huwa wanawekwa nyuma sana, hawana uhuru wa kutoa mawazo wala ushirikiano; hivyo, wanawake wanajikuta kuwa nyuma na kutokuendelea kiuchumi katika nyanja mbalimbali.

Serikali imejitahidi sana kutoa fursa nyingi za kumuwezesha mwanamke katika masuala ya ujasiriamali lakini jamii zimekuwa zikiwarudisha nyuma sana.

Katika utekelezaji wa Itifaki hii, ningeliomba elimu iwafikie wananchi wengi hasa walio vijijini kwa mantiki ya kutoa elimu kwa wote. Tunaamini sana kuwa, mwanamke anapowezeshwa, anaweza kuendelea rasilimali za aina zote.

(c) Utumikishwaji wa watoto. Mara nyingi tumekuwa tunapiga kelele kuhusu utumikishwaji, lakini mara kwa mara watoto katika baadhi ya maeneo utaona wao wenyewe ndio wanapenda kujitumikisha kwa ajili ya kutafuta maslahi kwa kubeba mizigo katika maeneo ya masoko, bandarini na kwengineko. Serikali inapochukua uamuzi wa kuwakusanya na kuwarudisha walikotoka wanarudia tena.

Naiomba serikali itekeleze Sheria ya Mtoto tuliyoipitisha ndani ya Bunge hili. Vile vile itafute uwezekano wa kupunguza gharama za masomo mashuleni ili wazazi walio maskini waweze kuwapeleka watoto wao mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wanafunzi wanaolazimishwa kuacha masomo kwa kisingizio cha ndoa; ni vema wazazi wa watoto hao wapewe onyo na kukomeshwa tabia hii ili kuweza kuwapa uhuru watoto wa kike kuendelea na masomo.

Wazazi wasisitizwe suala la kuwapa uwiano ulio sawa watoto wa kike na wa kiume, elimu na malezi yaliyo mema ili kujenga tabia za kupendana na kuheshimiana.

Baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja hii.

MHE. CHARLES N. MWERA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nichukue nafasi kutoa pole kwa Familia ya Marehemu Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa, kwa kumpoteza kiongozi mashuhuri aliyekuwa mwadilifu, shujaa na aliyetumikia nchi kwa uaminifu mkubwa. Kwa niaba ya Wananchi wa Tarime, naomba kutoa pole nyingi kwa Familia na Watanzania wote na Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amina.

Pili, nachukua nafasi hii, kumshukuru Waziri, Mheshimiwa Margaret Sitta na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina pingamizi na Azimio hili, kwa kuwa halipingani na Katiba ya Nchi; cha msingi ni kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kulifahamu hasa wanaoishi vijijini ili waweze kuwa na ufahamu mkubwa.

Tanzania ni nchi huru, tupo katika Dunia moja, ni lazima na muhimu kuridhia Itifaki ya Jinsia na Maendeleo ili kuweza kumjenga mwanamke kijasiri ili aweze kushiriki katika shughuli za maendeleo ili kujiletea maendeleo ya kifamilia, kijamii na Taifa kwa jumla.

Serikali iendeleo kutoa elimu kwa jinsia zote, maana kwa tafsiri, wananchi wengi wanafahamu kuwa jinsia ina maana ya mwanamke; ambavyo sivyoy.

Wanawake wapewe nafasi mbalimbali za kiutendaji, pamoja na nafasi katika vyama vya siasa. Akina mama wapewe nafasi wasome maana kwenye nafasi nyingi zinahitaji kuwa na sifa za kulingana.

Wanaume wenye tabia mbaya ya kuwabaka wasichana, Serikali isimamie sheria na wale wanaopatikana waweze kuhukumiwa.

Ni vema Itifaki ya Haki sawa kwa Mwanaume na Mwanamke kuonana kwa umri wa miaka kumi na nane, mimi sikubaliani na vijana kuoana chini ya umri wa miaka kumi na nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu wa shule zetu za Kata ziwe na Hosteli kwa ajili ya wanafunzi wa kike, hii itasaidia sana kuepusha upatikanaji wa wanafunzi wa kike kupata mimba na kwa vile watakuwa wanaishi shuleni, watapata nafasi nzuri ya kujisomea na ufaulu wao utakuwa mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za afya ziboreshwe, akinamama wajawazito wapate huduma nzuri ili wajifungue salama. Wataalamu, vifaa na madawa ni vitu muhimu. Itifaki itakuwa ya umuhimu kwa Watanzania kama afya ya akinamama, akinababa na watoto itakuwa bora ili waweze kufanya kazi kwa bidii. Huwezi kufanya kazi yoyote ile iwe ukulima au ofisini kama afya ni mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru kwa kupata nafasi hii. Ahsante.

MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kufika hapa na kuweza kuchangia Azimio hili. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kufanikisha Azimio hili, ambalo linatoa mwanga kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sasa napenda kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Naipongeza sana Serikali kwa kuweza kukitoka kifungu cha 20(2)(a), kinachohusu utoaji wa mimba. Mila zetu na dini zetu, hazikubali kitendo cha kutoa mimba; kufanya hivi ni kuua. Dhamira ya Azimio hili ni kumkomboa mwanamke katika hali ngumu ya kimaisha na usawa wa jinsia. Ukimtazama mwanamke, amekandamizwa sana na mila au mume kwa wale ambao wameolewa. Naiomba serikali ifanye kweli katika kumtetea mwanamke. Pia Azimio hili liwafikie walengwa mijini mpaka vijijini. Elimu itolewe kwa akinamama ili wajue haki zao. Ahsante.

MHE. HEMED MOHAMED HEMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake, pamoja na Wataalamu wote, kwa kuweza kutuletea Azimio hili lenye nia njema kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia tamko hili, ipo haja Bunge hili kulipokea kwa asilimia mia moja. Kwa vile ni haki ya Bunge kutoa mchango wake katika tamko hili, nami napenda kusema yafuatayo:-

Kifungu ama ibara ya tisa, inahimiza kuwepo kwa sheria zitakazowalinda walemavu na kuwasaidia kupata haki zao shirikishi.

Kwa kuzingatia haki za walemavu hapa nchini, utaona bado tunawatenga na kuwanyanyapaa. Tukiangalia Sheria za Barabarani katika nchi yetu, kuna alama nyingi zinazoonisha onyo kwa madereva, kwa mfano, mbele kuna kona, kuna shule, na kadhalika; imefika hadi maeneo ya mifugo kuoneshwa alama za picha ya ng'ombe ili madereva waendeshe magari kwa hali ya usalama; je ni alama gani inayomwonesha dereva kuwa barabarani kuna walemavu?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza serikali kwa kukikataa kipengele cha 20(2)(a), kinachohusu utoaji mimba, kwani mila zetu, tamaduni zetu na dini zetu, hazikubali mtu kuua. Kutoa mimba ni kuua.

Baada ya maelezo hayo, nasita kwa kusema namshukuru Mama Sitta.

MHE. DORAH H. MUSHI: Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uzima nami niweze kuungana na wenzangu katika kuridhia Azimio la Itifaki ya Maendeleo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*).

Nitoe rambirambi zangu za dhati kwa Familia ya Marehemu Rashid Mfaume Kawawa, Mungu ailaze roho yake mahala pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuzungumzia suala la mwanamke hasa mjane. Wajane na yatima wamekuwa wakinyanyasika sana. Utakuta mali, nyumba, mashamba, biashara na magari, hawa wawili walichuma pamoja na mara nyingi mwanamke ndiye mwangalizi wa mali hizi wakati wa uhai wa mumewe; inapotokea yule mume ameugua kalala tena hajafa, ndugu wa mume wanaanza vurugu na kusema kuwa yule mwanamke ndiye anayemroga mumewe hasa kutokana na Ugonjwa hatari wa UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu hawa wanaanza kumtenga yule mama, wanaanza kumhudumia wenyewe mgonjwa na wanaanza kugawana mali hata kabla ya ndugu yao kufariki. Anapofariki, wanamzuia kwenda kumzika mumewe. Hivyo, baada ya kumzika wanagawana zile mali na mjane na yatima wanabaki hawana kitu. Mjane akifugua mirathi hapewi haki, utakuta zile fedha zake ndizo zinamnyima haki. Matokeo, mama mjane na watoto yatima, wanarudi kuwa ombaomba mitaani. Hivyo, Itifaki hii itasidia sana kuwapatia haki wajane na yatima.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mtoto wa kike hasa anapokuwa amefanyiwa vitendo viovu kama vile kubakwa, utakuta mambo haya yanaishia kwenye familia eti kwa kuhofia au kwa kuona aibu. Wale wanaofanya hivyo, hawachukuliwi hatua yoyote hatimaye mtoto huyu anabaki na maumivu. Je, mtoto huyu aende wapi ili apate msaada wa kisheria ikiwa yuko kijijini? Elimu iendelee kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la watoto wa kike kutumika katika madanguro limekuwa likizungumziwa sana. Watoto wa kike wenye umri mdogo kati ya miaka 12 – 16, wamekuwa wakifanyiwa biashara hii ya unyanyasaji wa kijinsia na madanguro hayo yanajulikana lakini sijasikia hata mmoja aliyechukuliwa hatua za kisheria wala kupewa adhabu. Je, Serikali inakubaliana na madanguro hayo; kwa nini hatua kali zisichukuliwe iwe fundisho?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Siku ya Mwanamke Duniani (*International Women's Day*), inaadhimishwa Duniani kote kila mwaka; kwa nini Sikukuu hii isiadhimishwe Kitaifa kama Saba Saba na Nane Nane; wanawake wote washerehekee kuanzia ngazi za Kata hadi Taifa? Ni vema Sikukuu hii ipewe umuhimu wake, wanawake wakapewe jukwaa la kuzungumzia mambo yao, kutangaza bidhaa zao na biashara zao kwa ujumla.

Mchango wangu hi huo. Ahsante.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Nami naungana na Wabunge wenzangu wote waliochangia Azimio hili, kulingana na uzito ulivyo.

Kwanza, matatizo tunayoyapata; naomba nifafanuliwe kuna makabila mengi yananyanyasa akinamama; je, Azimio hili litafanikiwa bila Serikali kupeleka elimu mpaka vijijini ambako ndiyo kwenye matatizo kwa kuwa watu wachache wana uwezo wa kusikiliza vyombo vya habari?

Serikali iunde kamati iende mpaka chini kulingana na kazi nyingi zinazofanywa na akinamama. Uwezo wa wanawake wengi ni mdogo sana, kitu ambacho serikali ina uwezo wa kukabiliana nacho. Hivi sasa tunakwenda kwenye Kilimo Kwanza, mwanamke kama mwanamke, atatumia jembe la mkono ili aweze kukidhi haja yake. Naomba angalau wapewe matrekta na zana za kisasa zitakazoweza kuwasaidia akinamama. Vilevile ninapenda kuwashauri akinamama wajitokeze kugombea nafasi mbalimbali katika chaguzi zetu.

Naomba niainishe mambo ya kufanyia kazi kwa akinamama na watoto wa kike:-

Wasaidiwe kuondokana na mikopo inayowanyanyasa na kuwadhalilisha; wapewe zana za kilimo; wapewe semina mara kwa mara; wajane wasimamiwe na wasinyang'anywe mali zao; wajane walipwe mapema haki za waume zao ili waweze kulea watoto wao vizuri; iwepo sheria mwanamke kama mwanamke ajisimamie mirathi yeye mwenyewe na siyo kusimamiwa na mtu mwingine; wazazi wanaokatisha masomo watoto wa kike wachukuliwe hatua kali za kisheria; na pia Azimio hili liwalinde watoto wa shule wasitolewe mimba na wala wasibebeshwe mimba wakiwa masomoni.

Azimio hili lisaidie Wizara itoe vipeperushi sehemu mbalimbali vya kuelimisha na madhara yake. Sheria pia iende kwa madaktari wa kike wanaowanyanyasa wanawake wenzao wakati wa kujifungua. Kuna baadhi ya wanawake wana matatizo, wanashindwa kuwasaidia wanawake wenzao tofauti na wanavyosaidiwa na wanaume.

Naomba masuala haya yazingatiwe. Kuna wanaume wanawanyanyasa wanawake kwa kuwapiga na kuwavua nguo tena mbele ya watoto wao. Azimio hili likomeshwe mara moja. Naomba tusibaguane, tukipendana hata manyanyaso yatapungua.

Kwa hayo machache, naunga mkono hoja. Wanawake oyee.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuleta Itifaki hii kwa wakati muafaka na unaendana na maisha ya kila siku ya Mtanzania; iwe mjini au vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki iwe ya Wizara zote na inapopeleka taarifa yake kwenye Vikao basi ishirikishe Wizara zote, jamii na asasi mbalimbali katika kukusanya na kupata takwimu sahihi.

Wizara ya Jinsia; vyombo vya habari vishirikiane katika kulitafsiri Azimio na kulisambaza kwa wananchi ili waweze kulifahamu na kulitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kufungua Desk la Jinsia na Unyanyasaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasichana wanaopata mimba shuleni na kufukuzwa ni kuwanyima haki zao za msingi katika Itifaki hii; Wizara zinazohusika zikubaliane kuweka utaratibu utakaowasaidia kielimu wasichana hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Itifaki hii bila Ibara ya 20(2)(a).

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza mtoa hoja kwa uwasilishaji wa haja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati muafaka, hoja hii imetufikia. Wanawake sasa wameongezewa nguvu za Kikatiba, Kisheria na Kiutaratibu. Naamini wanawake tumepewa faraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza wanawake waongezwe katika nafasi za uongozi kwa njia za viti maalum, uteuzi na ushindani kupitia usaili na uchaguzi. Ninashauri kila eneo liwe na utaratibu mzuri ili mwanamke anayepata nafasi, uwezo wake uzingatiwe. Hii itaongeza uwezo wao na jamii itawatambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza pia elimu itolewe kwenye jamii nzima; wanawake na wanaume wote; mashuleni watoto wa kike wasome kwa kadiri wanavyoweza; na watoto wa kike walindwe ili wasiathiriwe na watu wenye nia mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ilianganalie hili la ongezeko la nafasi za wanawake kufukia 2015 kufikia 50 kwa 50, ni lazima vyama vya siasa viliunge mkono. Uteuzi wa wagombea wanawake uwe wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wanapogombea pia sheria iwalinde na lugha za kuudhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wajipe moyo, wawe wajasiri na wajitokeze kugombea nafasi mbalimbali bila woga. Haki haiwezi kusubiriwa ije yenyewe; pamoja na sheria hii, wanawake pia wajipigania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba utekelezaji.

MHE. MARGRETH A. MKANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Wizara kuhakikisha kuwa mkataba huu muhimu nchi yetu unairidhia haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kipengele cha 9 cha Mkataba kimesisitiza ulazima wa nchi mwanachama wa *SADC* baada ya kuridhia pamoja na masuala mengine, kutunga au kufuata sheria na taratibu mbalimbali ili kulinda haki za watu wenye ulemavu na maendeleo yao kutegemea aina ya ulemavu wao na hali za hatarishi wanazokumbana nazo katika maisha, hivyo kwa msingi huo, nasisitiza kwa vile leo tunaridhia Mkataba ni vema sasa ule Muswada wa Haki na Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu ambao unasubiriwa sana na walengwa uweze kuletwa Bungeni na kuujadili. Nalisisitiza suala hili kwa sababu nchi yetu naamini sana kuwa ni ya mfano mzuri katika kutekeleza yaliyomo katika MaAzimio mbalimbali tunayoyaridhia. Pia kwa vile Sera ya Watu wenye Ulemavu tayari ipo, Mkataba wa Kimatifa nao tuliridhia basi ni vema kisera na kiutaratibu tukakamilisha kuhusu jamii ya watu wenye ulemavu kwa kutekeleza hiyo miongozo tutakayojiwekea kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi naunga mkono Azimio hili kwa vile yote yaliyomo ni kwa faida ya wanawake, watoto wa nchi yetu.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mungu kwa kunijalia kunipa afya njema na kuniwezesha kuchangia Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutoa pongezi kwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote, kwa kuleta Azimio hili Bungeni ili liweze kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kuletwa Azimio hili Bungeni ni jambo zuri na la msingi na litawezesha wanawake kuwaondolea kero na uzalilishaji wa kijinsia na kutekeleza Sheria na Sera na kuleta usawa wa jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi wanachama wa *SADC* ni vyema kuzingatia vifungu vya Katiba za nchi zao ili kuondoa ubaguzi wa sekta mbalimbali na kutoa adhabu kwa wale watakaokwenda kinyume na sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wanawake wengi baadhi yao wanapata ulemavu wakati wa kujifungua kwa kupata FISTULA au matatizo mengine, sheria hii izingatie jamii ya watu wenye ulemavu kwani binadamu anaweza kupata ulemavu wakati wowote au wa kuzaliwa nao. Kwa hiyo, sheria hii iwaangalie kwa kuwasaidia na kuwatengenezea mazingira mazuri katika sehemu zao kazi kama wale walemavu wasioona wapatiwe mashine za kuandikia na vifaa vyenye kwa walemavu wa aina zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 10 inayozungumzia haki za Wajane na Wagane, kwa kweli nchi yetu inaguswa na matatizo mbalimbali ya kimila na kidesturi pamoja na kidini ikiwemo Islam wanataka sheria yao. Matatizo wanayopata wajane ni

mengi baada ya kufiwa na waume zao, hufukuzwa ndani ya nyumba pamoja na watoto wake, sheria hii ipendekeze kuwa mjane apewe nyumba, aishi na familia yake sio ndugu wa marehemu kuchukua mali na familia hiyo kukosa haki zao. Vilevile baba kuandika wosia ni vizuri kama ana madeni au kama amefariki mali yake asimamie mtu aliyemuamini ili kuitunza familia yake au mali ili ikamatwe na Serikali mpaka watoto wake wakue ili wakabidhiwe mali ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itoe tamko rasmi la kuwarudisha shuleni wanafunzi wa kike baada ya kujifungua ili waendeleo na masomo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeze Serikali kwa kuweka Azimio kuwa ifikapo mwaka 2010 wanawake wafikie asilimia 50 kwenye vyombo vya maamuzi na sekta mbalimbali za Serikali na vilevile tunaipongeze Serikali kupitia Wizara ya Jinsia kwa kuanzisha Benki ya Wanawake ili kutukwamua kimaisha na kutuwezesha kupata mikopo ya kutusaidia. Nawaambia wanawake wenzangu wajitokeze kwa wingi kununua hisa ili Benki yetu ikue kwa manufaa ya wanawake na Watanzania kwa jumla na vile vile wapewe elimu hasa vijijini kuhusu benki yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu, naunga mkono Azimio hili namtakia kila la kheri Waziri na Naibu Waziri na timu yake, kwa kazi nzuri.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote, kwa kuweza kuleta Azimio hili la Kuridhia Itifaki la Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya *SADC* ambayo ni muhimu sana kwa nchi zetu hasa Bara la Afrika ambalo kwa kiasi kikubwa lina mila na desturi za kugandamiza sana wanawake aidha kwa kuwabagua, Itifaki hii itasaidia sana kuleta usawa katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 14 inayozungumzia kupata elimu kwa usawa (bila ubaguzi wowote), kwa sasa hivi wanafunzi wa kike wakipata mimba wakiwa shuleni huwa wanafukuzwa na kukosa fursa ya kuendelea lakini mara nyingi yule wa kiume unaweza kukuta ni mtu mzima au kamaliza shule asipojulikana yeye ataendelea na shughuli zake kama kawaida. Serikali ina mpango gani na huyu mtoto wa shule anayekatiza masomo na kufukuzwa na haruhusiwi kuja kuendelea na shule? Je, huu usawa wa elimu utatekelezeka kwa mtindo huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara 27, kuhusu maambukizi ya VVU, pamoja na Bunge letu kupitisha Sheria yenye kutoa adhabu kwa wenye kuambukiza VVU kwa makusudi bado hili ni tatizo kubwa, wanawake na wasichana wadogo wanaambukizwa sababu ya umaskini wetu. Ushauri, Serikali ingeangalia au kuzungumza na Benki ili wawapatie akina mama mikopo yenye riba nafuu labda kwa kuwa na shughuli ya msingi hataweza kudanganywa kirahisi ikiwa ni pamoja na elimu kwa wingi zaidi itolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 10 inayozungumzia haki za Wajane na Wagane, hii ni muhimu sana hapa kwetu kwa sababu mwanamke akishafiwa na mume wake kuna baadhi ya makabila hana ruhusa kabisa ya kusimamia mali walizochuma na

marehemu mumewe. Kwa baadhi ya jamii hata watoto wa marehemu hawaruhusiwi kabisa kusimamia mali za baba yao na mwishowe huja kuwadhulumu mali zote na wengine kufikia kufukuzwa hata kwenye nyumba waliyokuwa wanaishi. Ni mategemeo yangu kwamba Serikali itahakikisha ile Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inaletwa haraka Bungeni na kubadilishwa ili nchi iweze kuendana vizuri na hili Azimio la *SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Tisa, inazungumzia Sheria zitakazowalinda walemavu na kupata haki zao. Ninashauri Serikali isisitize kwa kuanzia basi katika shule, makazi ya watu, mazingira rafiki kwa walemavu yawepo maana ni maeneo mengi hayana sehemu za watu wenye ulemavu kupita au hata kujisaidia. Ni matumaini yangu Serikali italichukulia suala hili kwa umuhimu mkubwa.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono. Azimio hili linatokana na Azimio la Beijing ambalo lililoridhia Sera ya Usawa wa Jinsia, suala hili ni muhimu kama tukiungana na *SADC*, kutakuwa na nguvu ya pamoja kumwezesha mwanamke kujua haki zake pia kuondokana na umaskini uliokithiri kwa wanawake hasa vijijini pamoja na hayo, itasaidia kuondoa Mfumo Dume uliopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika muunganiko huu, utasaidia kusimamia suala zima la kuhakikisha hakuna ndoa za utotoni ili wasichana wote wapate elimu. Pamoja na hayo adhabu kubwa itolewe kwa wale wote watakaobainika kuhusika na vitendo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kusimamia adhabu kwa wale wote watakaobainika kuuza dawa za kulevya ili watoto wa kiume nao wasiathirike, ambao huwatumia kuuza dawa hizo na kukatisha masomo. Kwa ufahamu uliopo ni kwamba nchi zilizoungana na ambazo zinashirikisha jinsia ndizo ambazo zina maendeleo makubwa, kwani mchango wa wanawake katika jamii ni mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuteua jinsia katika siasa na utaalam pia kwa kuvalia njuga suala 50/50 kwa mwaka 2010. Niwapongeze *TGNP*, *TAWLA*, *NOLA*, *WLAC*, kwa elimu wanayotoa katika jamii, kuhusu haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili pia lisaidie nchi ambazo zina vita, kwani wanaopata madhara ni wanawake. Kwa Azimio hili kwa nchi ambazo hazisikii ziwekewe vikwazo, kama zipo ndani ya *SADC*, kwa kufanya hivyo itasaidia wengine kutofanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii isaidiane na *NGO's* kutoa elimu ya uchaguzi kwa wanawake hapa nchini na haki ya kupiga kura ili wachague viongozi wanaofaa. Pia wasiuze haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake waelimishwe kuhusu utoaji na upokeaji rushwa kwenye haki zao, hivyo, Wizara itenge fedha kwa mwaka huu kwa ajili ya kutoa elimu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Azimio hili.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza kabisa, ninachukua nafasi hii kuipongeza Wizara na Serikali kwa kuipeleka makala hii ya Itifaki mbele ya Meza ili iridhiwe Bungeni. Itifaki hii ni nzuri sana kwa nchi yetu, kwani hapa duniani binadamu ameumbwa bwana na bibi makusudi kabisa. Makusudi yake ni kusaidiana mambo kadhaa. Bwana peke yake hawezi kuleta maendeleo na mke peke yake hawezi kuleta maendeleo, kwa hiyo, mke na mume wanahitajika kuendeleza nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi, ninaishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuridhia Mikataba mbalimbali inayohusu Haki za Wanawake na Masuala mazima ya kuondoa unyanyasaji wa kijinsia, kutokana na hilo, wanawake wa Tanzania tumeweza kufika mbali katika elimu, siasa, utamaduni, kijamii na kiuchumi kwani kuna nchi zingine hapa duniani wanawake hawaruhusiwi kupiga kura, wala kufanya shughuli za kiuchumi wala kugombea uongozi wowote ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni kwamba nchi zote Afrika na duniani, waache unyanyasaji wa kijinsia na wawe radhi kuridhia Mikataba ya Kuondoa Unyanyasaji wa Wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Vyama vyote vya Kisiasa viweke mazingira mazuri ya kumwendeleza mwanamke ili aweze kupata maendeleo, kwani wanawake wote wana mahitaji sawa na itikadi isiwe chombo cha kumdhalilisha mwanamke katika maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusaidia wanawake kiuchumi tuyaangalie maeneo ya wanawake hao kimpangilio ufuatato; Wanawake Vijana, Wanawake Wazee, Wanawake waishio mjini, Wanawake Waishio Vijijini, Wanawake walioolewa, Wanawake wasioolewa, Wanawake wafanyakazi, Wanawake Wakulima, Wanawake Wafugaji na Wanawake Wavuvi. Ni muhimu sana kuwaangalia wanawake katika makundi hayo, vingivevyo utakuta baadhi hawafaidiki chochote katika maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake katika siasa/ngazi za maamuzi. Tungeomba suala la 50/50 katika ngazi za maamuzi lizingatiwe, kwa mfano, Madiwani, Ajira Serikalini na Ubunge ngazi za Kata/Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Benki ya Wanawake litiliwe mkazo pia kwa kuisambaza angalau Mikoani ikikaa Dar es Salaam peke yake, wanawake wengine hawatapata pesa za mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo chombo cha Umoja wa Wanawake wote bila kujali kabila, dini au itikadi ya kisiasa; ili umoja huo uweze kuwainua wanawake wote kwani wanawake wote wanahitaji kula, kuvaa, kulala, kuishi huru, kutafuta mahitaji mbalimbali, wanawake wote wana mahitaji sawa ila matatizo yetu sisi ni nyenzo za kufanyia kazi ili kujiendeleza. Nyenzo hizi ziwafikie wanawake wa aina zote nilizozitaja hapo juu. Umoja huo ndio utakaosaidia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono 100/100.

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kuchangia kuhusu hoja hii iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa, ninapenda kumshukuru Waziri na jopo lake pamoja na Kamati iliyoweza kukubali na kupitisha hoja hiyo, ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna ubakaji ambao bado unaendelea kwa kuwabaka watoto na wanawake, bado hawatendewi haki wanapokwenda Mahakamani kushitaki. Haki hiyo hawapewi na mwisho wake wanaume wanazidisha vitendo hivyo vya ubakaji. Hata kama ni mume na mke, mume humlazimisha mwanamke kitendo cha ndoa kwa kumfanya kama mbuzi, je, hawa tuwaweke kipengele gani, tunaomba wanaume hao waweze kuchuliwa hatua kali iwapo itatokea ili mwanamke awe na ndoa ya kihalali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wajane na wagane wanapata matatizo, ndugu wa marehemu hawawapi haki yao ya urithi hivyo wawe na haki ya kumiliki mali zote baada ya kufiwa na Mahakama iweze kuwasaidia siyo kulalia upande mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Margaret Sitta na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, bila ya kumsahau Katibu wa Wizara, Dada yetu Mariam Mwaffisi, kwa kuleta Mkataba huu wa *SADC* ili uridhiwe na Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Itifaki hii iweze kutumika ipasavyo ni vema itafasiriwe kwa lugha ya Kiswahili na itawanywe katika ngazi zote mpaka ngazi ya Kata. Mkataba huu ni taswira halisi ya mambo mengi yanayozunguka jamii zetu na hasa wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema pia nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali yetu ya Tanzania, hususani Rais wetu Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete pamoja na viongozi wote walioendeleza harakati za kumkomboa mwanamke na kuondoa ukandamizaji wa kijinsia. Ni vema Itifaki hii ichunguzwe kifungu kwa kifungu ili kutambua ni vifungu vipi ambavyo vimeshazingatiwa katika Sera zetu pamoja na Sheria zilizopo ili msukumo zaidi ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba tayari sera nyingi zinatambua jinsia kama tatizo mtambuka mfano *SME Policy 2003, Rural Development Policy 2002, Population etc.* Hali kadhalika Sheria zetu hasa zinazopitishwa siku hizi zinaanza kulenga na mambo ya jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo, kuna upungufu katika baadhi ya maeneo, mfano, ili kufikia 50/50, ni vema namna bora kuwapata Wabunge wa Viti Maalum ndani ya Vyama vya Siasa iwepo, utaratibu uwe wazi na ikibidi ufanane kwa vyama vyote ili kuondoa wanawake kunyanyaswa na baadhi ya Vyama. Isitoshe Vyama vyote vieleze jinsi ya kufikia *gender parity* ndani ya Vyama vyao ama sivyo vifutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu uliopo katika Katiba wa namna ya kuongeza wanawake inabidi uangaliwe zaidi namna ya kuwaongeza kwenye Majimbo, kuwe na kifungu kinachoweza kwani *formula* ya sasa inakabiliwa na ukomo wa viti Bungeni na hivi viti maalum si rahisi kuwe na zaidi ya asilimia 50 ya Wabunge. Kwa misingi hiyo, 50/50 ni ngumu kufikiwa kama Wabunge wa Majimbo watakuwa na idadi ndogo

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *gender violence* mfano kukeketa wanawake ni unyama, ukomeshwe na ukatili wa kubakwa – siku hizi *case* hizi ni nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Walemavu italetwa lini? Haki za watoto, Sheria imepitishwa mkutano uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 20(2)(a), tumefanya vema kukiacha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 33, budget i.e shule (mabweni kwa mabinti, maji, vyoo) vizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 29, *media, equal representation*, wahamasishwe wamiliki wa vyombo hivyo na Waandishi wa Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 30, picha za matusi, wanawake kutumiwa vibaya, walemavu barabarani, hivi Serikali imeridhika na ile kazi ya Walemavu kuomba mpaka usiku?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wasaidiwe rasilimali za kumwezesha kwenye uchaguzi mfano pesa kidogo nk.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 31, *access to information*, mfano humu Bungeni tunapoendesha shughuli zetu hakuna mkalimani wa shughuli zetu kumsaida kiziwi na kipofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono kuridhia Itifaki ya Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii ni muhimu sana hususani katika nchi za Kusini mwa Afrika na Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Article 2.1(a), nchi lazima zirekebishe Sheria zao, Sera, Mikakati na *programmes* ili zilingane na *International Instruments* zinazohusiana na kumwezesha mwanamke kwa lengo la kuleta usawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokubali kuridhia Mkataba huu lakini una *implications*. Utatuweka katika wajibu. Article 2.1 (b) nchi zitapaswa kuamaua masuala yote yanayohusu utekelezaji wa Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunazo Sheria nyingi sana ambazo hazitoi haki sawa kwa wanawake na watoto mfano Sheria ya Matunzo kwa Mtoto "*Affiliation Act*" viwango bado ni vidogo kwa Itifaki hii itahitajika irekebishwe. Sasa hivi kuna watoto wengi ambao hawana baba au baba amekataa kuwa mtoto huyu ni wake n.k. Aidha, ili kuwepo na usawa katika sekta mbalimbali ni lazima tuwe na sera za usawa (ushirikishwaji) kati ya wanawake na wanaume. Hivyo vyombo vya maamuzi ni lazima kuwepo na wanawake na wanaume kwa usawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Article 12 (Uwakilishi), nchi lazima zihakikishe kuwa ifikapo mwaka 2015 angalau katika vyombo vya maamuzi kuwepo na asilimia 50/50 hii ni pamoja na Vijiji – Udiwani – Ubunge. Nchi zinapaswa kuweka mikakati mbalimbali katika utekelezaji wa azma hiyo. Ninaomba basi mikakati hiyo iwe ni pamoja na kuwapa elimu wanawake. *Loans Board* pamoja na kigezo cha *quantity* kiwepo kigezo cha *quality*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Article 16, ipo hoja ya kuwa na sera nchini inayosema kuwa ni lazima mabenki watoe mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kila kipengele cha Itifaki hii kiwe *domesticated, every Article* ili itifaki hii iweze kuleta maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Article 26, inasema kupunguza vifo vya akina mama kwa asilimia 75 ifikapo 2015, Article 35, *Implementation/Monitoring and Evaluation*. Itifaki hii inahitaji kuweka mikakati thabiti ya kutunga Sheria na kufanya marekebisho ya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na azma hii, sisi wataalamu wa *International Laws* tumegundua kuwa bado kuna upungufu katika utekelezaji kwani nchi nyingi sana huridhia na baada ya hapo mikakati ambayo inapaswa kutekelezwa haitekelezeki. Aidha, bado *International Law* haijatoa jibu kamili kwa nchi ambazo zimeridhia na hazitekelezi maridhiano na Mahakama za ndani wakati mwingine huwa hazinukuu Itifaki katika sheria husika kwa mfano *The Vienna Convention on the Law of Treaties*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuleta Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) ya mwaka 2008. Naunga mkono Azimio la Kuridhia Itifaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wengi hasa wa vijijini hawana elimu ya Sheria za msingi na pia hawana ufahamu wa haki zao za msingi hivyo elimu iendelee kutolewa. Serikali ishirikiane na taasisi mbalimbali ili kuwafikia wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wasiozwe katika umri mdogo kwa kisingizio chochote kile kama wana umri wa chini ya miaka 18. Kwani hii itatoa mwanya kwa jamii kuoza watoto wa chini ya miaka 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 10 inahusu haki za wajane na wagane. Ni muhimu Serikali ikaweka mpango maalum wa ngazi mbalimbali hasa Halmashauri kuhakikisha kwamba haki zote za wajane na wagane zinalindwa. Pia wapate mikopo ili kuweza kuhudumia familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 11 inazungumzia ulinzi na usalama na ulinzi wa watoto wote wa kike na kiume. Kwa vile Tanzania tumeshatunga Sheria ya Mtoto na *Anti-trafficking in Persons Act Na.6 of 2008*. Ni muhimu sheria hizi zote zikatafsiriwa kwa Kiswahili na kanuni zake, sheria hizi zifanyiwe kazi. Watoto wengi wanakosa haki zao za msingi na wananyanyasika. Serikali iangalie uimarishaji wa Mabaraza ya Watoto ngazi zote ili wapate fursa ya kutoa maoni yao na kushirikishwa katika kutoa maamuzi ya masuala mbalimbali yanayowahusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wanaopata ujauzito waruhusiwe kuendelea na elimu kama wavulana waliowapa mimba wanavyoendelea na masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa vituo vya kulelea watoto wadogo upewe umuhimu. Serikali iweke utaratibu unaoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wapewe kipaumbele katika kupata mikopo yenye riba nafuu na elimu ya zana za kilimo ili kuachana na kilimo cha jembe la mkono. Wanawake binafsi na pia kupitia vikundi vyao wapewe mafunzo ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake waelimishwe kuhusu Sheria ya Umiliki wa Ardhi ili waweze kuwa watumiaji halali kwani wanawake wengi hawana elimu kuhusu umiliki wa ardhi hivyo mume anapofariki wanawake wananyang'anywa ardhi ambayo alikuwa analima siku zote, anakosa haki ya kuwa mmiliki halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 22 & 23 inazungumzia wanawake waliobakwa kupewa dawa za Ukimwi, ni muhimu sasa Serikali kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali ianzishe vituo vya kusaidia wanawake wanaonyanyasika kijinsia na kubakwa kuweza kupata matibabu na pia kupata msaada wa kisheria wa kuweza kupata haki yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Itifaki hii.

MHE. MWINCHOUM A. MSOMI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza Viongozi/Wakuu wote wa nchi zilizo chini ya *SADC* kwa Kuridhia Itifaki hii akiwemo Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vile vile nampongeza Mheshimiwa Margaret Sitta, Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto bila kumsahau Naibu Waziri wa Wizara Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Katibu Mkuu Ndg. Mariam Mwaffisi, kwa juhudi zao zilizowezesha Itifaki hii kuingia Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo Serikali haina budi kulipa uzito unaostahili, ni kuipa fungu (Bajeti) ya kutosha Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Bajeti yake ya sasa ni ndogo sana na kwa kweli haikidhi mahitaji ya kuwawezesha kufanya kazi au kutekeleza majukumu yao kwa kiwango kizuri sana. Naomba Serikali ilione hili kwa umuhimu wake hasa katika kuelekea kwenye mgawanyo wa madaraka na wanaume (50-50).

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama na maisha ya amani kwa mwanamke nayo ni muhimu sana hivyo Wizara ishajiishe/ihimize Taasisi zinazoshughulikia masuala ya wanawake kuweka mipango ya kuwaelimisha wanawake juu ya umuhimu wa kushiriki katika harakati za kujiandikisha kupiga kura ili wapate fursa ya kuchagua viongozi watakaoweza kuendeleza amani na usalama wa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wanawake kuelewa haki zao, ni muhimu, ni vyema Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto itafute njia ya kuwasaidia wanawake kuelewa haki zao na kuwatetea katika vyombo vya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii haina budi kukaa pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kuhimiza kuwekwa mkakati wa kuanzishwa kwa kila kata huduma za uzazi hivyo zifanywe/zichukuliwe juhudi za makusudi za kusomesha Wakunga wengi kwa lengo la kutekelezwa azma hiyo. Imewezekana kwenye Ualimu ninaamini tukiamua vilevile tunaweza kwenye sekta ya afya, tuamue kupunguza vifo vya wazazi na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FLORENCE E. KYENDESAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Nane ya Itifaki hii inayozungumzia kuwepo sheria ya kuruhusu kwa kibali maalum na kwa maridhiano huru ya mwanamke na mwanaume kuoana chini ya miaka 18 na ndoa hiyo inaweza kuwa ya Kiserikali, Kimila au Kidini, napendekeza kuwa pamoja na kuwepo kwa maridhiano hayo iwekwe sheria kali kwa wazazi wa pande zote mbili, za mzazi wa kike/kiume itakapobainika kuwaoza watoto hao kwa makusudi ili kujipatia mali au kumkatisha elimu mtoto wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 11, ulinzi na usalama wa watoto wa kike na wa kiume, ili watoto wetu waweze kulindwa na kupata haki zao, ni vema iwekwe adhabu kali kwa wote watakaobainika kuwaajiri watoto chini ya umri wa miaka 18.

Aidha, ufanywe utafiti kuhusu watoto wadogo wa kike na wa kiume wanaombaomba barabarani kwa kuwatambua wazazi/walezi wao, kutolewa adhabu kali kwa watakaobainika wana hali nzuri ila kwa makusudi huwatumia watoto hao kwenda kuomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 12 na 13 inayozungumzia uwakilishi na ushiriki wa wanawake katika vyombo vya maamuzi, kwa kuwa unapofika wakati wa chaguzi mbalimbali, baadhi ya wanaume na wanawake hutoa maneno ya vitisho/matusi kwa baadhi ya wanawake wanaogombea, ni vema kuwepo na sheria itakayowabana watakaobainika kufanya vitenda hivyo, kwani wapo wanawake wanaogopa kwenda kwenye majukwaa kwa hofu ya vitisho vya aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, Napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Margaret Sitta (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara hii, Watendaji wote walioshiriki kuandaa Azimio hili, Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati, kweli wamefanya kazi kubwa ya kuchambua Azimio hili ili haki iweze kutendeka kwa jinsia zote mbili yaani wanawake na wanaume. Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukiri kuwa Azimio hili la mwaka 2008 limeletwa muda muafaka sana, kwani sasa litaenda sambamba na utaratibu wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete wa kutambua uwezo wa wanawake na kuwateua kwenye nafasi mbalimbali za uongozi mfano Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi, Majaji nk. Mungu awape afya Rais wetu na maisha marefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia nafasi hii kuipongeza Serikali kuridhia utaratibu wa hamsini kwa hamsini kwa wanawake na wanaume kuwa Wabunge na Madiwani lakini azma hii itatekelezeka tu endapo wanawake wengi tutajitokeza kugombea Majimbo. Pia wanawake watahinda tu endapo tutapendana, tutaungana mkono na tutawezeshwa. Ninaomba Serikali na vyombo mbalimbali mfano TAMWA n.k. viwaunge mkono na kutoa elimu kwa wanawake. Vile vile itasaidia sana ikiwa Vyama vya Siasa vitawasaidia wanawake kwa kuwateua wengi kugombea. Nashauri viongozi na watendaji kuteua wanawake kuwa Wakuu wa Idara, Watendaji Watumishi na Wajumbe wa Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kuwa wanawake wanafanya kazi masaa mengi sana katika familia kuliko wanaume, lakini unakuta wakati unapofika ndoa kuvunjika mwanamke hapati haki ya mgao wa mali ambazo mchango wake ni mkubwa.

Sio kuachana tu hata wajane kudhalilika. Ninaimani kupitia Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jinsia itasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna tabia ya akina baba kulazimisha mwanamke kufanya mabao mengine hata kama amechoka, anaumwa na hata kupigwa ovyo na hata akienda Polisi, Mahakamani anakosa haki kwa unyonge au kukosa uwezo wa pesa hata kuzalishwa watoto wengi hata kama uwezo wa kulea au nguvu ya kubeba mimba imepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema sasa kuwapa elimu wasichana wengi ili kuwaandaa kushika nafasi mbalimbali za uongozi ili wasichana wengi waweze kusoma na kuwalegezea masharti mfano maksi za wasichana ziwe tofauti na wavulana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili wanawake waweze kushinda kwenye nafasi za Udiwani na Ubunge, ni vema jamii ifike mahali kusahau mila au imani potofu mfano mwanamke hawezi kuwaongoza wanaume, wanawake wao kwa wao kutopendana na wanawake kutokujiamini.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa kuna elimu nyingi mfano elimu ya kuzaliwa nayo, elimu ya kusoma, elimu dunia, elimu ya kuiga n.k. Hivyo, wapo wanawake au wanaume ambao wanaweza kushika madaraka hata kama ana elimu ndogo. Naomba akumbukwe Mwanafalisafa, Sokretes wa Ugiriki hadi leo falsafa yake inafundishwa Vyuho Vikuu vyote duniani na hata nchini wapo viongozi walioongoza nchi hii kwa nafasi mbalimbali kwa elimu za kawaida walizosoma lakini walioongoza vizuri sana mfano Mzee Songambe alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumaliza mchango wangu wa maandishi kwa kuunga mkono Azimio hili nikiwa na imani kuwa itifaki hii itatekelezwa vema.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wa Wizara ya Jinsia na Watoto, kwa kuleta Azimio hili hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 7, haki za mwanamke za kisheria. Wanawake wengi hapa nchini wamekuwa wanakosa/wananyimwa haki zao za msingi kutokana na kutojua sheria zinazotetea haki zao na pia kukosa uwezo kifedha wa kufuatilia haki zao. Mwanamake inapokuja suala la kumiliki mali au mirathi au kupata mikopo, ni matatizo atazungushwa, atasumbuliwa hata kukata tamaa. Napongeza juhudi za *NGO's* zinazofanya kazi kubwa kutoa misaada ya kisheria kwa akina mama wanaoteseka mfano *TAWLA, TAMWA* nk. Pia napongeza sana vyombo vya habari kwa kuibua matatizo/manyanyaso wanayofanyiwa akina mama maeneo mbalimbali na kuyaweka wazi na hivyo kufanyiwa kazi. Hivyo, nchi yetu kutunga sheria na kuweka taratibu zitakzohakikisha usawa kwa wanawake, ni muhimu san ili kuwapatia haki wanawake wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 10, kuhusu haki za wajane na wagane, wanawake wengi wananyanyasika sana pale mwenzie/mumewe anapofariki. Wakiwa hai mali wanachuma pamoja kwa shida na kwa raha lakini pale anapoondoka mwanamke anaonekana hana haki na zile mali. Hili linasikitisha wana. Ipo mifano mingi na kesi nyingi Mahakamani za aina hii. Yapo makabila yanadai ni mila zao hizo zimepitwa na wakati. Umiliki wa mali zilizochumwa pamoja anapoondoka mmoja anabaki nazo mjane kwa ajili ya watoto. Sheria ya Ndoa itakapoletwa Bungeni iainishe vizuri haki za mjane ili kuondoa manyanyaso kwa wajane.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 12, uwakilishi wa wanawake kwenye nafasi mbalimbali za maamuzi. Wanawake wakipewa nafasi wanaweza tena sana. Suala la kuwashirikisha wanawake katika ngazi mbalimbali ni muhimu sana. Hili limedhihirika kwa wale wachache wanapotoa nafasi hizo. Lazima kuwepo mkakati maalum wa kuhakikisha (50%) usawa kwenye nafasi za maamuzi. Serikali itoe maagizo kwenye sekta binafsi kuhakikisha wanatoa haki sawa kwa wanawake. Kwa uzoefu wetu, wanawake Tanzania walisahaulika na pia zipo mila zinazokandamiza mwanamke – mwanamke hawezi kuongoza mwanaume. Hivyo elimu itolewe kwa wananchi wote wanawake kwa wanaume watambue nafasi ya mwanamke na hivyo kuwaunga mkono na kuwachagua pale wanaposimama kugombea nafasi mbalimbali za kisiasa, uongozi nk.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 20(2)(a), utoaji mimba (kwa dharura). Suala la utoaji mimba nalipinga kabisa ni kinyume na imani yetu, mila zetu na hata sheria zetu za nchi. Hivyo Serikali iendeele kuimarisha sheria zetu za ndani ambazo zinakidhi matakwa ya Watanzania. Hakuna mimba ya bahati mbaya ikishatungwa, ni haki itunzwe ikue na mtoto azaliwe na wale wawili walioshiriki kutunga hiyo mimba washiriki kuitunza. Pale inapolazimu kwa sababu maalum za kiafya tuwaachie Madaktari/wataalam waone jinsi ya kuokoa mama/mtoto.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaunga mkono hoja 100%. Kipekee ninaomba kutoa pongezi zangu za dhiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri arejee Ibara ya 12 na 13 zinazozungumzia uwakilishi na ushiriki wa wanawake katika vyombo vya maamuzi. Hapa Tanzania, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 – 2010, kifungu 120(a) kinasema:-

“kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi wa kisiasa, kiutendaji na nafasi za maamuzi kwa lengo la kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2010 kama ilivyokwishaazimiwa na Umoja wa Afrika.”

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne zimeteuliwa bodi nyingi sana za mashirika na baadhi za taasisi lakini hakuna hata moja ambayo ina jinsia 50/50. Endapo katika uteuzi unaofanywa na Mheshimiwa Rais na Mawaziri inakuwa ngumu hivyo kutekeleza, je, ni nani atakayesimamia au atakayetokeleza haya? Kwa mfano, Bodi ya Tumbaku, Bodi ya Mweka Wildlife, Bodi ya AICC, Bodi ya TPDC, Bodi ya NSFF etc. Je, Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, yuko tayari

kutuhakikishia kuwa atasimamia na atawasiliana na Mawaziri wenzie kuhakikisha kuwa kuanzia leo, kila uteuzi wa bodi utakofanyika itakuwa 50/50? Ninaomba majibu wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, rejea Ibara ya 15 na 17. Ibara hizi mbili zinazungumzia mwanamke na uchumi. Kwa kuwa ni takribani miaka 49 sasa tangu tupate uhuru na nafasi ya mwanamke imebaki kuwa duni. Zingatia *Pro-poor Budget*. Kila Wizara inapopanga *budget* itenge *budget* ya mwanamke/jinsia na watoto kwani Wizara kama Wizara ya Jinsia na Watoto imekuwa ikipata *budget* ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napongeza kwa kuletwa Itifaki hii ya jinsia katika Bunge hili. Ni ukweli usiopingika kuwa Itifaki hii itazifuta sababu nyingi zinazotolewa ili kumwagamiza huyu mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Itifaki hii. Baada ya hoja mbalimbali kutolewa pande zote mbili kisiasa, naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri kwa vikundi vyenye uwezo wa kuwawezesha watoto/vijana/wanawake wenyewe ili waweze kuzijua haki zao na si kupitia makundi mengine. Ni mazoea ya nchi yetu kutoa elimu katika vikundi mbalimbali ambavyo havihusiki au vikundi hivi tayari wameelimishwa na uelewa wanao tayari. Hivyo, nashauri uwezeshwaji huu usitishwe kwa ngazi hasa za juu na elimu hii ya unyanyaswaji wa kijinsia wapewe hasa ngazi za chini wakihusishwa hasa watoto, vijana na wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vijana na hasa wa kike hudhalilishwa sana na vyombo vya habari aidha kwa mavazi au hata mambo ya ngono. Natoa ushauri kuwa mara matukio hayo yanapotokea vyombo hivyo vifungiwe mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mara mzazi mmoja atakapofariki, aendelee kuwa mlezi au msimamizi wa mirathi. Pia ziwekwe taratibu za msimamizi huyo kutoa taarifa Serikalini kila baada ya mwaka mmoja hadi muda kukamilika.

MHE. MCH. LUCKSON MWANJALE: Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kutoa maelezo yangu, naomba nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pia pongezi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote katika Wizara husika kwa kulileta Azimio hili ili Bunge liweze Kuridhia Itifaki ya Jinsia na Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili limeletwa kwa wakati mwafaka hasa wakati huu ambapo nchi nyingi hasa nchi zile zinazoendelea zikiwa katika Maazimio mbalimbali yahusuyo haki za mwanamake na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili ambalo Bunge linaridhia lisiishe tu katika nafasi ya uongozi na ngazi za juu lakini mikakati mbalimbali ibuniwe ili kero hizi za ubaguzi wa jinsia zitokomezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zinazotungwa kutoa adhabu kwa wanaovunja au wanofanya ubaguzi, hazitoshi isipokuwa sheria hizo ziende sambamba na utoaji wa elimu ihusuyo haki za wanawake na watoto. Elimu hii ianze kutolewa kuanzia huko vijijini ambako jamii kubwa ya watu bado mila na desturi zinawagandamiza. Mila na desturi zinafuatwa kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo Azimio hili linagusa ni kufikia asilimia 50% ya uwakilishi katika vyombo vya maamuzi. Bado natoa ushauri wangu kuwa uwakilishi huo uanzie huko katika ngazi mbalimbali vijijini hadi katika ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kuunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge ambao mlikuwa mmejitokeza vizuri sana kuchangia Itifaki hii mtakosa nafasi lakini kama ni suala la uwakilishi sawa kijinsia katika nchi kuna Muswada ule wa Marekebisho (*Miscellaneous Amendment*) suala hili litajitokeza tena. Kwa hiyo, nyie mliokosa nawaalika tena mjiandae kwa Muswada ule mwingine, kwa sasa nitaomba nimwite mtoa hoja aweza kutoa ufafanuzi wa michango ya Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa mtoa hoja. Wale waliochangia kwa maandishi yataingia kwenye *Hansard*, pengine Waziri atashindwa kujibu kwa sababu, hawezi kusoma kwa dakika hizi mbili tu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuhitimisha hoja ambayo tumeanza kuijadili kuanzia jana. Awali ya yote, natoa shukrani nyingi kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia, kwa michango yao mingi ambayo itawezesha utekelezaji wa Itifaki hii ikiridhiwa leo kuwa ya manufaa kwa Taifa letu hasa katika kuzingatia usawa wa kujinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza unipe ruhusa ya kuwataja waliochangia kwa kuongea na pia kwa maandishi. Kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge waliotoa hoja zao kwa kuongea ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii; Mheshimiwa Anna Maulidah Komu kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Jaji Fredrick Mwita Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Joseph Mungai, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu na Mheshimiwa Anna Lupembe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa njia ya maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Mgeni J. Kadika, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Khadija Salum, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Mch. Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanywa, Mheshimiwa Zaynab Vulu na Mheshimiwa Ruth Msafiri. Iwapo itatokea kwamba nimemruka Mheshimiwa Mbunge yeyote niko tayari kumsoma baadaye nikiarifiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoanza, nilitoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia kwa njia zote mbili kwa maandishi na kwa njia ya kuongea. Michango yao itakuwa ya manufaa sana hasa katika utekelezaji wa itifaki hii. Naomba kwanza nitoe maelezo ya ujumla kwamba, Bunge hili likiridhia Itifaki hii litakuwa limetoa fursa kwa Serikali kuandaa mkakati wa utekelezaji. Mkakati wa utekelezaji ndiyo utakaoainisha majukumu na wahusika katika utekelezaji. Kwa hiyo, mkakati wa utekelezaji utainisha majukumu ya Serikali na wadau mbalimbali zikiwemo *NGO's* na wengine wote ambao tunashirikiana katika kuleta maendeleo nchini. Kwa hiyo, ni muhimu sana Itifaki hii kuridhiwa ili hatimaye uwepo mkakati wa utekelezaji wake katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kwa ufupi, naomba sasa niwataje Wabunge na hoja walizozichangia. Nawaomba radhi Waheshimiwa Wabunge ambao huenda wamechangia lakini hawatasikia majina yao, lakini naamini yote waliyozungumza tumeyachukua na yatatiliwa maanani katika uandaaji wa mkakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, msemaji wa kwanza, kama nilivyosema, alikuwa ni Mheshimiwa Jenista Muhagama ambaye alizungumza na aliunga mkono hoja kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii ya Bunge letu na ushauri wao na maoni kwa ujumla yalikuwa kama ifuatavyo; yalihusu Katiba na nafasi ya wanawake katika ngazi za maamuzi, Serikali kutoa tamko kuhusu watoto wanaopata mimba kurudi shuleni, kuhusu usajili wa ndoa za kimila na kidini kwa mujibu wa sheria za nchi, kuifanya elimu ya sekondari kuwa ya lazima kwa wote, suala la usafiri kwa watoto wa kike na mabweni, sheria za kuwalinda walemavu na kupata haki zao na upatikanaji wa dawa za tahadhari mara baada ya tendo la ubakaji kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa ushauri na maoni yao ya msingi waliyoyotoa kuhusu Itifaki hii. Serikali imekuwa

ikifanya jitihada mbalimbali za kuleta usawa wa jinsia kwenye maeneo mbalimbali yakiwemo ya uchumi, ajira, elimu, afya na sheria. Kwa hiyo, Itifaki itatoa changamoto kwa Serikali kuweka nia na juhudi zaidi. Lakini kimsingi, yote haya ambayo yametajwa, Serikali kwa njia moja au nyingine imekuwa ikiyashughulikia. Kwa kuwa Itifaki hii itatekelezwa na wadau mbalimbali kwa kuzingatia Sera, Katiba, Sheria na Taratibu za nchi, maoni yote yatafanyiwa kazi katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambao uliwasilishwa hapa na Mheshimiwa Maulidah, yalihusu nchi za wanachama wa SADC ni vyema zikaingiza vifungu katika Katiba za nchi zao ili kuondoa kero za jinsia kama uzingatiaji wa masuala ya usawa wa jinsia wakati wa utungaji wa sheria na kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kuishukuru Kambi ya Upinzani kwa maoni yao na ushauri. Kuingiza suala la jinsia katika Katiba ya nchi Wanachama wa SADC ni muhimu. Itifaki ndivyo inavyoelekeza. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 13(1) hadi (6)(a), kinakataa aina zote za ubaguzi na unyanyasaji wa kijinsia na kuhimiza usawa mbele ya sheria. Hii ni pamoja na kuwepo kwa sheria zinazojali na kulinda usawa wa kijinsia kama vile Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 kama ilivyorekebisha mwaka 2002. Naamini Serikali itaendelea kurekebisha sheria zisizozingatia usawa wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia ilihoji kwa nini nchi nyingine zinachelewa kuridhia Itifaki hii. Kuridhiwa kwa Itifaki hii na nchi wanachama, ni kwa maridhiano na si vinginevyo. Kwa hiyo, naamini iko siku na wao wataridhia kama tunavyofanya sisi siku ya leo.

Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mbunge Viti Maalum, alizungumzia Muswada wa Haki na Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu uletwe Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na hoja hii pia imezungumziwa na Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Anna Lupembe. Muswada wa Haki na Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu utaletwa Bungeni, Serikali ilishaandaa kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa hiyo tuvute subira tu, yote hayo yatazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge tulijadili kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa Kuhusu Haki za Watu wenye Ulemavu na Mkataba wa nyongeza wa Kimataifa kuhusu Haki za Watu wenye Ulemavu uliwasilishwa na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na kuridhiwa na Bunge. Ni imani yangu kwamba maoni ya Mheshimiwa Mbunge hasa Margreth Mkanga kama alivyotoa hoja, yatatekelezwa.

Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya na Mheshimiwa Mgeni Kadika, walizungumzia kuhusu ulemavu unaotokana na uzazi (*fistula*). Wameshauri walemavu wa aina nyingine wapewe haki zao za msingi pamoja na vifaa vya kutumia. Ushauri wa

Waheshimiwa Wabunge kuhusu utekelezaji wa hayo, utategemea mkakati wa utekelezaji utakaoandaliwa na kutekelezwa na sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu haki za Wajane na Wagane, hili limezungumziwa na Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Anna Lupembe. Tunakubaliana na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, aidha, sheria husika iko kwenye mchakato na inashughulikiwa na sekta husika ya Wizara ya Sheria na Katiba. Ntoa wito kwa jamii ya Watanzania kuwa na utaratibu wa kuandaa wosia, tuisubiri marekebisha ya sheria. Sisi kama wanajamii tuweke utaratibu wa kuandaa wosia na kufungua mirathi ili hatimaye matatizo yanayotupata ya kifo basi tuwe tumelekeza jinsi ambavyo warithi wetu watanufaika nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie hoja inayotaka Serikali itoe tamko rasmi la kuwarudisha shule watoto wa kike wanapojifungua ambao wamekatishwa masomo yao, ili kutoa usawa kwa watoto wa kike katika suala la elimu. Hili limezungumziwa na Mheshimiwa Owenya, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Joseph Mungai, Mheshimiwa Ledian Mgo'ong'o, Mheshimiwa Florence Kyendesya na Mheshimiwa Stella Manyanya. Sisi kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, tumeupokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na naamini Serikali inalifanyia kazi kwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tunakubaliana na ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Joseph Mungai wa umri wa kuanza shule uangaliwe upya ili kupunguza changamoto zinazotokana na suala la mimba, utoro na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uwakilishi wa akina mama kufikia *fifty-fifty* Bungeni na pia katika Serikali za Mitaa, limezungumziwa na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Bernadeta Mushashu. Tunawapongeza Wabunge ambao wameunga mkono jitihada za Serikali za kufikia asilimia hamsini kwa hamsini, lakini napenda kutumia nafasi hii, kutoa wito kupitia Bunge lako Tukufu kuwa usawa wa kijinsia na hata huu tunaozungumzia wa asilimia hamsini kwa hamsini, unatokana na utashi wa kisiasa. Ntoa wito kwa Vyama vya Siasa kufanya jitihada za makusudi katika kuongeza nafasi za wanawake katika Vyama vyao na katika kipindi cha uchaguzi na hasa mwaka huu. Aidha, Serikali itaendelea na juhudi za kuelimisha jamii ili iweze kutambua umuhimu wa wanawake kuwa na nafasi ya maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuwatoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge hasa Mheshimiwa Bujiku Sakila na Waheshimiwa Wabunge wengine wenye hofu kwamba wanawake watazidi na mwisho watawapita hata wanaume. Lakini wanawake kwa sasa hivi, hiyo ndiyo hali waliyonayo na wanaangalia jinsi ya kujikwamua. Kwa hiyo, napenda kurudia wito ambao tumeutoa mara nyingi na kurudiwa

na Mheshimiwa Naibu Spika, Anna Makinda tulipokuwa kwenye semina Ubungo alisema “wanawake msioCOPE, wanaume msihofu”.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wawakilishi kufikia asilimia hamsini kwa hamsini, pia liliungwa mkono na Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mogella, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulijitokeza hoja ya uwezesaji wa wanawake kiuchumi kupitia Benki ya Wanawake na taratibu za benki nyingine kutoa mikopo kwa wanawake kwa masharti nafuu. Hili lilizungumziwa na Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Ledian Mng’o’ng’o, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Mgeni Kadika, Mheshimiwa Magdalena Sekaya, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi na Mheshimiwa Fatuma Mikidadi. Serikali inalifanyia kazi suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wanawake iliyoanzishwa mwaka jana tarehe 28 mwezi wa Saba, 2009, imeanza kutoa mikopo kwa wanawake kwa masharti nafuu. Changamoto iliyopo ni kuiwezesha benki hiyo kuwa na matawi nchi nzima. Kwa hiyo, napenda kutumia nafasi hii kwa kupitia Bunge lako Tukufu, kutoa wito kwa wanawake na wanaume, wote wenye uwezo mkubwa, wa kati na mdogo, kufungua akaunti pamoja na kununua hisa ili kuiwezesha Benki ya Wanawake kufungua matawi Mikoani. Tulitahadharishwa na mgeni rasmi, Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa kuifungua Benki hii, kwamba tuimarisha benki hii kwanza kabla hatujasambaza nguvu sehemu zingine. Kwa hiyo, wakinunua hisa Watanzania wanaume kwa wanawake, tutaweza kusambaa sehemu nyingine haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilihusu umuhimu wa elimu kwa umma kuhusu haki za wanawake. Hoja hii iliungwa mkono na Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mogella, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Joseph Mungai, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Maria Hewa. Tunashukuru sana kwa michango yao kuhusiana na suala la elimu kwa umma. Natoa wito sisi wote viongozi tulio katika nafasi mbalimbali, tutumie nafasi za mikutano, warsha, mikutano ya hadhara na semina kuhamasisha jamii nzima kuona umuhimu wa kuwa na usawa wa kijinsia katika jamii yetu. Hili pia liliungwa mkono na Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Ledian Mng’o’ng’o.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge pia walizungumzia hoja ya kuundwa Baraza la Kufuatilia Utelekezaji wa Masuala ya Kijinsia katika ngazi za Kitaifa na Kimataifa. Hili lilizungumziwa na Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mogella na Mheshimiwa Fatuma Mikidadi. Tunashukuru na kuupokea ushauri wao na ninaamini tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa inahusu ukatili dhidi ya wanawake na usalama wao katika jamii, kwamba wanawake wanapata matatizo makubwa sana ya ukatili dhidi yao pamoja na watoto wao. Hili lilizungumziwa na

Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mogella, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o na Mheshimiwa Diana Chilolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubaliana na maoni yao, Serikali itaendelea kupiga vita. Wakati huo huo tunatoa wito kwa jamii nzima kuhusu suala la ukatili dhidi ya wanawake na usalama wao ambalo linahitaji ushirikiano wa jamii nzima, wote wanawake kwa wanaume ili tukomeshe ukatili huu ambao unarudisha maendeleo ya wanawake na wananchi kwa ujumla. Natoa wito kwa jamii pia kutambua haki za wanawake pamoja na madhara ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya kutafsiri Itifaki ya Jinsia na Maendeleo kwa Kiswahili na kuisambaza katika ngazi zote. Tunaukubali ushauri huu na utazingatiwa katika utekelezaji wa Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilihusu sheria zirekebishwe ili kutoa haki kwa wanawake. Hili lilizungumzwa na Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Martha Mlata. Tunakubaliana na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na Serikali itaendelea na mchakato wa kurekebisha sheria mbalimbali zenye upungufu ili kuleta usawa wa kijinsia nchini mwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya ndoa za utotoni ilizungumzwa na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Fatuma Mikidadi na Mheshimiwa Mwanne Mchemba. Hii ni changamoto kwa Serikali na naamini Serikali itaendelea na mchakato wa marekebisha ya sheria ili kuhakikisha kwamba maslahi ya mtoto yanalindwa na hasa kwa sasa ambapo tayari tuna Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia na hoja ya bajeti za sekta mbalimbali zizingatie jinsia na hili lilizungumzwa na Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mogella, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi na Mheshimiwa Esther Nyawazwa. Tunakubaliana na ushauri wa Waheshimiwa ambao unafanyiwa kazi. Wakati wa matangazo mmesikia kwamba tayari Waheshimiwa Wabunge wameunda kikundi chao cha wakereketwa ambao leo hii tunakutana nao kwenye semina ya kuwapa uwezo zaidi ili wafuatilie uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika bajeti zinazoletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia na hoja ya kutothaminiwa kwa wanawake katika jamii ambayo imezungumziwa na Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Tunakubalina na Waheshimiwa Wabunge na Serikali imeanza kulifanyia kazi suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa na Mheshimiwa Maria Hewa inahusu udhalilishaji wa kijinsia kupitia vyombo vya habari. Tunakubalina na maoni ya Mheshimiwa Mbunge. Nina imani Wizara husika inalifanyia kazi suala hili ili kusiwe na udhalilishaji wa kijinsia kupitia vyombo vya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja nyingine iliyotolewa na Mheshimiwa Esther Nyawazwa iliyohusu Serikali kutoa tamko kuhusu taulo feki za wanawake ambalo pia limezungumzwa na Mheshimiwa Grace Kiwelu. Ni kweli si jambo zuri lakini nadhani Serikali imelisikia na inalifanyia kazi.

Mheshimiwa Anna Lupembe amezungumzia suala la watoto wa mitaani. Naamini Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 imelitilia maanani kwa kuweka vifungu mahsusi ambavyo vitahakikisha wazazi wanawajibika kwa sababu hawa watoto wa mitaani ni matokeo ya ndoa zinazovunjika na ni matokeo ya wazazi wasiowajibika. Kwa hiyo, kwa Sheria hii ya Watoto ambayo imepitishwa mwaka jana 2009, inatoa majukumu ya wazazi na adhabu watakapopewa wale ambao hawatawajibika. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba tukiwajibika katika familia zetu, watoto wa mitaani watapungua sana. Tukiheshimu ndoa zetu na tukizilinda, tukawajibika ipasavyo, suala la watoto wa mitaani litapungua kama sio kuisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa sio rahisi kuzungumzia hoja zote zilizotolewa ndani ya Bunge hili. Kwa hiyo, naomba nimalizie hoja ya mwisho kabisa ambayo ilizungumziwa na Mheshimiwa Anna Lupembe kuhusu elimu ya UKIMWI vijijini. Hili ni suala ambalo naamini limekuwa likifanyiwa kazi, kinachotakiwa sasa ni Serikali kuongeza nguvu zaidi. Lakini ni suala ambalo sisi wote ni mashahidi kwamba kuna vyombo vinavyohusika katika sekta husika ya kutangaza elimu ya kujikinga na UKIMWI mijini na vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuhitimisha kama ifuatavyo, kwanza kuwaomba Waheshimiwa Wabunge turidhie hii Itifaki kwa kuwa kipengele kilichokuwa kikitutia wasiwasi. Mwanasheria Mkuu ameshafafanua kwamba Serikali haitatekeleza na ametueleza kwamba inawezekana tukaridhia bila kutekeleza kifungu kinachoruhusu kutoa mimba. Kwa hiyo, ombi langu la kwanza Waheshimiwa Wabunge ni kuwaomba mridhie. Faida ya kuridhia nimeshaitaja na naomba nirudie, kwamba tukisharidhia, Serikali itaandaa mkakati wa utekelezaji ambao utaaanisha majukumu ya sekta mbalimbali katika masuala yote mliyontajia. Suala la watoto waliozaa wakiwa shuleni kurudishwa shuleni, linafanyiwa kazi. Masuala yote mliyozungumzia ya wajane, sekta husika zitashughulikia; kwa hiyo kitu kikubwa hapa ni turidhie hapa Bungeni na tuainishe majukumu, wapewe sekta husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo ninapenda kuliongelea hapa Bungeni katika kuhitimisha ni usawa wa kijinsia katika vyombo vya maamuzi. Sisi wote tunaamini na tunajua kwamba panapokuwa na usawa wa kijinsia, hutoa fursa kwa wote wanaume na wanawake kushiriki katika kuleta maendeleo nchini mwetu. Kwanza kwa kubuni mipango pamoja, pili katika kusimamia mipango yenyewe, tatu katika kugawa rasilimali na hata katika kumilikisha rasilimali, ili sisi wote wanaume na wanawake tuweze kufaidi matunda ya nchi hii na rasilimali za nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini utashi huu wa uwakilishi sawa kwa sawa au asilimia hamsini kwa hamsini lazima uanzie na Vyama vya Siasa. Kwa hiyo, natumia

nafasi hii kwa kupitia Bunge lako Tukufu, kutoa wito kwa Vyama vya Siasa tulivyonavyo nchini kwetu, kwanza kuangalia ndani ya Vyama vya Siasa jinsi gani wanazingatia usawa wa kijinsia, halafu pili wakati wa uchaguzi kuangalia akina mama wangapi wanasimamishwa ili waweze kugombea katika Majimbo. hili suala la Viti Maalum, tunashukuru, tunaomba Serikali iendelee navyo, lakini suala la Wawakilishi/Wabunge Wanawake katika Majimbo utategemea jinsi Vyama vya Siasa vitakavyoteua wanawake na kuwasaidia ili waweze kushinda katika Majimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatu, naomba pia kwa kupitia Bunge lako Tukufu, kutoa wito kwa wanawake kama alivyozungumzia Mheshimiwa Juma Killimbah, wanawake tupendane na tuungane mkono pale ambapo mwenzetu anaonekana ana uwezo na anagombea, tumuunge mkono, lakini pia tuwashawishi wanawake wenzetu ambao pengine hawako tayari kugombea, lakini sisi tunaamini wana uwezo, tuwashawishi wagombea ili na sisi tupate viongozi wanawake wengi zaidi. Kwa hiyo, wanawake tupendane na tuungane mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tuwaombe wanaume kutuunga mkono. Wanaume kwa sasa hivi ndiyo wanaoshikilia nafasi nyingi, ukienda kweye wajumbe wa mikutano mbalimbali wao ndiyo wengi, kwenye nafasi za uongozi za ngazi za juu, wao ndiyo wengi. Kwa hiyo, tuwaombe wanaume watuunge mkono, wakituunga mkono akina mama na sisi tutakuwa juu. Kwa hiyo, natoa wito kwa wale wanaoendesha semina za usawa wa kijinsia, za kuomba nafasi zaidi washirikishe na wajumbe wanaume, lakini ukiwaita wanawake watupu halafu unazungumzia umuhimu wa kupata nafasi nyingi zaidi haitoshi. Ni vizuri tuwashirikishe wanaume tunapozungumzia suala la usawa wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nawaomba wanawake kujitokeza, mwaka huu wa uchaguzi. Wanawake tujitokeze kugombea, tunaomba wanaume watuunge mkono ila na sisi wenyewe tujitokeze. Pia nitumie nafasi hii kuwaomba viongozi wote tuendelee kuhamasisha jamii huko tuliko kutokana na mila na desturi za nchi yetu, wanawake tunajua wanapewa nafasi ndogo, lakini tukiendelea kuelimishana, naamini akina baba, akina mama wote wataona umuhimu wa usawa wa kijinsia nchini mwetu. lakini pia tuanze na watoto majumbani mwetu, tuanze kuelimisha watoto wa kiume umuhimu wa kuwa na usawa wa kijinsia, shuleni na maeneo mengine ili watoto wakue wakijua umuhimu wa usawa wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na kwamba hoja zao tumezitia maanani na naamini zitazingatiwa wakati wa kuishughulikia Itifaki hii hasa katika kuweka mkakati wa utekelezaji, lakini pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge radhi wale ambao sikuwataja majina yao au sikutaja michango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Ndiyo Mheshimiwa Zainab!

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 64(7), jana baada ya kubishana sana na kutafuta ufafanuzi kuhusu kipengele kile cha kutoa mimba, aliyekuwa anaongoza Bunge alisema ataambiwa atakayeongoza Bunge leo kwamba tunapitisha Itifaki hii, lazima tutamke bila kipengele kile cha kutoa mimba angalau Mwanasheria kasema, ninaomba itamkwe hivyo ili iwe *clear*, kwa hiyo, naomba mwongozo wako.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, nadhani asubuhi hukuwepo. Ufafanuzi wa kisheria umetolewa, kwa hiyo, tunaendelea kujadiliana, hakuna utata wowote. Tumepewa ufafanuzi mzima na AG kuhusu suala hili na kwamba tunaweza kupitisha hoja hii kama ilivyo na kwamba sheria zinaruhusu vitu ambavyo nchi ile kwa mujibu wa Katiba yake hairuhusu ama sheria zake hairuhusu, haitubani, kwa hiyo tumepata ufafanuzi asubuhi hapa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) wa mwaka 2008 (SADC Protocol on Gender and Development) liliridhiwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, hoja hii imeshaungwa mkono. Kwa kweli *Protocol* hii ilikuwa inasubiriwa sana ipitishwe na Bunge letu na uzuri katika semina tuliyokuwa tumekaa kule Ubungo Plaza, wiki iliyopita, wajumbe wa vyama mbalimbali walikuwa wanaulizia hii *Protocol*, nadhani Waziri ametimiza ahadi yake alioisema kwamba atawakilisha katika Bunge hili.

Kuhusu usawa wa jinsia, mimi nasema hivi: ‘wanawake msio gope, wanaume msihofu’ kwa nini nasema hivi? Kama tunavyojua joto la uchaguzi linavyopanda na kushukuka, mtu akisikia mwanamke anaenda kugombea Jimbo fulani anaanza kuhofu, mimi nakuambieni atakayekupinga siyo huyu mwanamke aliyoko hapa, watakupinga watu lukuki pamoja na waliopo humu ndani. Kwa hiyo, ndiyo maana nawambia msihofu kwa sababu kupingwa ni kawaida, mtapingwa sio na wanawake tu na wengineo walioko huko mnawajua wenyewe, wengi watakuwepo na jinsi wanavyokuwa wengi ndio vizuri tu, kwa hiyo, ndio maana nasema wanawake wasio gope vivuli kwamba tusitengeneze uadui kati yetu hapa kwamba huyu mwanamke anakuja kugombea kwangu, sio, watakuwepo na wengine. Kwa hiyo, tusihofu wala tusio gope.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kutoa ufafanuzi kuhusu utaratibu unaotumika kuamua ni Muswada upi uende Kamati gani na utaratibu huu siyo kwamba ni hiari ya

mtu isipokuwa unatawaliwa na Sheria na Kanuni za Bunge. Kwa hiyo, napenda kutoa ufafanuzi kuhusiana na mwenendo wa kupeleka Miswada katika Kamati kwa mujibu wa Kanuni zilizotungwa na Bunge kama ifuatavyo:-

Kwanza, Muswada wa Sheria hupelekwa kwenye Kamati na Spika kama isemavyo Kanuni ya 84(1). Inasema hivi:-

“Spika atapeleka Muswada wa Sheria kwenye Kamati inayohusika na Kamati itaanza kuujadili Muswada huo mapema iwezekanavyo”. Mwisho wa kunukuu Kanuni ya 84(1).

Pili, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge toleo la 2007, Kanuni ya 114(14) kwanza imetoa maana ya Kamati inayohusika kwamba ni ile iliyopelekwa Muswada. Kanuni hiyo inasema hivi:-

“Kamati yoyote ambayo Spika atapeleka kwake kwanza Muswada au jambo lingine lolote, itahesabiwa kuwa ndiyo Kamati inayohusika kushughulikia Muswada huo au jambo hilo”. Mwisho wa kunukuu. Kanuni ya 114(14).

Tatu, halafu kwa mujibu wa Kanuni hizi, uamuzi wowote wa Spika kupeleka Muswada kwenye Kamati yoyote, ni halali kwa kuwa amepewa mamlaka ya kufanya hivyo.

Nne, hata hivyo, kwa kuzingatia matakwa ya Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 9(1)(b) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2007, moja ya Majukumu ya Kamati za Kudumu za Kisekta ni kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inayozisimamia, kwa hiyo tunazo Kamati za Kisekta ambazo zinaweza kupewa Miswada ya Sekta zake, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ndiyo inayosimamia Ofisi ya Rais – Utawala Bora kama ilivyotajwa kwenye Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 8(2)(a) kisemacho:-

“Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala itasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:

(a) Ofisi ya Rais:-

(i) Utawala Bora

(ii) Menejimenti ya Utumishi wa Umma.”

Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kwenye Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 8(4), Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama inasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:-

(i) Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa;

(ii) Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki;

(iii) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; na

(iv) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Hivyo, Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni, Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 8(2)(a) na 9(1)(b), hakukuwa na kosa wala tatizo lolote kwa maamuzi ya kupeleka Muswada huo katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa sababu sekta ile ama Wizara hile iko chini ya Kamati hii.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati inayopelekewa Muswada inaweza kuwaruhusu Wabunge ambao si wajumbe wa Kamati au watu ambao si Wabunge kuhudhuria na kushiriki katika shughuli za Kamati kama ilivyo Kanuni ya 114(8) kama inavyosema:

“Bila kuathiri masharti yaliyotangulia ya Kanuni hii, kila Kamati itajiwekea utaratibu wake, na Kamati inaweza kuwaruhusu Wabunge ambao si wajumbe wa Kamati au watu ambao si Wabunge kuhudhuria na kushiriki shughuli za Kamati lakini hawatakuwa na haki ya kupiga kura”. Mwisho wa kunukuu Kanuni ya 114(8).

Kwa hiyo, tarehe 3/11/2009 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, ilifanya kikao cha pamoja na Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kujadili kwa pamoja Muswada huo *Dodoma Hotel*.

Kamati ilikwenda mbali zaidi kwa kuwaita pia wadau mbalimbali waje kujadili Muswada huo na tarehe 15 Oktoba, 2009, Kamati ilialika wadau na waliofika walikuwa ni taasisi zisizo za Kiserikali za *NOLA (National Organization for Legal Assistance)* na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*Legal and Human Rights Centre*).

Kwa hiyo basi, tarehe 30 Januari, 2010, baadhi ya Vyombo vya Habari vimekuwa vikitoa taarifa potofu kuhusiana na kuondolewa na Serikali kwa Muswada wa Baraza la Usalama wa Taifa, kwa kutumia kifungu 87(1) cha Kanuni za Bunge baada ya michango ya baadhi ya Wabunge kuonyesha kutokukubaliana na baadhi ya vifungu katika Muswada huo. Habari hizo za upotoshaji zimekaziwa jana tarehe 2 Februari, 2010 katika gazeti lingine la Mtanzania, Toleo namba 512 lililobeba habari yenye ujumbe usemao “Sitta aikoroga Serikali” na lenyewe likiwa na madondoo kwamba: Apeleka Muswada kwenye Kamati siyo, siri yavuja, Ofisi yake ilionywa ikakataa, Malecela, Ngwilizi, Lubeleje washangaa. Gazeti lingine la Tazama Tanzania, toleo namba 378, nalo la tarehe 2 Februari, 2010 lililobeba habari yenye kichwa cha habari kinachosomeka ‘Spika Sitta achangia kumkwaza Waziri Sophia Simba’.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema ni vizuri magazeti yakatumia Kanuni zetu. Kuondolewa kwa Muswada uliowasilishwa na Mheshimiwa Waziri, Sophia Simba, ni utaratibu tu na wala siyo mara ya kwanza kwa Muswada kuondolewa. Kama itafikia mahali Serikali ikaridhika kwamba wanatakiwa warudi na kuona kwamba inafaa kuchukua hatua kama hiyo, jambo ambalo ni utaratibu wa kawaida ambao hufanyika ndani ya Bunge na kwa maoni yangu ni utaratibu mzuri kwa sababu Serikali inasikiliza watu wake wanajadili nini. Wakiona kama maoni yale hayaelekei basi Kifungu kinamruhusu Waziri kutoa, kwa hiyo, si kosa wala sio kushindwa kufanya kazi. Sasa mkiongeza tena kukoroga na kufanya nini, nadhani mnauza magazeti na siku zote

nimetoa wito kwamba magazeti mtafanya haki kwa wananchi wa Tanzania kama mtatumia Kanuni zetu. Kwa hiyo, mimi kwa maelezo haya, tunasema yale waliyoandika magazeti hawakutumia ufundi wa Kanuni zetu kuandika waliyoandika kilichofanya Serikali kuondoa Muswada si udhaifu wa Waziri au Serikali yenyewe, ni utaratibu wa kutunga Sheria, kwa hiyo, napenda hiyo ieleweke.

Baada ya kusema hayo, hata ratiba zetu wanasema tumehamishia Miswada, ni utaratibu wetu kupanga kazi na inafanywa chini ya Kamati ya Uongozi, kwa hiyo, tumejipangia kwamba leo hii, tarehe 3 Februari tumemaliza hili Azimio asubuhi hii, baadaye saa kumi na moja Waheshimiwa Wabunge mtarudi tutakuwa kwenye Ukumbi wa Msekwa. Katika Ukumbi wa Msekwa tutapewa taarifa au utaratibu wetu wa Kanuni yetu nyingine ya 94 kuhusu Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango. Tumefikiria kwamba tuelewane sisi wenyewe Wabunge, ile Kanuni ilikuwa inataka nini kabla ya kesho baada ya kipindi cha maswali kuingia katika Kamati ya Mipango ambayo tutakaa humu humu ndani. Kwa hiyo, saa kumi na moja mtakaporudi tunarudia kwenye Ukumbi wa Msekwa kwa sababu itakuwa kama ni taarifa au ni *briefing* ambayo mnapewa na Wizara ya Mipango pia na Kamati yetu ya Kanuni za Bunge tulipoingiza kile kifungu maana yake ilikuwa nini kusudi sisi tuelewe na Serikali iweze kujua mipaka yetu ya ile Kanuni. Kwa hiyo, saa kumi na moja, leo tukitoka hapa haturudi Bungeni, tunarudi kwenye Ukumbi wa Msekwa.

Halafu nilikuwa nimetangaza pia kwamba saa saba Kamati ya Maendeleo ya Jamii na kikundi kile cha *Parliamentary Gender Group* wakutane kule *African Dream*, naona wengine wanasema hawakuelewa, kwa hiyo, ni saa saba lakini inategemea kama mtawahi shughuli nyingine hizi za mchana.

Wakati huo huo, nafikiri Kamati ya Uongozi ya Chama cha Mapinduzi inabidi wakutane saa saba na nusu katika Ukumbi wa Spika na wanawake Wabunge wanaobaki ambao hawatokwenda kule, wakutane Ukumbi wa Msekwa, yaani wanawake wote wa Bunge *TWPG*, wakutane pale kuna *briefing* ambazo mnatakiwa kupewa.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge hatuna matangazo mengine, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 6.42 Bunge lilihairishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 4 Februari, 2010 Saa Tatu Asubuhi)

